Kikao cha Tano – Tarehe 17 Machi, 2015

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

Dua

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi naomba kuweka mezani ya Hotuba ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza iliyotokana na Kamati ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza la Wawakilishi yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuweka mezani Hotuba ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2013/2014. Naomba kuweka.

Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Utawala na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka mezani Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2014/2015.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 2

KVZ KUVAMIA ENEO LA KIWANDA CHA SUKARI

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa uongozi wa Kiwanda cha Sukari cha Mahonda kuwa kuna ekari zipatazo 42 walitaka kupanda miwa lakini ekari hizo zimezuiliwa na Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ).

a) Je kwa sababu gani Kikosi cha Valantia Zanzibar kimevamia eneo hilo la uwekezaji.

b) Nini hatma ya Kiwanda katika kutumia eneo hilo. Je, Kiwanda hakina haki ya kutumia eneo lake la uwekezaji.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni. Naomba kumjibu swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, mnamo mwaka 2002 Serikali ilikabidhi matumizi ya eneo alilolitaja Mhe. Mwakilishi na kuwa eneo la kiulinzi na kukabidhiwa kikosi cha KVZ, kuaznisha Kambi ijulikanayo kama Kambi ya Pangatupu ili kuimarisha shughuli za ulinzi kwa maeneo hayo. Eneo hilo limepimwa na kwa sasa si sehemu ya shamba la miwa la Kiwanda cha Sukari cha Mahonda. Na uongozi wa Kiwanda cha Mahonda unaelewa eneo hilo kuwa sio sehemu ya eneo lao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kikosi cha Valantia Zanzibar hakikuvamia eneo la muekezaji wa Kiwanda cha Sukari Mahonda.

(b) Kama nilivyojibu katika suala (a) eneo hilo si la kiwanda na kiwanda hakina haki ya kisheria ya kulitumia eneo hilo. Aidha, maeneo hayo tayari yemeshapimwa na Serikali kwa ajili ya matumizi ya Kikosi cha Valantia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi ni mjumbe wa Kamati ya Fedha, Kilimo, Biashara kiwanda hicho Kamati imeshakwenda kukagua eneo hilo na ikashuhudia mgogoro huo uliokuwepo na hili suala la muda mrefu Mhe. Waziri. Kwa kuwa sehemu hiyo waliwahi kulima miwa na wakavuna haujatokea mgogoro huo, mmechukua hatua gani kama ni Serikali mkakutana na wahusika wale wenye kiwanda kile ili kutatua mgogoro huo na kwamba wale watu wamechukua mbegu kutoka *South Africa* kuzalisha pale na eneo lao limekuwa ni finyu.

Isitoshe wana nyumba 271 wanadai wamepewa nyumba 13, zile nyumba ziko mikononi kwa nani. Hivi kweli tunakaribisha wawekezaji au tunawafukuza wawekezaji.

Polisi wamekodi nyumba zile kutoka mikononi mwao. Kwa kuwa sehemu ile ni Kiwanda cha Miwa asili yake Serikali imetumia vigezo gani kwa wawekezaji wakiwa wanaendelea kulalamika ufinyu wa eneo hilo.

Pili, tangu Serikali kuchukua eneo hilo imechukua hatua gani kukutana na wawekezaji kuangalia utaratibu wa kuwapatia eneo jengine muafaka.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Jaku Ayoub swali lake la nyongeza lenye maelezo marefu lakini lenye maswali (a) na (b).

Kwanza kupitia maelezo yake natambua kwamba yeye ni mjumbe wa Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara nikiwa kama Waziri wa Serikali na mjumbe wa Baraza lako Tukufu. Ni kweli suala hili lilijitokeza kwenye Kamati yao na Kamati nyengine lakini bado naendelea kusisitiza kwamba eneo ambalo kipo Kikosi cha Valantia KVZ Pangatupu kwa sasa si eneo la Kiwanda cha Sukari na Manukato.

Serikali ilipoamua kumkodisha muekezaji tayari ilishafanya maamuzi ya kulitoa eneo hilo kwa Kikosi cha Valantia KVZ. Je tumeshakaa na uongozi wa Kiwanda?

Mhe. Mwakilishi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, na wajumbe wa Baraza nataka niwahakikishie kwamba Wizara yangu imeshakaa na muekezaji kwanza kwa mazungumzo ya muekezaji kutaka kukodi eneo la KVZ kwa ajili ya kupanda miwa. Kwa hivyo hata muekezaji mwenyewe anajua kwamba eneo hilo sasa sio la kwake na kwa sababu taasisi inayohusika kwa maana ya Wizara ya Ardhi tayari imelipima kwa ajili ya matumizi ya KVZ. Kwa hivyo nataka nimuhakikishie kwamba wizara imeshakaa.

Kuhusu suala la nyumba nadhani suala hilo alitafutie utaratibu wa kuliuliza, lakini natambua kwamba ziko nyumba ambazo wanazo Kiwanda cha Sukari, ziko nyumba ambazo bado Serikali haijawakabidhi, lakini Serikali imeunda Kamati Maalum kwa ajili ya kuzungumza na wapangaji waliomo humo ili wazirejeshe Serikalini na Serikali iweze kuwakabidhi nyumba zao.

Jengine je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa eneo jengine. Natambua kwamba Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili inao mpango madhubuti wa kutafutia eneo jengine wawekezaji hao ili iweze kuwakabidhi na Serikali yetu haina nia ya kuwafukuza bali ina nia ya kuzungumza nao ili ielewe matatizo yao na yaweze kupatiwa ufumbuzi ili waendelee kuekeza katika mradi huo wa kuzalisha sukari.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana yaliyotolewa na Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa miongoni mwa madhumuni ya vikosi vyetu hivi ni kuongeza nguvu katika ulinzi wa wananchi na mali zao na kwa msingi huo mule ambamo vikosi hivi vipewa maeneo ni kwa ajili ya kuimarisha ulinzi kwa mfano kama Kikosi cha KMKM huwa kinakaa maeneo ambayo kuna vigezo vya kwamba kuna magendo fulani yanafanywa.

Sasa nataka nimuulize Mhe. Waziri ni kwa vigezo gani ambavyo Serikali imeviona mpaka ikaweka kambi vya vikosi viwili pahali pamoja kule Pujini, Kikosi cha KVZ na Kikosi cha JKU wakati si maeneo ambayo yanashukiwa kuwa labda kuna magendo au uovu fulani unaweza kufanywa kule.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kigezo na sababu ya msingi ni kuimarisha ulinzi ndani ya visiwa vya Zanzibar. Na kwa mujibu wa sheria Rais wa Zanzibar anaunda Idara Maalum kwa ajili ya kazi hiyo na popote pale ndani ya eneo la Zanzibar tunaweza tukaweka kituo ama kambi ya ulinzi kwa sababu ni jukumu la msingi katika Idara Maalum. Kwa hivyo kuwepo kambi mbili au vikosi viwili katika eneo moja si hoja, vinaweza vikawepo vikosi vyote vitano katika eneo moja na zinaweza kambi hata 30 za vikosi hivyo vitano katika eneo moja kutegemeana na haja iliyopo wakati huo.

Nam. 3

Askari wa KVZ kunyan'ganya Wachuuzi wa Samaki Bidhaa zao na Kuwabambikizia Kesi

(Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 21

Upatikanaji wa Fedha katika Kituo cha Mkwajuni TC

Mhe. Panya Ali Abdalla - Aliuliza:

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi za kuwaendeleza walimu wa Kituo cha Mkwajuni TC, ikiwa ni miongoni mwa vituo vinavyosaidia kuwaongezea walimu taalum ili wafanye kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Je, kwa nini kituo hiki hakiingiziwi fedha ili walimu wakaweza kupiga hatua kwa kujiongezea taaluma zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafuno ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake swali lake namba 21 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, vituo vya walimu vina majukumu makubwa ya kuendesha mafunzo ya walimu kazini kutegemea mahitaji ya mafunzo ya kada na zinachangia katika kuimarisha uwezo wa walimu. Hivi sasa tunavyo vituo 10 vya walimu vipo katika sehemu zote za Unguja na Pemba, vituo vya elimu vinaendesha shughuli zake kwa kutegemea fedha kutoka sehemu tatu kuu. Nazo ni mchango unaotolewa na skuli, fedha zinazotengwa katika bajeti ya Serikali na fedha za mafunzo zinazotolewa na wahisani mbali mbali kama vile *UNICEF Global for Partnership Education* na mradi wa TZ 21 ambapo mafunzo yanaendeshwa katika vituo hivyo.

Kwa mwaka 2014/2015 vituo 10 vya walimu vilipangiwa kutumia 6,750,000 kutoka katika bajeti ya Serikali na hadi hivi hakuna pesa yoyote iliyopatikana. Hata hivyo mafunzo mbali mbali yanaendeshwa katika vituo vya walimu kikiwemo kituo cha Mkwajuni kwa kutumia msaada wa fedha za wahisani, kwa mfano kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2014 hadi Disemba 2014 kwa msaada wa *Global Partnership for Education,* jumla ya shilingi 13,064,500 zimetumika kuendesha mafunzo ya aina 4 katika Kituo cha Walimu cha Mkwajuni.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:

Kituo cha Walimu cha Mkwajuni hakijaingiziwa fedha kutoka bajeti ya Serikali kutokana na uhaba wa fedha katika kifungu hiki. Hata hivyo mafunzo mbali mbali yameendeshwa kama vile mafunzo ya takwimu, matumizi ya teknologia ya habari na mawasiliano katika elimu na mafunzo ya mada ngumu za kufundishia. Wizara yangu itaendelea na juhudi za kupatia vituo hivyo vya walimu fedha kwa ajili ya kuendesha mafunzo ya walimu kazini kwa robo hii ya fedha inayokuja.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa hii kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwapatia fedha kituo cha TC Mkwajuni au vituo vyengine vyote vya TC vilioko hapa kama navyo vina tatizo kama liliopo Mkwajuni ni kuwapatia ufanisi walimu wawezi kufanya kazi zao kwa ujuzi zaidi baada ya kupata taaluma jambo ambalo lingeleta mafanikio kwa wanafunzi kuweza na wao kupata matokeo mazuri baada kufundishwa na

walimu ambao tayari wamepata taaluma. Je ni muda gani kituo hiki cha Mkwajuni hakijaingiziwa fedha hizi ambazo zinaweza kuwasaidia walimu kwa kupata mafunzo hayo.

b) Ni lini serikali itawaingizia fedha ili walimu waendelee kupata ujuzi huo katika vituo vyao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza kwenye jibu langu mama kama kwa mwaka huu bado kituo hiki hatujakitilia pesa, na si hiki tu Kituo cha Mkwajuni ni vituo vyote kumi vya Unguja na Pemba ambavyo havijapata pesa. Na nikaelezea tunatarajia kuwatilia pesa ambazo tulitenga katika bajeti milioni 6,700,500 katika robo hii pindi tu Wizara ya Fedha wakitutilia pesa katika kifungu hicho.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kutokutiliwa pesa hizo sio kama zile kazi ambazo zimepangwa na *TC* hazifanyiki. Ni kwamba zinafanyika na kituo chako cha Mkwajuni tu kimetumia zaidi ya milioni 13, 604,500 kwa mwaka huu kwa ajili ya mafunzo mbali mbali ambayo yametolewa katika kituo kile. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti tutajitahidi kadiri ya uwezo wa fedha tutakavyotiliwa na Wizara ya Fedha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kuna msemo, Waswahili wanasema “hoi hoi nacho kilindo” hili suala ni la muda mrefu baada ya kulipeleka niipongeze sana serikali kwa kuchukua juhudi muafaka za kuwalipa wahusika pesa hizi karibu milioni mia moja na thalathini na ushei chini ya uongozi wa Katibu Mkuu kwa umakini wake wa hali ya juu Dkt. Jidawi, naishukuru serikali kwa hilo naomba kuondosha suala.

Nam. 36

Malipo kwa Wasimamizi wa Mradi wa Nyumba za Madaktari

(Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 17

Tatizo la Kujaa Maji Barabara ya Posta – Kijangwani

Mhe. Ali Salum Haji – Aliuliza:-

Kwa miaka mingi eneo la barabara ya mbele ya jengo la Posta Kijangwani wakati wa mvua hujaa maji na kupelekea usumbufu kwa wanaohitaji huduma za posta na nyengine.

Je, wizara imejipanga vipi kumaliza tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa eneo la barabara iliyopo mbele ya jengo la Posta maeneo ya Kijangwani wakati wa mvua hujaa maji ambayo huwa ni kero kubwa kwa wananchi ambao hutumia maeneo hayo kwa shughuli zao mbali mbali. Tatizo hilo linatokana na eneo hilo kukosa mitaro yenye uwezo mkubwa wa kuchukua maji yanayokusanyika hapo kutoka maeneo ya juu kwa vile eneo hilo kimaumbile liko eneo la bondeni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile maji kutoka maeneo mbali mbali yamekuwa yakituama hapo na kwa kuwa jambo hili liko ni mradi tegemezi Wizara ya Miundombinu pekee haiwezi kulitatua tatua hilo. Hivyo, serikali kupitia program ya *ZUSP* chini ya mchakato unaosimamiwa na Wizara ya Fedha mradi ambao uko chini ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum uko katika hatua za kutafuta wakandarasi ili kuweza kuona tunafanya mradi mkubwa wa kujenga mitaro itakayoweza kuondosha huduma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, wizara tumejipanga kwa kushirikiana na taasisi nyengine za serikali kama maelezo ya awali ya hapo juu ili kuondoa tatizo hilo katika eneo husika pamoja na baadhi ya maeneo katika mji wa Zanzibar kwa kupitia mradi huo utakaojenga mitaro maeneo kadhaa katika mji wa Zanzibar.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa eneo la posta nakubali ni eneo la bondeni lakini eneo hili lilikuwa limemalizikia mpaka Kariakoo na kwa muda mrefu eneo la Posta na Kariakoo ni maeneo yote ambayo yalikuwa yakijaa maji, lakini cha kushangaza tu baada ya kujengwa uwanja wa Kariakoo eneo lile wameenda kulifanyia marekebisho ya dharura. Je, wakati tunasubiri huo mradi na mradi ambao haujulikani lini utatekelezeka haoni kuna haja ya kutafuta njia za dharura kuweza kuondosha maji yale.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tumekiri kwamba eneo lile lina tatizo na ili tatizo uliondoe kimaumbile eneo lile ndilo linalopokea maji na tumelazimika kutengeneza utaratibu mzuri wa kuwa na mitaro mikubwa na mipana ambapo serikali tayari imeshafanya mchakato wa kuanza kuona namna gani wanaweza wakapata mkandarasi wa kuweza kujenga michirizi hiyo mipana ili tuondoe tatizo. Sasa kwa haraka haraka tunachoweza kufanya sisi serikali ni kuona mitaro ile ile midogo iliyokuwepo tuhakikishe kwamba inakuwa misafi, haina michanga, haina vizuizi ili kuona hata kwa kasi ndogo maji yanayotuama pale yanaweza kutiririka kuelekea katika mitaro mikubwa ili kuelekea upande wa pwani kwa madhumuni wa kuondoa usumbufu ambao unajitokeza kwa kutuama kwa maji katika eneo tunalolizungumza.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi asubuhi ya leo kuweza kumuuliza swali Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yake mazuri sana Mhe. Naibu Waziri ni kwamba mara nyingi sana serikali tunakuwa tunasema tuko mbioni mbioni au tuko kwenye harakati au tunasubiri michoro ikamilike. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kuna jambo ambalo linakuwa lina athari kwa wananchi na hasa katika mambo ya mripuko wa maradhi na kipindi hiki cha mvua.

Je, Mhe. Naibu Waziri pamoja na kusema kuwa utasafisha kutoa michanga lakini hilo jambo kubwa ambalo ulilowe ka katika mikakati ya serikali, ni lini wananchi waweze kutegemea kusikia kauli yao kuwa hili jambo serikali imetamka siku ambayo itaweza kufanikishwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, jambo hili linahusisha taasisi zaidi ya wizara moja, kwa hiyo sisi kama Wizara ya Miundombinu tutahakikisha kwamba tunakaa na wenzetu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum kwa kupitia Taasisi yao na Manispaa pamoja na washirika wengine ili tuweze kuona kwa kiasi gani kama serikali tunaweza tukanusuru kipindi hiki cha mvua maji yale yasituame eneo lile, ili kuweza kuwakinga wananchi na majanga ambayo Mhe. Mwakilishi ameyatolea tahadhari.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwanza kabla ya kuuliza maswali madogo tu ya nyongeza mawili, nataka nichukue fursa hii kumpa pole rafiki yangu Naibu Waziri kwa kuumwa tokea jana. Kwa kuwa nchi yoyote duniani barabara zinajengwa kwa kuzingatia ramani na mipango miji, kitu gani kinachokuja mwanzo kati ya barabara au mtaro.

La pili kutuwama kwa maji katika maeneo ya barabara kunajenga barabara au kunabomoa barabara.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ameuliza maswali mawili ambayo yote kwa pamoja swali la barabara au mitaro kipi kinakuja kwanza. Ni kwamba utaratibu wa ujenzi kwanza mnafanya *design* katika *design* mnayoifanya ndio itaonesha kama kuna haja ya kujenga mitaro ama hakuna haja ya kujenga mitaro. Inapobainika kwamba kuna ulazima kujenga mitaro maana yake mnajenga barabara baadae mkimaliza kujenga barabara mnajenga mitaro ama mnaweza mkajenga wote *simultaneously*.

La pili analouliza kwamba maji kutuama yanajenga barabara au yanaharibu barabara. Ni kwamba maji yakituama barabarani yanaharibu barabara na maji ya mvua ndio adui mkubwa wa barabara.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana niendelee kusema msemo ule ule tena mara ya pili “hoi hoi nacho kilindo” nimpongeze waziri dhamana wa wizara hii kwa juhudi alizofanya badala ya kujifungia mlango akaanza kusaini ma-*file* yale, nilimshukuru sana Waziri Ramadhan Abdalla Shaaban kwa jitihada zake kwa wananchi anazozichukua. Kwa hiyo, naomba swali hili nalo likae upande tuliondoshe.

Nam. 52

Wananchi Kutopatiwa Hati za Ardhi kwa Wakati

(Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 70

Dhamira ya Kujengwa Studio za Rahaleo

Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Aliuliza:-

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa nia njema alijenga Studio ya Rahaleo kwa ajili ya wasanii waliopo Zanzibar wakiwemo wasanii wa maigizo, *Zenj Flava,* sambamba na wasanii wengine wa taarab, akiwa na dhamira ya kuinua vipaji vya wasanii ili kuona kwamba kazi za jasho lao zinakua sehemu ya ajira yao.

(a) Ni kwa namna gani studio ile imewasaidia wasanii wetu hawa wa *Zenj Flava* kuinua vipaji vyao kama vile studio ya *Tanzania House of Talent (THT)* ya Tanzania Bara iliyoanzishwa na Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete inavyowasaidia vijana wa *Bongo Flava* na hata wale wa *Bongo Movie* vipaji vyao na hatimae kuwapatia umaarufu mkubwa sambamba na kutwaa tuzo kubwa za ndani na nje ya nchi yetu.

(b) Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imewasaidia vijana wangapi kuinua kazi zao kwa lengo la kuhakikisha kuwa kazi zao zinaingia sokoni na hatimae kuwasaidia vijana hao angalau kupata kifuta jasho cha kazi zao hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa nia njema ilijenga Studio ya Rahaleo kwa ajili ya wasanii waliopo Zanzibar, wakiwemo wasanii wa maigizo ya *Zenj Flava* na wasanii wa taarab ikiwa ni dhamira ya kuinua vipaji vya wasanii ili kuona kwamba kazi zao na jasho lao zinakua sehemu ya ajira.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ni kuona kwamba wasanii wanainua vipaji vyao kwa kuweza kupata ajira kuwasaidia kwenye maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, hatua ya kurikodi haijafikiwa kutokana na kuchelewa kufika vifaa vya kurikodia. Hata hivyo, vifaa vimeshawasili nchini vikiwepo Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume. Hatua itakayofuata ni kuvifunga na kuanza kazi na wasanii wetu wa maigizo wa *Zenj Flava* na taarab wataanza kufaidika kwa kupitia kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inaendelea kuwasaidia wasanii wote waliosajiliwa katika Baraza la Sanaa kuwapatia mafunzo ya kuendeleza sanaa zao kwa semina kwa madhumuni ya kuwapatia ujuzi wa kazi zao katika tasnia zao.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri naomba nimuulize swali kwamba kwa kuwa amekiri kwamba vifaa vya kurikodia vimechelewa kuingia nchini na kwa hivi sasa amesema kwamba vifaa hivyo tayari vipo nchini ila tu bado havijafungwa. Ni lini vifaa hivyo vitafungwa ili wasanii wapate kurikodi kazi zao kama nilivyosema ili wapate na wao kufaidika na jasho lao.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi lakini kama nilivyoeleza kwenye swali la msingi ni kwamba vifaa vimefika na sasa hivi tunasubiri mafundi waje wafunge kwa ajili wanatoka mbali, wanatoka Uingereza sasa hatuwezi kufunga kwa mafundi waliopo hapa Zanzibar kwa sababu *studio* ile imejengwa kwa ajili ya wasanii wetu wa Zanzibar.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (b) na (b).

a) Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba vifaa hivi viko Uwanja wa Ndege, swali langu ni kwamba ni sababu gani mpaka leo vifaa hivyo havijatoka Uwanja wa Ndege.
b) Katika majibu yake pia amesema kwamba wizara imeweza kufanya mafunzo na warsha mbali mbali kwa wasanii wetu. Je, ni mafunzo mangapi yaliyofanywa kwa wasanii wetu na warsha ngapi zilizofanywa kwa ajili ya wasanii wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nitaanza kwa swali (b). Mhe. Mwakilishi sasa hivi kuanzia mwaka jana tulitembelea Mkoa wa Kaskazini Pemba ili kuweza kutoa mafunzo ya wasanii pamoja na wasanii wa kazi za mikono kama mikoba na mambo mengine ambayo yanahusiana na wasanii.

Pia ni vikundi ambavyo viko Mkoa wa Kaskazini Pemba na Kusini Pemba, na Kaskazini "A" na Kaskazini "B". Mhe. Mwakilishi nakuomba sana na wewe kama una kikundi chako pia tushirikiane na wizara ili tuje tuwape mafunzo ya usanii wa mambo mbali mbali ambayo yamo kwenye visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mheshimiwa katika swali langu la mwanzo niliuliza alijibu kwamba vifaa vipo Uwanja wa Ndege nikamuuliza kwamba ni kwa sababu gani mpaka leo havijatoka vifaa hivyo katika Uwanja wa Ndege bado sijapata jibu hilo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ni kwamba vifaa vimefika wiki iliyopita taratibu za kuvitoa zinaendelea mafundi wanatarajiwa kufika mwishoni mwa mwezi huu kutoka Uingereza Kampuni ya *SONY*, Kampuni Tanzu ya *on air* vitafika hapa kuja kuvifunga na tunategemea mwanzoni mwa mwezi nne *studio* itakuwa tayari.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, tunakuwa tunauliza swali halafu unajibiwa jibu ambalo lilokuwa kama ni *simple* sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa tunapouliza swali inakuwa majibu yake yanakuwa *very simple* sijui inakuwa ni tatizo gani.

Mhe. Mwenyekiti, tulichouliza kuwa vitu viko Uwanja wa Ndege na Mhe. Waziri amejibu kuwa hivi sasa hivi vitu hivyo vina wiki moja vipo Uwanja wa Ndege, ni kwa sababu zipi mpaka leo hii wiki moja kuwa vyombo vimeshindwa kutolewa tunaambiwa jibu la kungojea wataalamu wakati kwanza tutoe vitu na baadae tulete wataalamu.

Pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, jibu jengine la (b) ni lini mheshimiwa ataahidi wasanii hawa kwa sababu sanaa sasa hivi Zanzibar imeanguka kwa hali kubwa sana kutokana na kukosa *studio* ya kisasa kama wenzetu walivyopata. Ni lini Mhe. Naibu Waziri atafunga baada ya vitu hivyo kutolewa kama wiki mbili au mwezi mmoja ni lini basi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nadhani labda Mhe. Mwakilishi hakusikiliza vizuri au hafahamu vizuri nilichoeleza, ni kwamba vifaa vimefika wiki iliyopita Uwanja wa Ndege, taratibu za kutoa vifaa bandarini au Uwanja wa Ndege sote tunazielewa sio kwamba ukifika unavitoa. Kila mmoja anaelewa kama mzigo umefika lazima kuna taratibu zinafanywa, tupate pesa, tufanye mambo mengine halafu unavitoa unaviweka *store*, na hili tunaliendeleza, tunategemea wakati wowote leo au kesho vifaa vitatoka. Suala la lini nimeshaeleza kwamba mwisho wa mwezi wahandishi watakuja kutoka Uingereza baada ya hapo wata-*test* kama kila kitu tayari *studio* itatumika. Kwa hivyo, kumwambia lini siwezi kumwambia kwa sababu hayo ni mambo ya kifundi, naweza kusema keshokutwa lakini ikawa bado. Kwa hivyo, ninachomwambia kwamba mwisho wa mwezi wahandisi watakuja watafunga vifaa baadae tutaangalia kama viko *okay* watavi-*test*, watatukabidhi, wakishaviangalia baadae *studio* itaanza kufanya kazi, lakini kumwambia lini tarehe ngapi hiyo nitashindwa kufanya kwa sababu baadae nitalidanganya Baraza ni mtihani. Sasa namwambia hivyo, tumo katika *process* ya kulimaliza suala hili.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, 2015

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe jana tulimaliza michango ya Wajumbe kwa hiyo leo tutampisha Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora kufanya majumuisho. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kwa mara nyengine tena kuweza kufanya majumuisho ya michango ya Waheshimiwa Wajumbe kama walivyochangia Mswada wetu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Miradi ya Maridhiano Nam. 1 ya mwaka 1999 na kutunga sheria mpya kwa ajili ya kuanzishwa na kuendesha mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote asubuhi ya leo tumeamka salama na sisi tulijipinda kweli kweli jana usiku mpaka saa nane kujaribu kuziweka sawa hoja zao, ili tuweze kuwajibu au kutoa ufafanuzi kwa pale walipotuuliza. Lakini naomba nitoe shukurani za kipekee kabisa kwa Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata kuchangia ndani ya ukumbi na wale ambao hawakupata najua ilikuwa ni tatizo la muda tu, lakini wangependa kuchangia.

Kwa ujumla tunashukuru sana kwamba hili wazo letu la sheria hii ya mashirikiano limekubalika na kulikuwa na maswali ya hapa na pale, moja mawili na ushauri na maelekezo. Hayo maelekezo na ushauri wa kufanya sheria yetu iwe bora zaidi tumeyachukua na wale waliounga mkono moja kwa moja tunashukuru. Lakini hata wale ambao hawakuunga mkono wachache tu na walisema mpaka wajibiwe, tutawajibu na tutajitahidi tuweke sawa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwa ujumla tu hili alilizungumza sana Mhe. Mohammed Haji Khalid kwamba miswada yangu mara nyingi inakwenda ikirejea. Sio kwamba inakwenda ikirejea hapa ukumbini haujaja hapa ukarudi, isipokuwa kama utapeleleza na yeye alikuwa Mjumbe wa Kamati yetu kwa kweli miswada yangu mara nyingi inakuwa migumu na inagusa maslahi, inagusa watu wenyewe, inawagusa Waheshimiwa na unajua tena mambo yanapowagusa watu, Waheshimiwa, jamii kwa kweli siku zote mambo yale yanakuwa ya kubadilishana mawazo lakini ndio demokrasi. Tunabadilishana mawazo ukumbini hapa lakini mwisho wanashauri na sisi tunakubali mwisho tunapitisha.

Kwa hiyo, sio kama wagumu tu, hatuko wagumu isipokuwa penye kutetea yale masuala ya msingi na ile dhana yenyewe lazima tuitetee. Kwa sababu ukiibadilisha ile dhana yenyewe ule mswada unaupotosha, kwa hiyo hatuko wagumu. Kwenye ma-*group* yetu, wataalamu wetu tunachuana kweli kweli, sasa pale ambapo tunafika kwamba hatukubaliani kwa kukubaliana ndio demokrasi hiyo, tunakuja ukumbini hapa tunabadilishana mawazo lakini hatimae mswada unapita. Kwa hiyo Mhe. Mohammed Haji Khalid nitakuomba tu kwamba hiyo ndio demokrasia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba niwatambue wale wote waliopata nafasi ya kuchangia mswada wetu. Kwanza naomba nianze na Kaimu Mwenyekiti, Mhe. Shadya.

1. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
4. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
5. Mhe. Marina Joel Thomas
6. Mhe. Saleh Nassor Juma
7. Mhe. Fatma Mbarouk Said
8. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
9. Mhe. Mohammed Haji Khalid
10. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
11. Mhe. Mussa Ali Hassan
12. Mhe. Panya Ali Abdalla
13. Mhe. Subeit Khamis Faki
14. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu

15. Mhe. MohammedRaza Hassanali
16. Mhe. Farida Amour Mohammed
17. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
18. Mhe. Abdi Mosi Kombo

Waheshimiwa tunakushukuruni sana kwa michango yenu, maswali yenu, mawazo yenu ya kurekebisha mswada wetu na kwa kweli niseme yametusaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza na hoja alizotoa Mhe. Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mhe. Shadya Mohammed Suleiman alisimama kwa niaba. Kwa kweli Mhe. Shadya tunamshukuru sana kwa maoni ya kamati na pia niwashukuru Mhe. Makame Mshimba Mjumbe wa Kamati, Mhe. Saleh Nassor Juma, mjumbe, Mhe. Subeit Khamis Faki kwa kutilia mkazo mengi ambayo tulizungumza na tukakubaliana na yale ambayo kidogo walihisi hatukuyakazia wao wakayakazia ukumbini. Kwa kweli tunawashukuru sana pamoja na Mhe. Mussa Ali Hassan.

Mhe. Shadya Mohammed alizungumza kifungu cha 9(3)(c), kifungu cha 38(5), kifungu cha 38(6). Kamati ya wataalamu na kubwa lile la kuingiza wajumbe wawili kutoka sekta binafsi katika kifungu cha 14(1). Takriban hili Waheshimiwa Wajumbe wengi waliogelea katika suala hili au katika fikra hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, kamati ya wataalamu ni kamati ya kudumu ambayo inafanya kazi kwa kuzingatia taratibu za kiserikali, katika kutunza siri zinazohusiana na taarifa muhimu za miradi. Hivyo, kamati ya wataalamu inatakiwa ibakie na wataalamu kutoka sekta ya umma tu, kwa sababu zifuatazo:

Kwanza, kulinda siri ambazo zitatolewa na washirika binafsi, tunahisi wakiingia sekta binafsi mule kama wajumbe wa kudumu basi wanaweza zile siri wakazitoa katika ushindani wa miradi husika.

Unajua kuna *competition* sasa wakiwemo wale kuna *conflict of interest* sasa huo ndio wasiwasi wetu mkubwa. Lakini sio kama tumekataa wasiwepo, tumetafuta mbinu humu tumewatia tutazungumza baadae wapi tumewatia. Kwa hiyo ile dhana ya ushirikishwaji tumeikubali na wao watashiriki lakini sio wa kudumu moja kwa moja na kwa sababu kubwa kwamba, miradi ile itakuja mfano leo mradi wa mafuta, kesho wa barabara, kesho hospitali, kesho wa kilimo, kesho mwengine.

Sasa tukiwatia wale wa sekta binafsi mule moja kwa moja wakiwemo muda wote tuna wasiwasi kidogo wataweza kuhodhi baadhi ya mamlaka na unajua tena mambo ya biashara yana ushindani.

Sasa tumetoa kipengele huku nitakisema baadae, ambapo tumetoa fursa hizo nafasi walizosema na wataingia lakini kama waalikwa na watakuwa na *role* ile ile kama wengine. Sasa hivyo sio kama tumekataa tunaitenga, hatuitengi sisi ndio serikali tuliosema tuwaite sekta binafsi tufanye kazi nao pamoja na tunaishukuru; tumefanya vikao vingi katika *Zanzibar Business Council,* tumebadilishana mawazo na *NGO's*, tumebadilishana mawazo pamoja na washirika wengine mpaka tulipofika hapa.

Hayo sio mawazo ya serikali peke yao, wao wenyewe wafanyabiashara wakasema kweli tumekubali kwa kuepuka hii migogoro. Kwa hiyo hili wazo sio kama tuliunda hapa tu, tumeanza nalo mbali na wao wametuunga mkono moja kwa moja kwa wazo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kuepusha migogoro ya kimaslahi miongoni mwa wawekezaji binafsi hii inaweza kutokea, endapo kamati hii itamuingiza mjumbe kutoka sekta binafsi ambaye hahusiani na miradi inayojadiliwa na kuwaacha wawekezaji binafsi ambao wanahusika na mradi huo bila kuingizwa katika sekta hiyo.

Sera ya *PPP* ambayo imejadiliwa na wadau wengi kama nilivyosema wakiwemo sekta binafsi na taasisi mbali mbali za kiraia imejadiliwa na wameshawishika na ushauri wetu.

Mhe. Mwenyekiti, sababu nyengine kubwa pia ni kuepusha migogoro ya kimaslahi baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ambayo inaweza kutokea kama ataingizwa mjumbe kwenye kamati hii kuwa wa kudumu, yeye kwamba atatetea maslahi zaidi ya mtu au kikundi cha watu bila ya kuzingatia maslahi ya jamii ambayo ndio inaizingatia

zaidi. Serikali imeona kuwa ushiriki wa sekta binafsi ni muhimu tumekubali na tumeuzingatia. Sasa naomba nisome moja kwa moja kile kifungu kama tulivyokirekebisha kwenye ukurasa wa 361 kifungu cha 14(2).

"Kamati ya Wataalamu inaweza kumwalika mwakilishi wa Sekta ya Umma ambae ni wenye mamla ya utekelezaji wa miradi iliyobuniwa kwa mfumo wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, manunuzi au makubaliano ili wawe wajumbe wa muda wa kamati ya wataalamu".

Sasa naomba niongeze pale, "kamati ya wataalamu inaweza kumualika mwakilishi wa sekta ya umma na mwakilishi wa sekta binafsi, ambao ni wenye mamlaka ya utekelezaji wa miradi iliyobuniwa".

Kwa hiyo, nafasi zitakuwepo hapa kwa watu wa sekta binafsi kuja kujadili, kuzingatia kadiri ya ile hali inavyoruhusu basi wataalikwa hakuna wasiwasi kwamba hawatashirikishwa. Sisi ndio wenye dhana hii kwa hiyo moja kwa moja hilo wazo lao Waheshimiwa hatukulipinga, lakini tumeona kwa ule wasiwasi niliosema wasiwemo moja kwa moja kwenye ule utaratibu wa kiserikali kidogo, unajua mambo ya siri mambo haya kidogo watakayaondoa. Huo ndio hasa mtizamo wetu.

Hii pia imezungumzwa kwa uwazi katika sera, sera ambayo tumeshaipitisha kwa sasa imezingatia hivyo. Kwa hiyo hilo tumehisi tusiende kinyume na sera na nafikiri *copy* za sera ile Waheshimiwa katika semina mmeipata naomba tuisome na tuizingatie. Najua kuwa juzi kwenye semina hamkupata muda mkubwa lakini imeelezwa kwa ufasaha kabisa sababu na mwelekeo wa suala hili. Kwa hiyo nakuombeni sana Waheshimiwa Wajumbe ilivyokuwa hiki kitu kipya tunaanza basi tukubaliane hapa.

Kenya kweli wao wameingizwa lakini lazima tutizame uchumi wa Kenya na wao walivyoendelea, wao wako mbali kabisa na wao walianza zamani, lakini na wao wameona wawatie kwa sababu ya misingi yao, uchumi wa Kenya mpana sana. Sisi ndio tunaanza na udogo wa nchi yetu tunaujua.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Shadya Mohammed pia alisisitiza suala mafunzo kwa wafanyakazi wa Kitengo cha *PPP*, wadau mbali mbali wakiwemo masheha na wananchi wengine. Nakubaliana naye kwamba kwa mtizamo wetu hii dhana ya *PPP* ni mpya kwa serikali na hapana budi lazima tujenge uwezo kwa wadau mbali mbali. Huu utakuwa ni mchakato endelevu katika mambo ya *PPP*, hivyo muamko na ufahamu wa *PPP* utaimarishwa kwa wadau ili kurahisisha utekelezaji wa sera ya *PPP*. Vile vile kuna umuhimu wa kujenga uwezo katika taasisi za umma na maafisa wa umma, sekta binafsi, watumiaji na wadau wengine.

Mhe. Mwenyekiti, mambo haya yote yametiliwa mkazo katika sera ya *PPP*. Vile vile sera imetilia mkazo kuwa na mkakati wa mawasiliano ndani ya idara ili waweze kuelimishwa wadau mbali mbali kupitia vyombo vya habari vikiwemo magazeti, televisheni, redio na majarida mbali mbali na pia katika mtandao.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema tunamshukuru Mhe. Shadya, kaimu mwenyekiti wa kamati na mengi kama alivyozungumza yeye mwenyewe ya michango yao tumekubali na tumebadilishana mawazo kwa ufasaha kabisa, kama kawaida mpaka tumeafikiana na kukubaliana mswada uje bondeni.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali, tunamshukuru kwa mchango wake na alisema kwamba sheria imekuja wakati mzuri na ipo haja ya serikali kuongeza nguvu kwa sababu yenyewe imeshindwa. Mhe. Abdalla Mohammed serikali haikushindwa kutekeleza majukumu yake, bali lazima tutambue kwamba mahitaji ya fedha ya kuendeleza miundombinu na kutoa huduma kwa ufanisi yanazidi kuongezeka. Vile vile bajeti ya serikali pekee haitaweza kukidhi mambo yote, hivyo serikali imeamua kukabidhisha sekta binafsi yenyewe kusaidiana na serikali kwa njia ya *PPP* ili kuleta ufanisi kwa kutoa huduma na kuweka miundombinu kwa wakati.

Dhana hii inatambulika na kutekelezwa duniani na nchi mbali mbali kama tulivyotoa mifano Kenya, Singapore na kwengineko. Sisi tumechelewa lakini hatukuchelewa, "chelewa ufike", twende taratibu kwa mpango mzuri, siku zote kupanga ni kuchagua.

Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa pia alisema mradi wa reli kuondolewa kwa Zanzibar katika jedwali namba 1 badala yake uwekwe usafiri wa nchi kavu na usafiri wa baharini. Tumebadilishana mawazo na Mhe. Abdalla Mohammed kabla sijafika hapa, nilichosema hasa yeye alitaka ule upangaji kwanza ije hii ya mawasiliano mengine kama viwanja vya ndege au ndege, meli na treni ndio ije baadae, ndio hasa alivyokusudia sio kama anai-*rollout* reli. Kwa

sababu nilimwambia kwamba lazima tukumbuke reli ya Unguja hapa ilikuja kunako miaka ya mapema huko, ilianza kutoka Mkunazini mpaka Bububu na nyengine ilianza Kiungani skuli tulikosoma kule mpaka leo njia ya mawe yale yaliokuwa inakaa reli yapo na inasemekana ndio reli ya kwanza katika Afrika Mashariki na Kati Wazungu walipofika.

Kwa hiyo, wakati huo kwenda Bububu walikuwa wanasema inachukua bidhaa kupeleka Bububu, magari ilikuwa unayahesabu kama yapo moja au mawili lakini wakaona bora reli.

Kiko kitabu kimoja cha *Coastal Air* wale wametoa mpaka picha na reli yenyewe inavyosukuma, nilitaka kuja nacho lakini nimeghafilika sikijui nimekiweka wapi. Kwa kweli alichokusudia hasa Mhe. Abdalla Mohammed ni hivyo na kama hivyo basi tunakubaliana naye. Pia amekubali baada ya kubadilishana mawazo na yeye.

Pia alisema matumizi ya sheria yaliyomo katika kifungu cha 45(1). Makubaliano baina ya *PPP* kwa mujibu wa kifungu cha 45(1) yatafanywa kwa sheria ya Zanzibar, isipokuwa ndani ya makubaliano ikiwa tume itanukuu kifungu ambacho kinazungumzia sheria ya nchi nyengine kwa mfano, Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutekeleza mambo ambayo yanahusu mambo yaliyokuwemo katika sheria hizo, ndio hayo sheria inaruhusu kutumia sheria hiyo Afrika Mashariki. Kwa ufupi labda itajwe *unless otherwise*, lakini kwa kweli tutatumia sheria ya Zanzibar.

Halafu kwenye kifungu cha 45(2) alitaka ufafanuzi zaidi. Hiyo iliyokusudiwa kuwa mwekezaji binafsi kuwa na hisa yake na wafanyabiashara wengine watakuwa na uhuru wa kuchagua sheria wanazozitaka kutokana na mahusiano yao kama kikundi na sio miradi ya *PPP*. Sote tunajua tukisema hisa, yuko na Mheshimiwa mwengine alitaka kujua hasa nini maana ya hisa. Hisa ni kama *share*, yaani mimi ninachangia hisa tuseme mradi ule una asilimia mia moja huyu anachangia 20, yule 10, yule 15 hizo ndio hisa na wana *right* nazo, alikuwa kapteni aliyetaka kujua. Hizo una *right* nazo mwenyewe hasa ndio maana yake na unavyoidhibiti ile mali basi unadhibiti kwa *percentage* fulani kile ndio chako.

Kwa hiyo, siku zote hatwendi sambamba mwengine ana 80, mwengine 20, mwengine 10 na yule mwenye nyingi ndio mwenye uwezo, ndiye anayeshika mpini, akisema mimi napunguza hisa zangu anataka kuuza basi lazima awe na *say* kubwa. Lakini pia hawezi kuvunja mradi kwa sababu tu ya yeye ana nyingi mwengine ana ndogo. Hili nafikiri wafanyabiashara, sote wafanyabiashara tunafahamu hasa kinachokusudiwa.

Mhe. Abdalla Mohammed pia alitaka kwenye kifungu cha 10(1), alisema kinazungumza idara tu. Fedha binafsi ya mwekezaji haitachunguzwa na Kitengo cha *PPP* wala kamati ya wataalamu, fedha binafsi zitapita njia halali na zitazotambulika kisheria. Mfano Benki, Bima au njia nyenginezo zinazotambulika kisheria na hakutakuwa na njia za mkato au uwajibikaji katika masuala yaliyotajwa kwenye fungu namba 10 lazima taratibu za nchi zifuate pamoja na kutumia Benki, Bima na njia nyenginezo.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad tunakushukuru sana kwa *philosophy* yako kubwa sana na hasa uliyotaka utatuzi wa migogoro utafanyika na Idara peke yake au Kamati ya Wataalamu pia itahusika. Kwa kweli Idara ya *PPP* itakuwa inashughulikia migogoro inatokana na miradi midogo ikiwemo ile iliyoanzishwa katika Serikali za Mitaa.

Aidha, Kamati ya Wataalamu kutoka na sheria hii haitakuwa na mamlaka ya kusuluhisha migogoro . Lakini mswada huu katika kifungu cha 67 umetoa usuluhisho wa migogoro. Hivyo uwezo wa kutatua migogoro kwa kiwango cha idara itakuwepo kutokana na kwamba idara itakuwa imeimarishwa.

Kwa hiyo, Kamati ya Wataalamu haitakuwa na *roll* hiyo kwenye fungu la 67 imelezwa wazi wazi migogoro itatatuliwa vipi. Ukasisitiza kwamba usimamizi wa miradi ni jambo muhimu katika utekelezaji wa sheria. Ni kweli kabisa ushauri wako huu ni mzuri na tunauchukuwa kuufanyia kazi. Lakini hapa hivyo Idara ya *PPP* na Taasisi inayotekeleza miradi ya *PPP* ndio mismamizi mkubwa wa miradi ya *PPP*.

Mhe. Marina Joel Thomas tunakushukuru sana kwa kuunga mkono hoja na hasa ufafanuzi ulioutoa katika kifungu kile cha 14 kwenye (1) tunakushukuru kwa ufafanuzi ule na kuunga mkono hoja moja kwa moja. Suala la elimu kwa wadau pia umelisema Mhe. Marina Joel tunakushukuru na kama nilivyosema ushauri wako tumeuchukuwa na tutauzingatia.

Mhe. Hussein Ibarahim Makungu uliuliza je, Sekta Binafsi inaweza kwenye mikataba na ikishirikiana na serikali katika miradi iliyopo kama vile *ZECO*. Mhe. Mwenyekiti, serikali inaweza kuingia kwenye mikata katika miradi iliyopo inaendelea iwapo inaona iko haja kufanya hivyo miradi ya mashirikiano inaweza kuwa ni mradi wa serikali ambao unaonekana kama utatekelezwa kwa njia ya *PPP* kutakuwa na ufanisi zaidi. Miradi ya aina hii huitwa *Brown Field Project* ama ile miradi ambayo muwekezaji ambayo muwekezaji anaanza unaitwa *Green Field Project*.

Mhe. Mohamedraza Hassanali tunakushukuru kwa michango yako na kubwa ulizungumzia yale mapungufu ya sheria ambayo tunapendekezwa ifutwe ile ya Maridhiano ya namba 1 ya mwaka 1999. Haya nilipokuwa natoa utangulizi nilisema lakini si vibaya kuyarudia tena kwa kutoa ufafanuzi zaidi. Tulisema kwamba miongoni mwa upungufu wa sheria hiyo ile ya namba 1 ya mwaka 1999 ni kama ifuatavyo:-

(1) Sheria hiyo imetungwa bila ya kuwepo Sera ya *PPP*
(2) Haikuweka utaratibu wa uhakika na uwazi katika Zabuni na ufatiliaji wa utekelezaji wa miradi. Vile vile haikueleza kwa uwazi majukumu ya kitaasisi na dhamana zao pia haikuweka utaratibu unaolewaka katika kusuluhisha migogoro baina ya washiriki. Halkadhalika haikuzingatia kuazishwa kwa mfako wa kuendeleza mradi wa *PPP*.

Aidha, sheria hii iko kimnya hiyo sheria namba 1 ya mwaka 1999 katika maeneo muhumu yafuatayo:-

(1) Miradi inayoasisiwa na muwekezaji kama ilivyo katika Rasimu Sera.
(2) Ushiriki wa Serikali za Mitaa ambao ni muhimu katika utekelezaji wa mifumo ya *PPP* sheria hii iko kimnya.
(3) Ugharamiaji wa matayarisho ya miradi ikiwemao tafiti ya awali na tafiti nyengine pamoja na kuwaajiri wataalamu washauri na waendelezaji miradi yaani *Technical Intersection Adviser*.

Mhe. Ismail Jussa na wewe tunakushukuru kwa pongezi nzuri sana kwa serikali nakushukuru *alhamdulillah* umekuwa mkweli na muwazi kwa wazo hili kuipongeza kwa kuleta mswada huu. Pongezi zako tumezipokea na tumefarajika sana kuona kuwa sheria hii ni miongoni mwa sheria mzuri hapa Zanzibar na vile vile umesifia uandishi tunakushukuru wewe mwenye tunajua mwana sheria muandishi kwa hiyo umetoa pongezi tunazipokea.

Lakini ulikuwa na maswali matatu ambayo nitayajibu haraka haraka.

(1) Je, miradi ya *PPP* Zanzibar haitaathiriwa na matakwa ya Serikali ya Muungano pale Serikali ya Zanzibar itakapoamua kuchukuwa mkopo wa kibenki katika masuala ya dhamana.

Nataka kukwambia Mhe. Ismail Jussa kwamba bado hivi sasa tunaendelea kupata mikopo yaani kuna dalili mikopo yetu kupitia katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama ulivyo utaratibu wao ndio dhamana bado tunaendelea. Lakini hii haitofanya Zanzibar kukosa dhamana katika miradi mkubwa *alhamdullah* hatukatai, urasimu upo na huo ndio tunaupigia vita kutokana na makero ya Muungano, lakini hatimae mwanzo tulikuwa hatuna fursa hizo lakini leo *alhamdulillah* fursa hiyo ipo na tuna- *negotiate* wenyewe kama ulivyosema mimi nilikuwa Waziri wa Fedha nadhukuru nimemwachia Mhe. Omar Yussuf Mzee na yeye anaendeleza na sasa imekuwa nyeupe zaidi *alhamdulillah,* sasa tuna- *negotiate* wenyewe bado dhamana.

Mhe. Jussa nimekuchukulia na *copy* naamini unayo lakini kama huna *copy* naomba uisome tu katika Katiba unayopendekezwa tumeweka kwa uwazi kabisa humu kifungu siku kinukuu lakini Zanzibar sasa itapata fursa ya kukopa wenyewe ndio hayo mamlaka tuliyokuwa tunayatafata sasa tunayo. Lakini kwa sababu ni Jamhuri ya Muungano yule tunamwambia tu kwamba tunafanya kiti hiki na hiki na yeye ndiye dhamana. Sasa nakuomba sana mna mengi mazuri humu Mhe. Ismail Jussa na mengine uliyanza mwenyewe kabla hujaondoka Dodoma kwa hiyo nakuomba isome unaweza ukapata ufasa wa jambo hili. Lengo letu ni kuleta tija kwa nchi yetu na wewe kama ni Mzanzibari mkereketwa basi tuungane, tutetee ili Katiba ipite ili tuweze hii mikopo yetu sasa ku- *negotiate* wenyewe vizuri kabisa.

Mhe. Ismail Jussa uliendelea kusema kwamba je, Miradi ya *PPP* Zanzibar haitaathirika na matakwa ya Serikali ya Muungano pale serikali itakapoamua kuchukuwa mkopo wa kibenki katika masuala ya dhamana. Kwa sasa kama nilivyosema tunaendelea kupata dhamana za mkopo katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama ulivyo utaratibu. Kuhusu miradi ya *Exim Bank* ulisema kweli kwamba kwa wakati ule ilikuwa taratibu za kukamika tukakosa. Lakini

hivi ninavyokwambia hivi sasa kuna tayari mazungumzo na *Exim Bank* ya India yanaendelea na wameshafika Zanzibar na tumeshaanza mazungumzo utekelezaji wa miradi ya maji tayari tunao na *alhamdulillah* mambo yanakwenda vizuri na *inshaallah* tutafanikiwa.

Ni kweli nikubali kwamba tulipopata tabu kuhusu misaada mikopo kutoka Jamhuri ya Muungano kwa wakati ule na hata mazungumzo katika mfumo uliopo hivi sasa. Lakini hayo sasa kama nilivyosema kwa kweli mengi yamesharekebishwa. Yamesharekebishwa na hasa kunakoelekea katika Katiba mpya.

Tulizungumzia suala zima la uwazi na uwajibikaji wa miradi mikubwa. Mimi nataka nijikite zaidi huko ulikuwa ni miradi ile niseme ya kiserikali peke yake. Lakini leo tunakuja kwenye miradi ya *PPP* kwa hiyo sifikirii kama udhoefu ule lakini yaliyotokea yale kwa kweli yatajirudia. Ninachotaka kusema kwamba utaratibu mzima wa mswada huu wa *PPP* uwajibikaji wake umezingatia na sheria hii inaonesha wazi wajibikaji ukosema sheria hii yote utaona wazi wazi kwamba tumezingatia sana suala la *transparence* na *accountability* hasa tunapo-*involve private Sector* hakuna mfanyabiashara ambaye anakubali apate hasara hakuna hata mmoja.

Kwa hiyo, kama kulikuwa na matatizo kwa upande mmoja mfano labda kwenye *Public sector* basi ile peke yake kuwa pande mbili mle ni *checking balance* moja anam-*check* mwenziwe anamdhibiti mweziwe. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba utaratibu mzima umezingatia sana suala la uwajibikaji na uwazi.

Miradi yote inaanzishwa na sekta husika ambayo inaingia wenyewe katika makubaliano ya awali tulizungumza kwamba labda Wizara ya Fedha wana- *dominate*. Nataka kusema kwamba aah miradi yote inaanzishwa na sekta husika ile mifano inatoka kwenye wizara mama na wao wenyewe wanaingia katika makubaliano ya awali ya *MOU* na iwapo mradi mdogo wenye thamani ya kufikia chini la dola milioni kumi upatishwa na Kamati ya Wataalamu na baadae kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali *roll* ya Mwanasheria Mkuu ipo tena kubwa na tumeshasema kwamba *MOU* yoyote tusisaini isikubalike bila ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuiona na kuidhinisha kuepuka hiyo migogoro ambayo umeinukuu iliyotokezea kwa siku za nyuma.

Hatua zote hizi zimeainishwa ndani ya sheria hii ukiisoma kidogo najua kidogo najua sasa hivi ulikuwa unakwenda mbio kidogo jimboni kuonana na vijana naona wanakimbia. Sasa ukitulia ukiisoma nafikiri utaona haya yote yamewekwa kwa uwazi kabisa Mhe. Ismail Jussa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusisitiza tu kwamba alizungumza kwamba kwa nini Mkurugenzi wa Mipango, Miji si Mjumbe katika Kamati ya Wataalamu. Hii inatokana na kuwa Katibu Mkuu wa Ardhi atakuwa na dhamana ya kuangalia maeneo yote yanayohusu ardhi. Lakini Mkurugenzi wa Mipango Miji anaweza kualikwa kwa mujibu wa kifungu cha 18 kwenye mabano (2) iwapo itaonekana ipo haja ya kuweza kufanya hivyo mtu yoyote, mtaalamu yoyote anaweza kualikwa kuja ku- *negotiate* kupanga mambo vizuri mpaka tuone lengo letu tumefikia hiyo ndiyo azma Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Ismail Jussa tunakushukuru kwa mchango wako na hizo *observation* ambazo umetupa.

Mhe. Abdallah Juma wa Chonga na wewe tunakushukuru na wewe kwa kweli *observation* zako zilikuwa *very constructive* tumezipokea hasa ile Kamati ya Wataalamu iwe makini sana kubaini wawekezaji wajanja. Ushauri wako huo tumeusikia na tumeuchukuwa.

Pili ulisema kwa nini Wizara ya Fedha igharamie kufanya upembuzi yakinifu wakati gharama hizo zingeweza kutolewa na Mfuko wa *PDF*. Fedha kutoka kwenye mfumo wa *PDF* ni fedha kutoka Serikalini kama ilivyo kifungu cha 20. Wizara ya Fedha itatakiwa kutoa fedha endapo Mfuko wa *PDF* hautakuwa na fedha za kutosha na haja ya kufanya upembuzi yakinifu imetokeza kwa mradi ambao serikali itaona ni mradi wenye tija. Baadae nitatoa ufafanuzi zaidi wa vifungu vyengine vya Mhe. Abdallah Juma.

Mhe. Mohammed Haji Khalid wa Jimbo la Mtambile tunakushukuru kwa mawazo yako mazuri fikira na masuali ulikuwa una mengi madogo madogo na vionjo pia. Umesema zimetajwa sifa za Mkuu wa Idara kwa nini hazikutajwa sifa za Wajumbe waliofanya kazi na Mkuu huyo.

Nataka kusema kwamba Mkuu wa Idara atakuwa ni mtendaji Mkuu na walio chini yake watakuwa wafanyakazi ambao watafanyakazi ambao watafanyakazi chini yake kama ilivyo idara nyengine serikalini, watakuwa na

majukumu kwa mujibu wa taalama zao. Taaluma ambazo zitakuwa na umuhimu katika miradi kama vile fani ya uchumi, sheria, utawala wa umma, uhandisi, fani zilizofanana na hizo.

Halafu ulisema kwamba serikali sio sikivu kutokana na kukataa kubadili msimamo wa kuingiza wawekezaji binafsi katika kifungu cha 14 kwenye (1). Nafikiri nimeshatoa maelezo kwamba sisi wasikivu sana na sie serikali ndio tulioleta hoja hii. Kwa hivyo, fikra hizi tumezichukuwa na tumekubali ushauri wenu hatuipingi hata kidogo *Private sector* lakini tumeona sababu umezieleza kwa nini tunashauri waingie kwenye kifungu cha 14 (2).

Kamati ya Wataalamu ina wajumbe kutoka Serikalini kutokana na majibu niliyotoa ni kwa miradi ya wafanyakazi ni miradi ya umma na kwamba serikali ni sikivu na imekubali kuengeza kifungu kidogo cha pili kiwe namba 3 cha kuwaalika wataalamu wanaotoka nje ya sekta ya Umma kutokana na utaalamu wao kila wanapohitajika. Ushauri wake kuhusu miradi wa Maji na Nishati haukuzingatia miradi wa *PPP* ni shauri la msingi hilo tumelizingatia.

Mhe. Mohammed Haji ulizidi kuuliza kwamba ili nchi iendelee kuna sehemu yanahithajika mambo manne yapatikane watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Bahati mbaya Zanzibar kwa maeneo yako imekosa siasa fasi na uongozi bora. Mimi nafikiri labda Mheshimiwa ulikusidia kutupiga kionjo tu kidogo na kama mwana siasa sikatai. Nataka kusema kwamba nikufahamishe tu labda takwimu huna. Mhe. Mohammed Haji mpaka kufikia Disemba 2014 Mamlaka ya Uwekezaji hapa Zanzibar imethibitisha miradi 593 ya uwekezaji yenye mtaji wa makisio ya dola za kimarekani zipatazo bilioni nne mia tisa sitini na tisa milioni, tisini na tatu elfu, mia tisa arubaini na saba nukta tatu nne, kati ya hiyo miradi 297 yenye mtaji wa makisio ya dola za kimarekani bilioni moja, milioni mia sita, thalathini na sita na sitini mbili mia nane ishirini na moja nukta moja moja, inafanya kazi na iliyobakia iko katika hatua mbali mbali za utekelezaji.

Kwa sasa naomba usikilize sana hapa Mhe. Mohammed Haji Zanzibar ina hoteli 17 za Nyota tano na Hoteli 9 za Nyote nne, Hoteli 43 za Nyota tatu Hoteli 6 za Nyota mbili bila ya kuwa na siasa safi na Utawala Bora maendeleo haya yangepatikana Mhe. Mohammed Haji mimi nakuachia umalize mwenyewe.

Ushauri wa Mhe. Mohammed Haji kuhusu miradi wa Maji na Nishati kuzingatia katika miradi ya *PPP* ni shauri la msingi tumelizingatia na kifungu hicho kwa kweli kimerekebishwa hakikujitokeza katika mswada uliwasilishwa kwenu. Maelezo kuhusu makubaliano ya awali katika kifungu cha 17 kwenye (3) hii inatokana na ugumu wa mswada Afisi yangu kama nilivyosema nimeshalieleza hili kwamba miswada mingi ilikuwa inagusa jamii na maslahi ya viongozi na ile iliyopitishwa hivi karibuni kama maslahi ya viongozi wakuu na viongozi wa kitaifa, maadili ya viongozi, maumbile ya miswada yenyewe kwa kweli ni migumu.

Mhe. Abdallah Juma narudia sasa uchambuzi wa moja kwa moja ulizungumza kwamba Kamati ya Wataalamu iwe makini sana kubaini masuala ya ujanja katika miradi. Ushauri wako tumeukubali na tumeuzingatia. Tatizo la kuruka kwa nambari katika fungu la 25 hoja yako ni ya msingi tunazingatia na marekebisho yatafanywa kwa kushirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu na itakuwa kama ilivyo katika mswada wa kiengereza, mswada wa kiengereza umekaa vizuri kabisa. Kwa hiyo, tutarekebisha tu hili.

Kifungu 17(1) neno bila ya mipaka anaomba ufafanuzi wake. Neno bila ya Mipaka lililojitokeza hapo muwekezaji binafsi anatakiwa kutokuwa na mipaka kwa mujibu wa makubaliano kama inavyosomeka katika mwazo wa kifungu hicho. Wazo lako Mhe. Abdallah Juma tumelichukuwa pia tutawasiliana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuweka sawa vifungu hivyo.

Kifungu cha 18(1) na (2) kuhusu wajibu na majukumu ya watumiaji wa miundo mbinu ya umma. Halafu pia Wajumbe wa Kamati ya Wataalamu wamependekezwa kutokana na sifa gani. Kamati ya Wataalamu kifungu namba 14 (1) kimeingiza wataalamu kutoka sekta waliochaguliwa kutokana na umuhimu wa sekta hizo kwa miradi ya *PPP* na sekta zilizotajwa ndio wamechaguliwa hawa wataalamu.

Mhe. Mussa Ali Hassan wa Koani Mheshimwia sheria hii ndio mkombozi katika kuteleta Maendeleo ya Zanzibar nakubaliana na wewe kabisa sahihi ulivyosema kwamba kwa kweli ukombozi hasa ni kuendeleza uchumi wetu unategemea sana utekelezaji mzuri wa sheria hii. Kwa hiyo, ushauri wako ni wa busara sisi tutauzingatia na kuhakikisha kuwa unafanywa kazi wakati wa utekelezaji wake.

Mhe. Fatma Mbarouk Said wa jimbo la Amani aliomba ufafanuzi wa neno *MDA* neno hili ni ufupisho wa maneno matatu ambayo ni *Ministry Derpartment and Agences.* Lakini nilisisitiza upatikanaji wa huduma bila ya ubaguzi kama ilivyo katika kifungu cha 50 (1b) ushauri wake umezingatiwa katika miradi ya *PPP* kwamba upatikanaji wa huduma bila ya upendeleo ni suala la msingi.

Hatuna lengo la kuweka ubaguzi wa aina yoyote si wa rangi wa kidini si ukabila si wa umajimbo na wanaofanya hayo tumpige vita kwa mbinu zote kwamba huyo haitakii mema nchi nyetu anaeleta ubaguzi wa aina yoyote, utekelezaji wetu sisi sote tuko hapa kwa lengo letu moja kuendeleza Zanzibar yetu. Kwa hiyo, mtu akija na ubaguzi wa aina yoyote kwa kweli huyo ndie adui namba moja, tumuandame sote kwa pamoja kwa hiyo Mhe. Fatma usiwe na wasi wasi huo.

Uliuliza nini maana ya hisa kama nilivyosema je wana hisa wana haki ya kuweka dhamana au hisa zao. Hisa ni mchango au ada inayowekwa na muwekezaji binafsi wa kampuni ili kutambua ushiriki wake ndani ya kampuni ambayo inakuwa kwa mfumo wa asilimia kwa mujibu wa makubaliano. Wana hisa wana haki ya kuweka dhamana au hisa zao kwa muwekezaji binafsi ili aweze kukopa fedha benki. Hii inapingana na ile haki ya kutoweza kuweka dhamana kwa serikali.

Mhe. Panya Ali Abdalla wa nafasi za wanawake, anakubaliana na mswada tunakushukuru kwa mchango wako. Lakini uliuliza kwenye kifungu cha 9 (3) tuongeze neno "awe" tunakubali ushauri wako ni vizuri na tumesharekebisha hili.

Pia umesema wa sifa wa anaependekezwa kwa Mkuu wa Idara uwe chini wa miaka 15 wewe unapendeleza uwe miaka 10 kwa sekta. Kwa kweli Mhe. Panya Ali kutokana na Sheria za Utumishi wa Umma Afisa Muandamizi anatakiwa kuwa na uzoefu wa miaka 15 au zaidi miaka 10 ni kidogo, vijana wengi siku hizi *alhamdulillah* tumewapatia ajira wapo miaka 10 hawajapata ule uzoefu wa kuitwa Afisa Muandamizi muandalizi awe kweli. Kwa hivyo tunakuomba utukubalie ambalo hili tulipata wenzetu kama nilivyosema kwenye taratibu za utumishi.

Pia ulitwambia kwamba umakini katika kufunga mikataba na utafiti unatakiwa ufanywe wakati wa kufunga mkataba. Ushauri huu umezingatiwa, ni kweli ni lazima tuwe makini yasitokee yale ambayo Waheshimiwa wengi waligusia yaliyotokea kabla.

Rafiki yangu Mhe. Subeit Khamis Faki ambaye yeye kwanza ni mjumbe wa kamati lakini tunamshukuru kwa michango yake, na hasa pale aliposema kwamba sheria ni nzuri na anaomba pia kwamba utekelezaji wake uwe wa ufanisi. Ninamuahidi kwamba Serikali itajitahidi kwa kushirikiana na sekta binafsi kuona kwamba uendelezaji wa sheria hii uwe mzuri ili maendeleo ya nchi yetu yale ambayo tumeyalenga yaweze kufikia kwa kipindi hichi kifupi.

Mheshimiwa pia aliuliza ni kiasi hasa cha fedha zinahitajika kuanza mradi, hii alikuwa Mhe. Ibrahim Hussein Makungu aliuzia mradi kuanza kutekelezwa ni kiasi gani inahitajika. Kwa kweli miradi inategemea aina ya mradi na uwezo wa mwekezaji. Kama mradi unagharimu chini ya Dola milioni kumi, utakuwa mradi mdogo na mradi utakaogharimu zaidi ya Dola milioni utakuwa ni mradi mkubwa huo.

Mheshimiwa Subeit alihoji kwamba sheria hii itasaidiaje katika uchimbaji wa mafuta yetu. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makungu uchimbaji wa mafuta utakuwa na sheria yake lakini kama utakuja kwa njia ya *PPP*, basi utaratibu utafuata au taratibu ambazo zitawekwa zitafuatwa za miradi ya *PPP*. Tutaweka utaratibu kwa miradi ya *PPP* ili huo uchimbaji wa mafuta uweje. Kwa mujibu wa sheria hii tutaweza ku-*incorporate* hizi sheria ili tuainishe na hao *investors* watakaokuja kwa kuchimba mafuta. Hiyo hasa ndiyo tuseme na sera kwa kweli tumo njiani kutengeneza na inshaallah itakapokamilika na sheria nayo itakuja.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali naye katika kuchangia aliomba maelezo ya sheria ya maridhiano, ninafikiri hii nimeshaeleza kwa urefu kabisa.

Halafu Mhe. Farida Amour Mohammed aliuliza kuhusu je, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ni sehemu ya kamati ya wataalamu. Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha siyo mjumbe katika kamati ya wataalamu. Yeye atakuwa na jukumu la kuidhinisha mikataba baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Yeye ni *over role boss* wa mambo ya fedha. Kwa hivyo, tumehisi kumtia mule tutakuwa na *kind of conflict of interest.* Sasa yeye tumemuachia atakuwa na mwakilishi

tu, lakini yeye tumemuachia na jukumu lake lile la kuidhinisha mikataba ambayo itafikiwa hapo baadae. Kwa hivyo, anapewa nafasi ya kipekee ya kuangalia mchakato wote kabla ya kuidhinishwa.

Nani mwakilishi kutoka Wizara ya Fedha. Mwakilishi kutoka Wizara ya Fedha atateuliwa na Wizara ya Fedha yenyewe. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nimechukua muda wako kidogo lakini nimeona upo umuhimu wa kueleza kwa undani. Lakini kwa ujumla nishukuru sana michango ya Waheshimiwa Wajumbe na takriban wote wamekubaliana na Mswada na hii imetupa fursa hii kutupa moyo kwamba twende tukarekebishe marekebisho haya ili hatimaye sheria yetu tuipeleke kwa Mhe. Rais iweze kutiwa saini na utekelezaji uanze. Maana yake miradi ipo inatungojea sisi tu ianze utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya sasa naomba nimalizie kutoa shukurani na niseme naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA KUTUNGA YA SHERIA

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake
Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA PILI

MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI

Kifungu 3 Mamlaka ya kuingia Mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi
Kifungu 4 Upeo na aina ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi
Kifungu 5 Mkataba wa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi
Kifungu 6 Muda
Kifungu 7 Umiliki wa Mali pamoja na marekebisho yake
Kifungu 8 Haki ya kifedha

SEHEMU YA TATU

MFUMO WA KITAASISI NA MAJUKUMU

Kifungu 9 Kuanzishwa kwa Idara ya Mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10 Majukumu ya Idara ya Masharikiano ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11 Upatikanaji wa Sheria au Kanuni
Kifungu 12 Uanzishwaji wa wa Kamati ya Wataalamu ya Mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi
Kifungu 13 Kazi za Kamati ya Wataalamu wa Mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi
Kifungu 14 Muundo wa Kamati ya Wataalamu wa Mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 15 Wajibu na Majukumu ya Wizara ya Fedha
Kifungu 16 Wajibu na Majukumu ya mamlaka ya utekelezaji
Kifungu 17 Wajibu na Majukumu mwekezaji binafsi pamoja na marekebisho yake

Kifungu 18 Wajibu na Majukumu ya watumiaji wa huduma au miundombinu ya umma

SEHEMU YA NNE

UTAMBUZI WA MIRADI YENYE TIJA NA TARATIBU ZA KUBARIKI KATIKA MARIDHIANO NA MASHIRIKIANO NA MAKUBALIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI

Kifungu 19 Utambuzi wa miradi yenye tija kupitia upembuzi yakinifu wa awali upembuzi halisi
Kifungu 20 Mfumo wa Maendeleo wa miradi
Kifungu 21 Madhumuni ya mfuko
Kifungu 22 Kugharamia upembuzi wa awali na upembuzi yakinifu
Kifungu 23 Uanzilishi wa sekta binafsi

SEHEMU YA TANO

UTARATIBU WA ZABUNI ZA MIRADI NA UTEUZI WA MWEKEZAJI BINAFSI

Kifungu 24 Hatua za uteuzi wa mwekezaji binafsi
Kifungu 25 Madhumuni na taratibu za vigezo vya awali pamoja na marekebisho yake
Kifungu 26 Vigezo vya uteuzi wa awali
Kifungu 27 Mgongano wa maslahi
Kifungu 28 Umoja wa Mashirika
Kifungu 29 Maamuzi juu ya uteuzi wa awali
Kifungu 30 Taratibu za miradi inayoasisiwa na Serikali
Kifungu 31 Yaliomo katika maelezo ya muombaji wa zabuni
Kifungu 32 Dhamana za zabuni
Kifungu 33 Ufafanuzi na marekebisho
Kifungu 34 Kuwasilisha mapendekezo
Kifungu 35 Vigezo vya tathmini
Kifungu 36 Kulinganisha na tathmini ya mapendekezo
Kifungu 37 Uthibitisho zaidi wa vigezo stahili
Kifungu 38 Mazungumzo ya mwisho na makubaliano pamoja na marekebisho yake
Kifungu 39 Kusitisha taratibu za manunuzi
Kifungu 40 Mazingira yatakayotumika kubariki bila ya kufuata taratibu za ushindani
Kifungu 41 Taratibu kwa ajili ya majadiliano ya makubaliano

SEHEMU YA SITA

MAOMBI YATOKANAYO NA MIRADI ILIYOASISIWA NA MWEKEZAJI

Kifungu 42 Kukubaliwa kwa maombi yatokanayo na miradi iliyoasisiwa na mwekezaji
Kifungu 43 Taratibu za kuzingatiwa kukubaliwa kwa maombi yatokanayo na miradi iliyoasisiwa na mwekezaji
Kifungu 44 Uanzishwaji wa utaratibu wa uteuzi

SEHEMU YA SABA

MAKUBALIANO YA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA BINAFSI

Kifungu 45 Sheria zinazotumika
Kifungu 46 Mambo yaliyomo katika makubaliano
Kifungu 47 Umiliki wa mali
Kifungu 48 Upatikanaji wa haki iliyohusiana na eneo uliopo mradi
Kifungu 49 Haki za matumizi

Kifungu 50 Uendeshaji wa miundombinu
Kifungu 51 Masharti ya fedha
Kifungu 52 Kampuni ya mwekezaji binafsi
Kifungu 53 Kuhaulisha usimamizi wa maslahi kwa mwekezaji binafsi
Kifungu 54 Dhamana
Kifungu 55 Kubadilika kwa sheria
Kifungu 56 Mapitio ya makubaliono
Kifungu 57 Uingiliaji kati ya mamlaka ya utekelezaji
Kifungu 58 Kumbadilisha mwekezaji binafsi
Kifungu 59 Kusainiwa makubaliano

SEHEMU YA NANE

MUDA, KUONGEZA MUDA NA KUSITISHA MAKUBALIANO

Kifungu 60 Muda na kuongeza muda wa makubaliano
Kifungu 61 Kumalizika muda wa makubaliano
Kifungu 62 Mkataba wa Kusitishwa mapema na mamlaka ya utekelezaji
Kifungu 63 Mwekezaji binafsi kusitisha mapema makubaliano
Kifungu 64 Kusitisha mapema makubaliano kutokana na sababu nyenginezo
Kifungu 65 Fidia baada ya kusitishwa kwa makubaliano
Kifungu 66 Kuvunja na hatua za kuhamisha

SEHEMU YA TISA

USULUHISHI WA MIGOGORO

Kifungu 67 Migogoro baina ya Serikali na mwekezaji binafsi
Kifungu 68 Usuluhishi wa kimataifa
Kifungu 69 Migogoro iliyohusisha wateja au watumiaji wa huduma ya miundombinu

SEHEMU YA KUMI

MASHARTI MENGINEYO

Kifungu 70 Haki za wazabuni
Kifungu 71 Kanuni
Kifungu 72 Kufuta na kubakiza

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria umeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa ninaliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, naafiki

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

MSWADA WA SHERIA WA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI YA 2015

(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ya 2015 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja ilikubaliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa michango yenu pamoja na utulivu wenu na kwa hivi sasa tumemaliza mswada huo. Kwa hivyo, tutaendelea na kazi nyengine ilioko mbele yetu kwa siku ya leo kwa sababu muda tunao. Kwa hivyo, tuna suala zima la taarifa za Kamati. Kwa hivyo, tutaanza na Kamati. Kwanza kutokana na sababu zisizoweza kuepukika Waheshimiwa Wajumbe, tutaanza na Kamati ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Waziri, karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha utekelezaji wa maagizo ya Baraza yaliyotokanana Kamati ya Katiba Sheria na Utawala.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha utekelezaji huo na naomba vile vile taarifa inayoanzia ukurasa wa 2 hadi ukurasa wa 4 iingie kwenye *Hansard* kama nitakavyosoma, utekelezaji wa maagizo hayo kwa njia ya bango kitita.

Mhe. Mwenyekiti, Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Agizo la kwanza, lilikuwa ni maoni, ilikuwa ni Kamati imeshauri na kuagiza Serikali kusaidia Halmashauri kutatua baadhi ya changamoto zinazoweza kuepukika, ikiwemo suala la kufanyia marekebisho sheria zote zilizopitwa na wakati kwa lengo la kusaidia Halmashauri ziweze kujitegemea na kujiinua katika mipango iliyojipangia na hatimaye kutimiza wajibu wake kwa wananchi ambao wanastahiki kupata huduma zilizo bora kutoka katika Hamashauri zao.

UTEKELEZAJI

Kufuatia kupitishwa kwa sheria mpya ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Nam. 7 ya mwaka 2014, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maakum za SMZ, imeanza kazi za kuandaa Kanuni pamoja na kupitia upya sheria ndogo ndogo za mamlaka za Serikali za Mitaa Zanzibar kwa lengo la kufanikisha majukumu ya taasisi hizo.

AGIZO LA PILI

Kamati iliagiza Halmashauri zote kuchukua juhudi za ziada kujitangaza kwa wananchi juu ya utendaji wake wa kazi pamoja na majukumu yake yote, ili kukabiliana na changamoto inayozikabili Halmashauri nyingi hapa nchini ya kutojulikana kazi zake na majukumu yake kwa wananchi walio wengi na baadhi ya taasisi za Serikali.

UTEKELEZAJI

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, imeupokea ushauri wa Kamati, aidha, kwa kutumia kitengo cha Habari na Mawasiliano cha Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, kinafanya ufuatiliaji na kutangaza shughuli zote muhimu katika taasisi zake kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, mkitoka naomba mtoke kidogo kidogo, lakini mjuwe humu ndani patakuwa hapana mtu.

MHE. WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

AGIZO LA TATU

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilishauri Serikali kuzidisha juhudi za kuajiri wataalamu katika Halmashauri zetu ili kupunguza changamoto ziliopo hivi sasa ambapo uajiri wa wataalamu unasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa changamoto zinazoweza kuepukika na kuzifanya Halmashauri zifanye kazi kwa utaalamu.

UTEKELEZAJI

Ofisi yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma, imeandaa utaratibu maalum wa kujua mahitaji halisi ya watumishi wenye sifa wanaoajiriwa na mamlaka za Serikali za Mitaa ili kukabiliana na majukumu mapya kwa mujibu wa sheria mpya Nam. 7 ya mwaka 2014, yenye lengo la kukasimu madaraka kwa wananchi.

AGIZO LA NNE

Kamati iliagiza Halmashauri kuwachukulia hatua kali za kisheria wale wote watakaokiuka taratibu zilizowekwa na Halmashauri likiwemo suala la kutupa taka kiholela, uharibifu wa mazingira na kadhalika. Aidha, Kamati ilipendekeza kwa Halmashauri kuwa katika maeneo yanayochimbwa mchanga na kutishia kuharibika kwa miundombinu, zikiwemo nguzo za umeme, kuwekwe ulinzi mkali katika maeneo hayo ili kupunguza uharibifu huo.

UTEKELEZAJI

Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa uwezo waliopewa na sheria pamoja na sheria ndogo ndogo ziliopo, watazitumia ili kukabiliana na wale wote watakaohalifu Sheria za Afya ya Jamii na Mazingira, pamoja na Sheria ya Mazingira. Aidha, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ itashirikiana na taasisi nyengine ili kuleta ufanisi katika suala zima la usimamizi wa mazingira, usafi katika mazingira safi na salama.

AGIZO LA TANO

Kutokana na uhaba wa ardhi uliopo hapa nchini, Kamati ilishauri Serikali kuu iangalie uwezekano wa kujenga makaazi katika ardhi isiyostawi kilimo na iachane na utaratibu wa sasa wa kujenga katika maeneo yote bila mpangilio.

UTEKELEZAJI

Ofisi yangu inakubaliana na ushauri wa Kamati, aidha, kwa kushirikiana na wizara dhamana ya ardhi chini ya Idara ya Mipango Miji na Vijiji, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitasimamia na kutekeleza mipango ya usimamizi wa matumizi bora ya ardhi pamoja na mipango miji.

AGIZO LA SITA

Kamati ilishauri Serikali kuliangalia upya suala la kutoa ruzuku kwa Halmashauri zetu, ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hii inatokana na hali halisi iliyo hivi sasa ambayo Halmashauri nyingi hazipati ruzuku kutoka serikalini na hatimaye Halmashauri hizo kufanya kazi katika mazingira magumu sana.

UTEKELEZAJI

Ushauri uliotolewa na Kamati umepokelewa, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha itaangalia uwezekano wa kuziongezea ruzuku mamlaka ya Serikali za Mitaa, ili liendane na mahitaji, ikizingatiwa baadhi ya majukumu ya sekta yanapelekwa kwenye mamlaka, hasa ukizingatia kwamba baadhi ya majukumu ya kisekta yanapelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

AGIZO LA SABA

Kamati ilishauri Serikali kufanya juhudi za makusudi ya kuzipatia Halmashauri usafiri ambao utatumika katika shughuli za kila siku. Kamati imesikitishwa sana na wakati inatembelea katika Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi na kusikia kuwa Halmashauri haina hata usafiri wa kufanyia shughuli zake. Hivyo, Kamati inashauri iombwe japo msaada wa magari ambao utasaidia kuondoa baadhi ya changamoto ziliopo hivi sasa.

UTEKELEZAJI

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum imeupokea ushauri wa Kamati na kuhakikisha Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi inapatiwa usafiri wa uhakika wa kufanyia shughuli zake. Aidha, taratibu zitafanywa kwa kuhakikisha Halmashauri zinaandaa bajeti ya kutosha kutokana na vyanzo vyake vya mapato kupitisha matumizi ya vitu mbali mbali muhimu ambavyo viwe vipaumbele katika kupitisha bajeti zao, ikiwemo ununuzi wa gari.

Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi imo katika mchakato wa kukamilisha taratibu za mkopo wa milioni 150 kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar, kwa ajili ya ununuzi wa gari zitakazowasaidia kufanya shughuli zao, mpango huo uko katika hatua nzuri na unaendelea.

AGIZO LA NANE

Kamati ilipotembelea katika Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, ilipewa taarifa kuwa wanajitahidi kukusanya mapato kupitia mabango ya matangazo mbali mbali ya biashara. Jambo la kusikitisha ni kitendo cha Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*), kutaka kukusanya mapato hayo kwa madai ya kuwa Halmashauri zinaachia mwanya mkubwa katika mapato hayo na kupelekea kupotea kwa mapato hayo, ambapo katika suala la ukusanyaji wa mapato ya *ZRB*, walitakiwa wajihusishe na ukusanyaji wa mapato kwa kupitia katika Kampuni mbali mbali zinazojisajili na sio kuingilia makusanyo yanayokusanywa na Halmashauri.

Kutokana na hali hiyo Kamati inasisitiza Bodi ya Mapato Zanzibar, kuziachia Halmashauri kukusanya mapato hayo na wao wajihusishe na makampuni kama ilivyo hapo awali. Aidha, Kamati inashauri *ZRB* ibudi vianzio vyengine vya mapato, sio kujikita katika vianzio ambavyo vimeshakubaliwa na taasisi nyengine.

UTEKELEZAJI

Ofisi ya Rasi Tawala za Mikoa na Idara Maalum inakubaliana na ushauri wa Kamati. Hata hivyo, suala la mwingiliano wa Sheria za Kisekta mbali mbali na za Serikali za Mitaa, wizara imeliona hilo wakati ilipokuwa ikiandaa sera mpya ya Serikali za Mitaa na sheria mpya ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014. Kazi kubwa tuliyonayo hivi sasa kama wizara ni kuandaa mpango wa utekelezaji wa sheria hiyo ikiwemo utaratibu mzuri wa kuondosha migongano inayojitokeza kisheria, baina ya taasisi za Serikali za Mitaa na sekta nyengine za Serikali Kuu.

Mpango huu utafanyakazi ya kubainisha mpangilio mzuri wa sheria ikiwemo ukusanyaji wa mapato yanayopaswa kukusanywa na taasisi za Serikali Kuu na yale yanayopaswa kukusanywa na mamlaka za Serikali za Mitaa.

Idara Ya Chuo Cha Mafunzo

AGIZO LA KWANZA

Maoni na maagizo ya Kamati. Kamati inashauri wizara na Serikali kwa ujumla, kufanya utaratibu wa kuchukua mradi wa ujenzi wa gereza jipya la Hanyegwa Mchana, kwa kufuata wafadhili watakaosaidia kulijenga gereza hili ambalo linahitaji fedha nyingi.

UTEKELEZAJI

Wizara ilivyoagizwa na Kamati mradi wa ujenzi wa gereza umerejeshwa Serikali kwa ajili ya kuzingatiwa na kupatiwa wafadhili au wahisani watakaosaidia ujenzi wa gereza hilo. Hatua inayoendelea kwa sasa ni kujenga uzio kwa ajili ya kulidhibiti eneo ambayo inatekelezwa kwa kutumia fedha iliyoingizwa kwa utekelezaji wa shughuli hiyo.

AGIZO LA PILI

Kamati inashauri wizara kukisaidia Chuo cha Mafunzo kwa kuzungumza na uongozi wa Wizara ya Afya na kukubaliana juu ya suala la kuwapatia kuwapatia dawa za kila mwezi Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya matibabu ya wanafunzi. Aidha, Kamati inashauri wizara itafute wafadhili watakaosaidia ujenzi wa hospitali katika kambi za Ubago, Kangagani na Kengeja.

UTEKELEZAJI

Idara imefanya mazungumzo na Wizara ya Afya kuhusu kupatiwa dawa kwa kila mwezi. Wizara ya Afya inaendelea na juhudi za kuipatia idara mgao wa dawa kila hali inaporuhusu. Aidha, kwa upande wa kufuata wafadhili kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa hospitali katika kambi za Ubago, Kangagani na Kengeja. Mazungumzo yamefanyika kwa shirika la msalama mwekundu *red cross* ambapo waliweza kusaidia katika ujenzi wa mnara wa kuwekea tangi la maji katika kambi.

Kwa upande wa ujenzi wa kituo cha afya, mazungumzo yanaendelea kufanyika kwa taasisi nyengine ikiwemo *Pharm-Access*, ambao kwa hatua ya awali wamesaidia ujenzi wa kituo cha afya cha Wete Pemba, ambacho kipo katika hatua ya kuezekwa.

AGIZO LA TATU

Kamati inaagiza huduma ya kiroho ya kutoa mawaidha kwa wanafunzi waliofungwa katika Vyuo vya Mafunzo, iendelee kutolewa na idara ifanye juhudi za makusudi za kuwalipa viongozi hao, kutokana na umuhimu wa huduma hiyo kwa wanafunzi waliopo kwenye Vyuo vya Mafunzo hivi sasa.

Idara imefanya mawasiliano na Ofisi ya Mufti na makubaliano yamefanikiwa, ni kwamba Ofisi ya Mufti itafanya mazungumzo na Masheikh, ili wawaelimishe suala hili na kujitolewa kutoa mawaidha hata ikiwa hawakupata malipo, kwani hiyo ni miongoni mwa ibada ya Mwenyezi Mungu, suala la malipo lisiwe kikwazo cha kutokuitumikia dini.

AGIZO LA NNE

Kamati inashauri wizara iendelee na juhudi ya kuwasaidia askari kupata mazingira mazuri ya kuishi, kwa kuwajengea nyumba za kuishi. Kamati ilishauri wizara ijenge nyumba hizo kupitia mfuko kutoka *ZSSF* au itafute wafadhili watakaosaidia ujenzi huo. Kamati inashauri wizara ifanye juhudi za makusudi za ukarabati barabara inayoelekea kambi ya Ubago.

UTEKELEZAJI

Kuhusiana na ukarabati wa barabara ya kambi ya Ubago, kwa hatua za awali tayari imeshawekewa kifusi na kwa hatua zinazofuata wizara ina mpango wa kuingiza barabara hiyo katika ratiba ya mpango wa ujenzi wa barabara zitakazosimamiwa na wizara kupitia mfuko wa barabara. Aidha, kuhusiana na kuwapatia askari mazingira mazuri ya kuishi, wizara itaendelea kulitekeleza agizo hilo kadiri hali itakavyoruhusu.

AGIZO LA TANO

Kamati inashauri wizara ijitahidi kuinunulia idara usafiri wa uhakika kwa ajili ya shughuli zao za kila siku.

UTEKELEZAJI

Katika kulichukulia hatua suala la usafiri, idara imeipatia Kambi ya Ubago gari moja kwa ajili ya shughuli zao za kila siku na hatua zitaendelea kwa kambi nyengine.

AGIZO LA SITA

Ni kuhusiana na deni kubwa la umeme, Kamati imekubaliana na ushauri uliotolewa na Idara ya Chuo cha Mafunzo kuwa fedha za bajeti ya umeme iliyotengwa na idara, zipelekwe moja kwa moja *ZECO* ili wakate deni hilo kwa lengo la kulipunguza na hatimaye kulimaliza kabisa.

UTEKELEZAJI

Idara imekaa kikao cha pamoja na Bodi ya Shirika la Umeme na Wizara ya Fedha, kujadili uwezekano wa Wizara ya Fedha kulipa deni la umeme moja kwa moja kupitia bajeti ya idara. Aidha, idara imechukua hatua ya kuunga mita za TUKUZA kwa ajili ya kupunguza mrundikano wa madeni.

AGIZO LA SABA

Kutokana na malalamiko iliyoyapokea kutoka kwa wanafunzi waliofungwa kifungo cha maisha, Kamati inashauri wizara iishauri Serikali ifanye utaratibu wa kurekebisha sheria iliopo sasa ambayo inaruhusu kunyonga na kuifanya iwe ni ya kifungo cha maisha. Kamati inatoa ushauri huo kutokana na uzoefu kuonesha kuwa wanafunzi wanaohukumiwa kifo, hukumu hiyo huwa haitekelezwi na hatimaye huleta malalamiko kutoka kwa wanafunzo hao.

UTEKELEZAJI

Idara kwa kushirikiana na taasisi husika tayari imelifikisha suala hilo serikalini. Kamati inaagiza Kamati ya *Visiting Justice,* irudishe utaratibu wa kutembelea katika magereza yaliopo hapa nchini, kwa lengo la kwenda kusikiliza matatizo mbali mbali yanayowakabili wanafunzi waliopo magerezani.

Wizara inafanya utaratibu wa kukutana na Wajumbe wa Kamati ya *Visiting Justice* kuweka utaratibu wa Kamati hiyo kutembelea katika magereza, kwa lengo la kwenda kusisitiza matatizo mbali mbali yanayowakabili wanafunzi waliopo magerezani.

AGIZO LA TISA

Kamati inakubaliana na ushauri uliotolewa na baadhi ya wanafunzi waliopo gerezani wa kuwashirikisha wadau au wahusika wengine na wawekezaji kuwekeza katika magereza yetu kwa lengo la kuvitafutia vitengo mbali mbali, vikiwemo kitengo cha ushoni na useremala ambavyo vimeanzishwa kwa lengo la mafunzo kwa wanafunzi ikiwa na lengo la kutimiza azma ya Vyuo vya Mafunzo ya kuwafundisha wanafunzi wawe raia wema hapo wanapomaliza muda wao na kurudi uraiani.

Aidha, ushauri ulitolewa wa kuanzisha viwanda vya sabuni, viatu na kuviboresha vile viliyomo, hatua imechukuliwa na Kamati inaomba Serikali ilifanyie kazi suala hilo.

UTEKELEZAJI

Idara tayari imeanzisha mradi wa mpango wa elimu kwa wanafunzi mradi huu umeanzishwa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kupitia kitengo cha elimu mbadala kwa lengo la kutoa elimu ya lazima na elimu ya amali kwa wanafunzi, hatua ya kuwapatia mafunzo wakufunzi tayari imeshafanyika.

AGIZO LA KUMI

Kamati ilipokea ushauri kutoka kwa wanafunzi waliopo Vyuo vya Mafunzo wa kuiomba Serikali ishauriane na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa kwa vile siku ya Muungano inajumuisha pande zote mbili ni vyema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anapotoa msamaha msamaha huo uwajumuishe na wanafunzi wa Zanzibar waliofungwa kwa vile huu ni Muungano wa nchi mbili. Hivyo, wanapaswa kunufaika na msamaha huo ni wananchi wa pande zote mbili.

UTEKELEZAJI

Hatua za kuwasilisha agenda hiyo kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu vinaendelea kwa ajili ya kupata ufafanuzi wa uwezekano wa utekelezaji wa jambo hilo.

AGIZO LA KUMI NA MOJA

Kamati ilishauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Katiba Sheria kulitafutia ufumbuzi suala la mrundikano wa *reminds* katika gereza la Kilimani, Serikali kupitia idara kwa kushirikiana na Wizara imewasiliana na Wizara ya Katiba Sheria kuwaomba Majaji na Mahakimu kutembelea katika Chuo cha Mafunzo ili kuona mrundikano huo wa mahabusu kufuatia ziara ya Majaji na Mahakimu, hatua mbali mbali zilichukuliwa ikiwemo kuwapatia dhamana mahabusu wote waliokamilisha taratibu zote za dhamana pamoja na kuanza kusikilizwa kesi zao. Hatua hiyo imepunguza kwa kiasi kikubwa cha mrundikano wa mahabusu katika gereza la Kilimani na Magereza mengine.

Kikosi Maalum Cha Kuzuia Magendo (KMKM)

AGIZO NAMBA MOJA

Kamati iliagiza Wizara ikae na Wizara ya Afya na wakubaliane kuhusiana na wazo la kikosi kupatiwa dawa hadi unapofika mwisho wa mwezi, fedha zinapoingia zilipwe kwa ajili ya dawa hizo. Kamati iliwaagiza wataalam wa Kikosi cha Kuzuia Magendo kukaa pamoja na bodi ya madawa ili kusaidiana mawazo na hatimae wakubaliane na kupatikana kwa mtaalam atakayekidhi viwango ili duka la dawa lisifungwe.

UTEKELEZAJI

Kikosi kinaendelea nakupata huduma za dawa kwa matumizi ya kila mwezi kama ilivyokuwa hapo awali, ingawa si kwa kiwango cha kutosha, aidha kikosi kinaendelea na ununuzi wa dawa hizo kwa bajeti yake Unguja na Pemba, kwa kadri ya fedha inavyoruhusu ili kukidhi mahitaji kwa wapiganaji na raia wanaopata huduma katika kituo hicho.

Kwa upande wa suala la duka la dawa ni kwamba hadi sasa linaendelea kutoa huduma kama kawaida na taratibu za kulisajili zinaendelea ili kupata mdhamini anayekubalika kisheria kwa kutoa huduma hii, sambamba na hilo, kikosi kimeshapata mpangaji mwenye sifa za kusimamia na kuendesha duka hilo kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa, kwa maana hiyo duka hilo sasa litakodishwa kwa mtu ambaye ana sifa ya kufanya kazi hiyo ya kuuza madawa.

AGIZO LA PILI

Katika changamoto ya ukosefu wa usafiri Kamati ilielezwa kuwa kikosi cha KMKM kimependekeza kuwa ili kuondoa tatizo hilo wapatiwa japo magari ya mkopo nafuu Mkopo ambao utalipa kidogo kidogo, kwa mujibu wa uwezo wa idara ambapo Kamati imekubaliana na wazo hilo la idara na inanishauri Wizara niifanyie kazi kama itawezekana.

UTEKELEZAJI

Kikosi cha KMKM kupitia bajeti yake ya mwaka 2014/2015 inayoendelea, imeendelea kutafuta njia ya kupunguza changamoto ya ukosefu wa usafiri na tayari imeshanunua gari moja aina ya *Land Cruise* bado pia zabuni kwa ajili ya ununuzi wa gari nyengine nne imeshafanyika, kinachosubiriwa ni kwa mdhabuni kutoa huduma husika.

AGIZO NAMBA TATU

Kamati iliguswa sana na suala zima la uokozi ambapo inashauri Serikali kufanya juhudi za makusudi za kununua vifaa vya uokozi ambavyo ni muhimu katika majanga ambayo yanaweza kutokea hapa nchini.Aidha, Kamati inaagiza kujengwa kwa *Rise Cure Base Centre* huko Nungwi ambako itakuwa ni kiunganishi katika shughuli za uokozi pamoja na maelezo yaliyotolewa kwa Kamati kuwa kuna mpango wa kujenga *Base* huko Kizimkazi, Nungwi, Mkoani na Wete. Lakini bado Kamati inasisitiza umuhimu wa *base* hiyo ambayo ni kiungo muhimu sana.

UTEKELEZAJI

Kikosi kupitia bajeti ya mwaka 2014/15 kinaendelea na jitihada zake za kupata vifaa vya uokozi na mafunzo kutoka kwa kampuni moja nchini Uingereza iitwayo *LNW UK HP HOUSE,* vifaa hivyo ni vya aina mbili; yaani *Equipment For Open Water Advance and Rise Cure Diver Training* na *Equipment For Deep Water Training and Advance.* Vifaa hivi vinategemewa kuwasili baada ya wiki sita kutoka sasa.

Pia, kikosi kina mradi mkubwa kupitia bajeti ya maendeleo ya mwaka 2014/15 kwa ujenzi wa vituo vya uokozi na ununuzi wa vifaa na kwa mwaka wa ujenzi vituo viwili vya Mkoani Pemba KMKM Kibweni umeanza unenzi wa Mkoani Pemba, umesita kutokana na kutokamilika mazungumzo baina ya shirika la Bandari na uongozi wa KMKM, juu ya matumizi ya kiwanja kilichopo hapo Mkoani ambacho kinamilikiwa na Shirika la Bandari. Aidha, ushauri wa Kamati kujenga *Base* ya uokozi hapo Nungwi utaelekezwa kwa kujengwa *Sub-base* na *Base* kuu itakuwa Kibweni.

KMKM Mkoani Pemba ambazo tayari zimeshaanza kujengwa utaratibu huu bado unaendelea mwaka wa fedha ujao kwa kuendelea kujenga vituo Unguja na Pemba sambamba na ununuzi wa zana za vifaa pamoja na mafunzo ya uokozi.

AGIZO LA NNE

Kamati ilitoa maagizo kuwa rada ya Sengenye mlima wa Mtambwe ifanyiwe marekebisho ili iweze kufanya kazi kama ilivyokuwa hapo zamani, ambapo Kamati ilipewa maelezo kuwa rada hiyo kwa sasa si rahisi kurekebishwa. Kamati inaagiza kuwa ufanywe utaratibu mwengine wa kuwa na rada kama hiyo maeneo ya karibu na ilipokuwepo hiyo ya mwanzo ili iweze kusaidia katika shughuli za kiusalama kama ilivyokuwa hapo awali.

UTEKELEZAJI

Serikali kwa kuelewa umuhimu wa rada kwa usalama wa nchi inaendelea na msimamo wake juu ya haja ya kuzifufua rada zote za KMKM ile ya Sengenya Mlima wa Mtambwe na ya Masingini Unguja, suala bado lipo katika mchakato ambao iliunda Kamati iliyojumuisha taasisi kadhaa za Serikali ikiwemo KMKM, Idara ya Uvuvi na Zanzibar *Maritime of Authority ZMA,* kuangalia umuhimu wa kuzifufua rada hizo na kuwasilisha pendekezo hilo Serikali kuu na hivi sasa lipo katika hatua ya kuridhisha.

AGIZO LA TANO

Ili kukamilisha ujenzi wa Hospitali ambayo imegharimu fedha nyingi za Serikali, hospitali ambayo inawasaidia sana wananchi wanaoishi karibu na maeneo yale pamoja na wananchi wote kwa ujumla, Kamati inashauri Serikali kulifikiria upya suala la kuingiza bajeti ya maendeleo ya mwakani kwa Idara ya KMKM ili kukamilisha hospitali hiyo na kuondoa baadhi ya changamoto zinazoikabili hospitali hiyo.

UTEKELEZAJI

Wizara inaishukuru sana Serikali kuu kwa kuendelea kuipatia bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2014/15 kwa ununuzi wa vifaa na thamani ya hospitali hiyo, kwa mwaka huu KMKM imeweza kununua vifaa vya upasuaji na thamani kwa ajili ya hospitali. Aidha, Wizara itaendelea kuomba fedha za maendeleo kwa mwaka ujao kwa ajili hiyo ili iweze kukamilisha ununuzi wa vifaa vya maabara, ili kuiweka hospitali yetu katika hali ya utayari ya kutoa huduma kwa viwango vipana zaidi.

Kuhusu mpango wa uendelezaji wa ujenzi Wizara itaendelea kuomba fedha hizo kwa bajeti inayofuata ili kukamilisha baadhi ya sehemu muhimu kama vile chumba cha *X-Ray, Ultrasound* na wodi wa wazazi kupitia fedha za mradi wa maendeleo.

Jeshi La Kujenga Uchumi (JKU)

AGIZO LA KWANZA

Kamati ilishauri Serikali kulisaidia Jeshi la Kujenga Uchumi kupatiwa Shilingi milioni 300 kwa kila mwaka katika bajeti ya maendeleo hadi utakapokamilika ujenzi wa Skuli ya JKU Mtoni.

UTEKELEZAJI

Tunazipokea kwa dhati pongezi za Kamati ya Baraza la Wawakilishi kwa kuona juhudi na hatua zilizofikiwa katika ujenzi wa skuli, jitihada za kuiomba Serikali kuingiza ujenzi huo katika bajeti ya kila mwaka zinafanywa. Kwa kuthibitisha hilo uongozi wa Wizara chini ya Idara ya Mipango Sera na Utafiti imeshasimamia uandaaji wa andiko yaani *Project write-up* za skuli ya JKU na kuwasilisha Tume ya Mipango katika mwaka uliopita wa fedha 2014/15, Kwa raratibu za Tume ya Mipango mradi huo haukuwa miongoni mwa miradi iliyochaguliwa kwa mwaka huo wa fedha. Hivyo, jitihada zinaendelea kwa kuombewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/16.

AGIZO LA PILI

Ilikuwa Kamati imeshauri uongozi wa skuli kufikiria kuanzisha somo la kilimo kutokana na umuhimu wake wa kuzalisha ajira.

UTEKELEZAJI

Ushauri ni mzuri ambapo hata hivyo kwa sasa skuli imeanza kwa kuingiza somo la uvuvi na ubaharia kuanzia mwaka 2015/16 kwa kuzingatia sababu sawa zilizoainishwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati, kuhusu somo la kilimo litazingatiwa siku za usoni kwa sasa vijana wanapatiwa mafunzo ya kilimo na ufugaji kwa vitendo katika makambi ya JKU kupitia chuo cha Kilimo kilichoko Kizimbani.

AGIZO LA TATU

Kamati inaiomba Serikali kufikiria kuwapandisha posho wanafunzi wote wanaojitolea kutoka shiligi 1,300 hadi shilingi 15,000 kutokana na uzito wa kazi na hali ya maisha.

UTEKELEZAJI

Hali hiyo imezingatiwa ambapo posho hupandishwa kwa awamu kila hali inaporuhusu kwa sasa kwa wanafunzi walioko skuli ya ufundi posho imeongezeka kutoka shilingi 1,300 hadi 5,000 na mategemeo ni kupandisha zaidi kwa awamu kila hali itakaporuhusu mpaka kufikia au kupitiliza kima kilichoainishwa na Waheshimiwa Wawakilishi.

AGIZO LA NNE

Ilikuwa Kamati ilishauri Wizara na Serikali kuimarisha Kiwanda cha Ufundi kilichopo Saateni kwa kujenga banda jipya pamoja na kununua mashine mpya za kisasa zitakazosaidia kiwanda hicho kuzalisha na kukabiliana na ushindani.

UTEKELEZAJI

Juhudi zimeanza kuchukuliwa ambapo katika hatua ya awali Wizara kupitia Idara ya Mipango Sera na Utafiti imeunda Kamati ya kufanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi na shughuli za uzalishaji za Idara maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hatua ya kukipatia hati miliki kiwanda hicho umekamilika na ununuzi wa vifaa unaendelea kwa awamu kwa kutumia nguvu za ndani zinazotokana na uzalishaji unaoendelea kiwandani kwa sasa, mpango wa kukipatia kiwanda mashine za kisasa unaratibiwa.

AGIZO LA TANO

Ilikuwa Kamati ilizidi kusisitiza kiwanda cha ufundi cha Saateni kijitangaze kupitia maonyesho mbali mbali ya wafanya biashara.

UTEKELEZAJI

Kiwanda kinashiriki maonyesho na kutokana na kutengeneza na kutokana na kutengeneza bidhaa ndogo ndogo zenye mvuto ambazo hazikuzoeleka kutengenezwa na mafundi walio wengi, kimekuwa kikitoa mvuto kwa wateja.

AGIZO LA SITA

Vijana wanaomaliza skuli wawekewe masharti kuwa ni lazima wapite JKU kama ilivyokuwa zamani.

UTEKELEZAJI

Ingawa kwa sasa kujiunga kumekuwa kwa hiyari muitikio wa vijana ni mzuri na Serikali imewezesha JKU kuweka vijana katika makambi na kuwapatia mafunzo ya uzalishaji na uzalendo, iwapo uamuzi wa kupitisha ajira JKU hasa vyombo vya ulinzi na usalama utasimamiwa kwa dhati muitikio wa vijana kujiunga na JKU utakuwa mkubwa.

Kikosi Cha Zima Moto Na Uokozi

AGIZO LA KWANZA

Kutokana na changamoto zilizoelezwa kwa Kamati wakati ilipofika Wizara katika kikosi cha Zimamoto, Kamati imesikitishwa sana na taarifa kuwa kikosi kinakabiliwa na changamoto ya ukosefu na uchakavu wa vifaa vya kuzimia moto, hususan katika vituo vya Zimamoto bandarini na Uwanja wa Ndege Unguja na Pemba. Kamati imesikitishwa na taarifa hiyo kutokana na ukweli kuwa maeneo ya Viwanja vya Ndege na Bandari ndio uti wa mgongo wa mapato yote ya Serikali.

Kutokana na Sheria za kimataifa endapo vifaa vilivyoainishwa katika changamoto vikikosekana wakati wowote viwanja vyetu vya ndege na bandari vinaweza kufungwa kuendesha shughuli zake, hadi hapo masharti yatakapotimizwa. Hata hivyo jambo la kusikitisha zaidi Kamati ilipewa taarifa kuwa jambo hili linajulikana hadi katika Serikali kuu.

Lakini cha kushangaza hadi hivi sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa ya kuondosha changamoto hizo. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kulichukulia hatua kwa umakini suala hilo kwa kutafuta vifaa vya kuzimia moto katika viwanja vya ndege na bandari zetu.

UTEKELEZAJI

Katika kutatua changamoto ukosefu na uchakavu wa vifaa vya kuzimia moto katika Kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume *International Air Port* (*AKIA*) Wizara kwa niaba ya Serikali imeingia mkataba na kampuni moja ya Uholanzi kwa ajili ya ununuzi wa gari mpya nne, pamoja na vifaa ambavyo vitakizi mahitaji ya viwango katika viwanja hivyo, gari hizo zitaundwa mara tu yatakapofanywa malipo ya awali ya Asilimia 25 ya gharama za gari hizo.

Kwa upande wa Pemba gari ziliopo zinakidhi utoaji wa huduma na suala la upungufu wa vifaa limeshachukuliwa hatua kwa kununua vifaa hivyo ikiwemo mitungi sita ya hewa, mavazi maalum ya kinga ya moto kwa waokozi.

AGIZO LA PILI

Kamati iliagiza Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kukaa pamoja na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na kukubaliana kuwapa maeneo ya kuweka Ofisi watendaji wa kikosi cha Zimamoto kutokana na maeneo yanayotumiwa na kikosi hicho kama ofisi kutoridhisha.

UTEKELEZAJI

Kwa upande wa Bandari ya Malindi tayari kituo kimeshahamishwa katika eneo jengine na kutengewa sehemu ya kuegesha gari za Zimamoto, kuhusu upatikanaji wa *boat* ya kuzimia moto hadi sasa bado hatujafanikiwa kutokana na gharama kubwa ya ununuzi wa *boat* hiyo, hata hivyo jitihada zinafanyika kuzungumza na wahisani kuhusu suala hilo inapotokea mwanya wa kufanya mazungumzo nao.

Kwa upande wa Bandari ya Mkoani na Wete mazungumzo na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano yanaendelea ili tupatiwe eneo la kituo cha Zimamoto na Uokozi, halikadhalika katika eneo la uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume.

AGIZO LA TATU

Kamati ilipewa taarifa kuwa taasisi zinazohusika katika upangaji wa miji zinapoandaa ramani za mipango miji huwa hashirikishi Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, jambo ambalo ni la kusikitisha hasa kutokana na unyeti wa idara hii katika suala zima la uokozi kutokana na umuhimu wa ushirikishwaji wa kikosi cha Zimamoto na Uokozi katika kazi ya mipango miji.

Kamati inashauri wizara kuzungumza na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, kupitia Idara yake ya Mipango Miji kuhakikisha kuwa wanapoamua kuandaa ramani za mipango miji iwashirikishe Idara ya Zimamoto ili wasikilizwe mawazo yao ambapo unapotokezea moto sehemu ni Idara ya Zimamoto pekee ndio yenye uwezo wa kuzima moto huo na ndio wenye utaalamu wa kujua kitu gani kiwekwe sehemu gani.

UTEKELEZAJI

Hatua ya kuwaandikia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati imechukuliwa na tunasubiri kukamilika kwa taratibu zao ili tuweze kushirikishwa katika Kamati ya mipango miji.

Kikosi cha Valantia

AGIZO LA KWANZA

Kikosi hiki Kamati ilishauri Serikali kufanya juhudi za makusudi kuzitafuta changamoto ziliopo zinazokikabili Kikosi cha Valantia, hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya changamoto hizo zinaweza kuondoka mara moja endapo zitachukuliwa hatua kwa haraka.

UTEKELEZAJI

Katika kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa majengo, kikosi kimeanza na ujenzi wa majengo kwa hatua ya mwanzo, yaani kujenga msingi kwa kambi za Muyuni na Kikungwi, majengo ambayo yatakapomalizika yatatumika kwa shughuli za kiofisi na mabweni ya kulala askari. Pia, kikosi kinaendelea na ujenzi katika kambi ya Mwanyanya kwa Unguja na Micheweni kwa Pemba, ambapo majengo hayo yamefikia hatua ya juu (*lintar*).

Aidha, katika hatua ya changamoto ya ukosefu wa umeme, kikosi kimeshachukua juhudi ya kufanya mazungumzo na Shirika la Umeme Zanzibar ambapo hatua za kuunganisha umeme zimeshaanza kwa kuanzia na Kambi ya Pangatupu ambapo vipimo kwa ajili ya uunganishaji umeme katika kambi nyengine vimefanyika.

AGIZO LA PILI

Kamati iliagiza Kikosi cha Valantia kikutane na Wizara ya Ardhi hasa Idara ya Ardhi na Usajili ili waweze kufanya mazungumzo na hatimaye wakubaliane wapatiwe hatimiliki ya maeneo yote yanayomilikiwa na kikosi hicho ili waweze kuyazuia kuepusha uvamizi ambao unaweza kufanyika endapo maeneo hayo yatakosa hatimiliki. Kamati inasisitiza kikao hicho kifanyike haraka iwezekanavyo kutokana na taarifa kwamba idara imeshalipa katika maeneo yake yote ya Unguja na Pemba, lakini bado hatimiliki hazijapatikana.

UTEKELEZAJI

Kufuatia maagizo ya Kamati, kikosi kimekamilisha malipo ya hatimiliki kwa maeneo yake Unguja na Pemba. Jitihada za kukutana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati hasa Idara ya Ardhi na Usajili kwa sasa mazungumzo yanafanyika ili kuweza kufanikisha upatikanaji wa hatimiliki ya maeneo hayo. Nataka nilithibitishie Baraza hili kwamba, mawaziri wawili tayari tumeshakaa kuzungumza na tumekubaliana kwamba hatimiliki za maeneo haya ziweze kutolewa hata kama hayo mazungumzo hayatafanyika.

AGIZO LA TATU

Lilikuwa Kamati inashauri Serikali kukisaidia Kikosi cha Valantia kwa kupatiwa fedha kujenga hospitali kama kilivyo Kikosi cha KMKM. Kamati inatoa ushauri huu kwa Serikali kutokana na umuhimu wa hospitali hiyo kwa kikosi chenyewe na hata kwa raia wanaozunguka maeneo ya kambi.

UTEKELEZAJI

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ iliuchukua ushauri huu uliotolewa na Kamati wa kujenga hospitali kubwa ili iweze kutoa huduma kwa wapiganaji na wananchi kwa ujumla. Kwa hatua za awali kikosi kimeweza kufungua vituo vya afya katika kila zoni, vituo ambavyo vinatoa huduma kwa askari na raia wanaoishi maeneo ya jirani.

Lakini Serikali kupitia wizara yetu, tumekubaliana kwamba hospitali ya KMKM ndio hospitali ambayo itapokea wagonjwa watakaokuwa *referred* kutoka katika vituo vyetu na sio kila kituo kujenga hospitali au sio kila kikosi kujenga hospitali ambayo itakuwa na hadhi kama ile hospitali ya KMKM.

AGIZO NAMBA NNE

Kamati ilipotembelea katika idara hii ilisikitishwa sana na taarifa iliyopatiwa kuwa uingiaji wa *OC* umekuwa ni wa kusuasua na kupelekea baadhi ya shughuli kutotekelezwa kwa ufanisi kutokana na ukosefu wa fedha hizo. Kamati iliiagiza Serikali kuhakikisha kuwa fedha zinazopangwa katika bajeti zinaingizwa kwa mujibu wa zilivyokubaliwa, hasa ikizingatiwa umuhimu wa taasisi yenyewe na majukumu yake kwa wananchi.

UTEKELEZAJI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ imepokea agizo hilo la Kamati na itazidi kuwasiliana na Wizara ya Fedha kuomba kuingiziwa fedha kikosi hiki ili kiweze kutekeleza majukumu yake na hatimaye kufikia malengo iliyojiwekea.

AGIZO NAMBA TANO

Kamati ilishauri Serikali kufanya juhudi za makusudi za kuvitafutia vikosi vyote magari japo kwa mkopo nafuu kutokana na vikosi vingi kukosa usafiri wa uhakika. Kila kikosi kilichotembelewa na Kamati na kutoa taarifa kwa Kamati suala la usafiri limekuwa ni kilio kikubwa. Hivyo, Kamati ilitoa wazo kwa Serikali kuvisaidia vikosi hivi kupata usafiri wa uhakika ili viweze kutekeleza majukumu yao kulingana na usalama wa nchi kwa umakini zaidi.

UTEKELEZAJI

Suala la usafiri limekuwa ni changamoto kubwa si tu kwa vikosi bali kwa idara nyingi ziliomo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, suala la usafiri limewekwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum. Kwa upande wa Kikosi cha Valantia kimefanya jitihada na kufanikiwa na kununua gari mbili kwa ajili ya kusambazia walinzi na gari moja kwa shughuli za kiutawala; jitihada za kupata gari zaidi zinaendelea.

AGIZO NAMBA SITA

Kamati ilipenda kuchukua fursa hii kukipongeza Kikosi cha Valantia Zanzibar kwa juhudi zake za kujikwamua na baadhi ya changamoto kwa kuanzisha kiwanda cha viatu. Aidha, Kamati ilifurahishwa sana na ilipotembelea na kukikuta kiwanda hicho ambacho kinafanya kazi nzuri katika mazingira magumu sana. Hivyo, Kamati inavishauri vikosi vya SMZ vinapotaka viatu vya kijeshi kununua viatu vinavyotengenezwa na Kikosi cha Valantia kutokana na viatu kuwa na ubora wa hali ya juu kama viatu vyengine.

Kamati pia inachukua fursa hii kuishauri wizara kuangalia uwezekano wa kutafuta wafadhili nje ya nchi ambao wataweza kusaidia kiwanda hiki ambacho endapo kitaendelezwa kitakuwa ni mkombozi wa suala la ukosefu wa ajira kwa vijana wengi wa Kizanzibari. Vile vile, Kamati ilipenda kuwashajihisha Wajumbe wa Baraza la

Wawakilishi kufika katika Kikosi cha Valantia na kununua viatu vinavyotengenezwa kiwandani hapo ili kukipa motisha kiwanda hicho.

UTEKELEZAJI

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa kwa dhati kabisa inapokea pongezi za Kamati. Aidha, imepokea ushauri wa kuangalia uwezekano wa kutafuta wafadhili nje ya nchi ambao wataweza kusaidia kiwanda hiki. Ofisi inaahidi kuitumia fursa iliyopo ya kuwekeza kwa mfumo wa ubia baina ya Serikali na taasisi binafsi ili kiwanda hicho kiweze kuimarika.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kwamba tuliagizwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kupitia Baraza lako tukufu katika kikao cha mwezi wa Machi/Aprili mwaka uliopita na haya ndio majibu ya utekelezaji wa mambo ambayo tuliagizwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Waheshimiwa Wajumbe, sasa hivi tutapokea ripoti ya Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria. Mhe. Waziri, karibu.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kufika hapa ili kuendeleza shughuli zetu hizi za ujenzi wa Taifa.

Pili, Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili nipate nafasi kidogo ya kuelezea utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Katiba na Sheria ambayo yalitupa katika kipindi cha mwaka...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, Wajumbe, wanaomba upaze sauti kidogo wale wa nyuma wanasema hawasikii.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria ilianzishwa baada ya uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010 chini ya kifungu chini ya kifungu cha 42 (1) cha Katiba kinachompa Mhe. Rais Mamlaka ya kuteuwa na kuunda wizara hizo.

Wizara iliundwa kuratibu shughuli za Sekta ya Sheria na kusimamia utoaji haki kutoa huduma za Usajili wa Biashara na Mali kutoa huduma za Usajili wa Biashara na Mali, Usajili wa Matokeo ya Kijamii na Usajili wa Hati Miliki, kusimamia Mali za Wakfu na Mali za Amana na kusimamia shughuli za Afisi ya Mufti.

Majukumu hayo yanatekelezwa na Taasisi 12 Mahakam Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, Afisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo, Afisa wa Msajili wa Hati Miliki, Kamisheni wa Wakfu na Mali ya Amana, Afisi ya Mufti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mipango Sera na Utafiti na Afisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa shughuli zake za kawaida kwa mwaka 2013/14 Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala ilifanya kazi na Wizara ya Katiba na Sheria na ilitoa maoni na maagizo kadhaa kwa wizara. Maoni na maagizo hayo yametekelezwa kama ifuatavyo:-

(1) Katika Mahakama Serikali ifanye juhudi ya kuyafanyia matengenezo majengo ya Mahakama na pia ijenge jengo jipya la kisasa kwa ajili ya Mahakama kuu.

Mhe. Mwenyekiti, majengo ya Mahakama kuu Vuga Mahakama ya Kadhi ya Wilaya ya Mwanakwerekwe na Mahakama ya Wilaya Makunduchi na Mahakama ya Mwanzo Chwaka yameshafanyiwa matengenezo makubwa, matengenezo kama hayo yanaendelea kwenye jengo la Mahakama Kuu...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, naona Waheshimiwa Wajumbe sijui wamepata taarifa yako katika maandishi, sijui kama imewasilishwa sasa wengine sijui hawakupata. Waheshimiwa Wajumbe, mmepeta nyote taarifa ya Mhe. Waziri ya maandishi?

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba tukusaidie kidogo, tulichopata kimeandikwa maagizo ya Baraza la Wawakilishi kutoka na Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mwaka wa fedha 2013/14. Halafu imeanza na kila idara iliyochaguliwa. Lakini humu yaliomo ni maagizo ya Kamati matupu, hayo majibu ya Mhe. Waziri hayamo na mengine yamechanganywa humu mna Kazi na Utumishi wa Umma humu ndani, mna baadhi ya mambo ya JKU yameingia humu ndani ambayo tumeshasomewa, ndio maana tukawa tunashindwa ku-*follow* anachokizungumza Mhe. Waziri pale.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa sawa na mimi kwa taarifa niliyonayo kwamba hii kazi imefanywa na Baraza na sio Ofisi yako Mhe. Waziri, sijui kama ni sahihi. Lakini taarifa tulikuwa tunaitaka ifike kwa Wajumbe ni taarifa ambayo unaisoma wewe hapa na hiyo Waheshimiwa Wajumbe hawana.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Sasa Mhe. Mwenyekiti, itakuwa ni kosa la meza yako, kwa sababu taarifa nimepewa sasa hivi mimi niisome na wakati katika ratiba ilikuwa bado. Kwa hivyo, hata pengine watu wangu hawajazileta. Sasa kwa sababu mimi nilikuwa nimeshajiandaa nikakwambia niko tayari. Kwa hivyo, sasa kama hazijaletwa sisi tutazileta zitakuwa zipo. Nasikiliza maelezo kutoka kwako.

Mhe. Mwenyekiti: Katibu, Waheshimiwa Wajumbe, ni hivi kwamba taarifa ambayo anaisoma waziri sasa hivi haipo hapa ndani na kutatakiwa kidogo kwenda kuangalia hiyo taarifa tayari kama imeshafikishwa au haijafikishwa Barazani. Sasa na tumwachie basi Waziri aisome taarifa na baada ya hapo tutapata. Mhe. Waziri.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, taarifa zetu zimeshawasilishwa Barazani leo asubuhi na mtu mmoja anaitwa Ndugu Khamis.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naheshimu sana kiti chako, lakini nadhani ushauri ulioutoa kwamba unatushauri tuendelee mimi nadhani utatupa tatizo Wajumbe wako.

Mhe. Mwenyekiti, msingi wa shughuli za Chombo cha Kitunga Sheria ni kufanya kazi na nyaraka hasa linapokuja suala la kupokea ripoti na hili swali limo ndani ya Kanuni. Tuna ripoti za aina mbili katika mjadala huu unaondelea; kuna ripoti ya Kamati na ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya mwaka uliopita kwa kila waziri husika jambo ambalo ilikuwa ni ubunifu wetu katika Baraza hili.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ukisema tuwasilishiwe tu, kwa kawaida huwa hatupewi mapema na tunaelewa, lakini angalau pale waziri anaposoma na sisi huna tuna karatasi zetu, kama kuna jambo unataka kulichangia kuja kulitolea ufafanuzi ni hapa ndipo tunaweka alama. Sasa tunapokuwa hatuna akiwa waziri asome tu na atakapokuja jioni pengine tukitoa pengine kuna mwengine anaendelea mjadala unaendelea, tutakuwa hatuwi na mjadala wa maana...

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nimekuelewa Mhe. Ismail Jussa, naomba ukae kitako. Nimekuelewa na mimi nimeshauri na bila shaka katika ushauri kuna kukubaliana au vipi, tupo kwenye demokrasia hapa. Kwa hiyo, cha kufanya sasa hivi ina maana kwamba hatuwezi kuendelea mpaka hapotutakapoipata ripoti. Nafikiria hilo litakuwa ni jambo ambalo tumekubaliana wote kwa pamoja Waheshimiwa Wajumbe, tutamwacha Mhe. Waziri aje awasilishe ripoti yake jioni baada ya kupata ripoti ya maandishi.

Sasa kwa maana hiyo kwa sababu bado Waheshimiwa muda tunao, lakini hata na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma na yeye aliomba kusoma taarifa yake jioni kwa sababu hajawa tayari.Kwa maana hiyo inanilazimisha kumuomba Mwanasheria Mkuu atengue Kanuni kwa ajili ya kuakhirisha kikao hadi jioni, Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe hoja ya kutenga kando Kanuni ya muda ya 23 ili tuakhirishe kikao hadi jioni leo saa 11:00.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa michango yenu pamoja na utulivu wenu kwa siku hii ya leo saa hizi mchana, basi niwaombe jioni tufike mapema wote, ili tuweze sasa kusiliza taarifa tatu ikiwemo ya Waziri wa Katiba na Sheria, ikiwemo ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma na ikiwemo na ya Mwenyekiti wa Kamati wa Katiba, Sheria na Utawala. Baada ya kusema hayo naakhirisha hadi saa 11:00 jioni. Ahsanteni sana.

(Saa 5:42 asubuhi Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2013/2014

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii, lakini mwanzo kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuwa na afya na tukafika hapa muda huu kwa kujadili masuala yetu ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria ilianzishwa baada ya uchaguzi Mkuu wa Oktoba, mwaka 2010 chini ya kifungu cha 42(1) cha Katiba kinachompa mamlaka Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuunda Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali. Kwa ujumla Wizara iliundwa kuratibu shughuli za sekta ya sheria na kusimamia utoaji haki, kutoa huduma za usajili wa biashara na mali, usajili wa matukio ya kijamii na usajili wa haki miliki, kusimamia mali za wakfu na mali za amana na kusimamia shughuli za Afisi ya Mufti. Majukumu hayo yanatekelezwa na taasisi zifuatazo:

Mahakama, Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, Afisi ya Msajili wa Haki Miliki, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Afisi ya Mufti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mipango Sera na Utafiti na Afisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa shughuli zake za kawaida kwa mwaka wa bajeti 2013/2014, Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala ilifanya kazi na Wizara ya Katiba na Sheria na ilitoa maoni na maagizo kadhaa kwa Wizara. Maoni na maagizo hayo yametekelezwa kama ifuatavyo, lakini maagizo hayo yalikuwa kwa Taasisi 7 tu kati ya 12 ambazo Wizara inazo.

Kwanza ni Mahakama ambapo kulikuwa na maagizo 6:

La kwanza, Serikali ifanye juhudi ya kuyafanyia matengenezo majengo ya Mahakama na pia ijenge jengo jipya la kisasa kwa ajili ya Mahakama Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, majengo ya Mahakama Mkuu Vuga, Mahkama ya Kadhi ya Wilaya ya Mwanakwerekwe, Mahakama ya Wilaya ya Makunduchi na Mahakama ya Mwanzo Chwaka, yamefanyiwa matengenezo makubwa. Matengenezo kama hayo yanaendelea kwenye jengo la Mahakama Kuu Chake Chake Pemba.

Wizara sasa inapanga kuyafanyia matengenezo majengo ya Mahakama ya Mkoa Kaskazini Unguja iliyoko Mfenesini, Mahakama ya Wilaya ya Mjini iliyoko Mwanakwerekwe na jengo la Mahakama ya Wete Pemba. Kwa upande mwengine Serikali imeshatoa kiwanja kwa ajili ya ujenzi jipya la Mahakama Kuu Tunguu Wilaya ya Kati

Unguja. Kazi inayofuata ni uchoraji wa ramani na makisio ya gharama ya ujenzi huo, kazi ambayo imepangwa kufanyika kwenye bajeti ya mwaka ujao tukijaaliwa wa 2015/2016.

Agizo la pili, lilikuwa ni Wizara iombe nafasi zaidi za ajira mpya Serikalini ili kuziba pengo la uhaba wa wafanyakazi katika sekta ya Mahakama hasa Kisiwani Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imechukua hatua kwa lengo la kupunguza tatizo hilo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mahakama iliruhusiwa kujaza nafasi 15 kwenye kada mbali mbali kwa Mahakama za Pemba na nafasi 23 kwa Unguja ili kuziba nafsi zilizoko wazi. Hatua za kujaza nafasi hizo zinachukuliwa baina ya Mahakama na Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma na tunategemea muda mfupi ujao suala hilo litakuwa limepata ufumbuzi na kupunguza uhaba wa wafanyakazi.

Agizo la tatu, lilikuwa Wizara ifanye uchunguzi kuhusiana na malalamiko ya tuhuma ya baadhi ya majaji, mahakimu, kujihusisha na vitendo vya kupokea rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba yamekuwepo malalamiko ya aina hiyo ya kuwatuhumu baadhi ya majaji na mahakimu kujihusisha na vitendo vya kupokea rushwa na kuendesha kesi kwa upendeleo. Kama nilivyoeleza kwamba hizo ni tuhuma na kwa kuwa ni tuhuma inabidi zisithibitishwe kwanza ndipo hatua zichukuliwe kwa wahusika.

Serikali kwa kuwa inakerwa kwa vitendo vya aina hiyo na kwa kuzingatia misingi ya utawala bora imeanzisha Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi, ambayo tayari imeshaanza kazi. Wizara yangu imewasiliana na Taasisi hiyo na kuiarifu kuhusu malalamiko hayo ili iyafanyie uchunguzi. Uchunguzi utakapothibitisha ukweli wa tuhuma hizo, hatua za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa kwa wale watakaobainika. Vile vile, katika shughuli zake taasisi hiyo imekuwa ikishajihisha wananchi kwenda kutoa taarifa kwenye taasisi hiyo wanapobaini kuwepo kwa matendo ya aina hiyo.

Agizo la nne, Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Kamati imeiagiza Wizara kuangalia utaratibu wa kuongeza maslahi kwa watumishi waliopo katika Mahakama za Mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeshachukua hatua ili kulipatia ufumbuzi tatizo la mishahara kwa mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo ambao walikuwa wanalalamikia udogo wa mishahara yao hasa Mahakimu kwa sasa mbali na mishahara inayoendana na elimu zao, pia, kila hakimu analipwa posho la Shs. 250,000/= kwa mwezi.

Agizo la tano, ni kwamba Wizara iongeze bajeti kwa Mahakama za Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla kuna tatizo la udogo wa bajeti kwa mfumo mzima wa Muhimili wa Mahakama ukilinganisha na ukubwa wa taasisi hiyo na tatizo hilo halipo kwa Mahakama za Pemba pekee. Wizara inafanya juhudi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kuongeza bajeti ya Mahakama ili iweze kutekeleza majukumu yake kulingana na ukubwa wa mtandao wake ambao umeenea kuanzia Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama za Mkoa na Mahakama Kuu kwa upande mmoja. Na kwa upande mwengine Mahakama ya Kadhi ambayo iko kwenye ngazi ya Wilaya, Kadhi Mkuu na Mahakama Kuu inapofikia hatua ya rufaa.

Juhudi hizo zimekuwa zikipata mafanikio kiasi kila mwaka katika miaka ya karibuni, kwani mgao wa fedha kwa ajili ya bajeti ya Mahakama umekuwa unaongezeka ingawa si kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji ya Mahakama, hii ni hali halisi kwa Wizara zote. Hakuna Wizara inayopata fedha zinazotosha kwa mahitaji yake yote, hata hivyo mazungumzo ya kuiongezea fungu Mahakama yanaendelea ili kupata nafuu kwenye mgao wa bajeti ya Mahakama Unguja na Pemba.

Agizo la sita, katika Mahakama kwamba Kamati iliiagiza Wizara kulipatia ufumbuzi tatizo la usafiri linaloikabili Mahakama Pemba.
Mhe. Mwenyekiti, hali hiyo inatokana na tatizo tulilolitaja hapo juu la upungufu wa fedha kwenye bajeti ya Mahakama. Tunalichukulia agizo hili na kuangalia uwezekano wa kutenga fedha kwa ajili ya kununua gari angalau moja kwa kuanzia ili kupunguza tatizo la usafiri kwa watendaji wa Mahakama Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika Ofisi ya Mwanasheria Mku kulikuwa na maagizo mawili:

La kwanza, Kamati inatoa msisitizo kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kulitunza jengo jipya la Ofisi ili iweze kudumu kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imepokea imepokea ushauri wa Kamati na katika kulifanyia kazi agizo hilo, Ofisi itakuwa inatenga fedha kwenye bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya kufanya matengenezo kila inapohitajika.

Agizo la pili, Ni kuwa kwamba Kamati inaishauri wanasheria wa Tume ya Kurekebisha Sheria watambuliwe kwenye Sheria Nam. 6 ya 2013 kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili na wao waweze kutambulika kihadhi na kimaslahi.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imepokea ushauri wa Kamati na ushauri huo unazingatiwa. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imekaa na Tume ya Kurekebisha Sheria ili kulijadili suala hilo na kuona kwamba kuona iwapo kuna haja au uwezekano kisheria wa kufanya hivyo kwa maslahi ya Ofisi zote mbili na maslahi ya nchi. Tunapaswa kukumbuka kwamba Ofisi zote mbili zimeanzishwa kwa mujibu wa sheria hivyo katika kulifanyia kazi suala hilo, ni lazima matakwa ya sheria zilizoanzishwa Ofisi hizo yazingatiwe kwanza kabla ya kufikia uamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi nyengine ya Wizara yangu ni Tume ya Kurekebisha Sheria ambayo kulikuwa kuna maagizo matatu.

La kwanza, Kamati imeshauri Serikali iipatie Tume ya Kurekebisha Sheria jengo la zamani la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili liweze kutumika kwa shughuli za Tume.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali tayari imelifanyia kazi suala hilo, Tume ya Kurekebisha Sheria imepatiwa jengo hilo kuanzia tarehe 24 Februari, 2014 na baada ya kulifanya matengenezo jengo hilo Tume imehamia kwenye jengo hilo na inaendelea na majukumu yake ya kawaida.

Swali la pili, Kamati imeishauri Serikali iangalie tena suala la mishahara kwa watumishi wake ili iweze kuweka sera sahihi ya ulipaji wa mishahara kwa ajili ya kuondoa malalamiko ya watumishi yanayohusu viwango tofauti wanavyolipwa kwa watumishi wenye kazi zinazolingana.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inayohusika na mambo ya utumishi imekuwa ikilifanyia kazi suala hilo tangu yalipofanyika marekebisho makubwa ya maslahi ya watumishi.Mara kwa mara hatua za kufanya marekebisho zimekuwa zikichukuliwa ili kusawazisha kasoro zinazojitokeza. Wafanyakazi wa kada na taasisi mbali mbali wakiwemo Madaktari, Mahakimu na Waendesha Mashtaka wa Ofisi ya *DPP* ni kati ya wale waliowahi kufaidika na marekebisho hayo.

Kwa kuwa suala la maslahi ya watumishi ni nyeti na tata, bila shaka malalamiko hayatasita kuwepo miongoni mwa watumishi wa umma. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara husika itaendelea kuyashughulia malalamiko ya aina hiyo kila yanapojitokeza ili marekebisho yafanyike kila inapoonekana kuna hoja za msingi.

Mhe. Mwenyekiti, agizo jengine ni kwamba Kamati imezishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Mahakama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Tume ya Kurekebisha Sheria kukaa pamoja na kujadili upya suala la mishahara kwa wanasheria wao.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili limejadiliwa na Wizara kwa kuzihusisha taasisi hizo katika nyakati tofauti na Wizara kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi. Kwa kuwa suala la mishahara linahusisha mambo mengi ukiwemo uwezo wa Serikali kulipa fedha zinazodaiwa hatua zimekuwa zikichukuliwa za kupunguza pengo la malipo baina ya pande zinazohusika. Lakini kwa tahadhari na kuzingatia uwezo uliopo. Hivi karibuni wanasheria wa Ofisi ya *DPP* wamepatiwa nyongeza ya maslahi yao.

Ya tatu, ni kwamba Kamati imesisitiza umuhimu wa wanasheria wa Tume ya Kurekebisha Sheria, maslahi yao kuangaliwa upya kwenye Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu hasa katika suala la maslahi ya wanasheria hao.

Mhe. Mwenyekiti, agizo hili limekwisha kutolewa maelezo kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Ya tatu, Kamati imeshauri Wizara ya Fedha kuingizia Tume ya Kurekebisha Sheria fedha zilizopangwa katika bajeti ya Tume kwa wakati ili kazi zilizopangwa za kibajeti ziweze kutekelezeka kwa wakati na kufikia malengo yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufatilia utekelezaji wa suala hili, Tume imekuwa ikifanya mazugngumzo ya mara kwa mara na Wizara ya Fedha kuhimiza uingizwaji wa fedha za matumizi yake, pamoja na kuchelewa kuingizwa fedha kwa baadhi ya miezi, tatizo kubwa zaidi ni mgao usiofikia *ceiling* ya mahitaji halisi ya mwezi ya matumizi ya taasisi zetu ikiwemo Tume. Ni tatizo la jumla la Serikali kuwa na uwezo mdogo wa kifedha na kuhudumia bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe wito kwa taasisi zinazokusanya mapato kuongeza kasi za ukusanyaji mapato ili Serikali iwe na uwezo mkubwa wa kuhudumia bajeti yake.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi nyengine ni Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambayo kulikuwa na maelekezo matatu:

Kwanza, Kamati imeitaka Serikali kuangalia upya ukomo wa bajeti, yaani *budget ceiling* ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kuiongezea fedha za matumizi ili kuweza kutekeleza makukumu yake kama inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni taasisi inayojitegemea na imeanzishwa kwa mujibu wa sheria, Ofisi hiyo ina fungu lake la fedha yaani vote na inajipangia matumizi yake kwa kuzingatia ukomo yaani *ceiling* iliyotolewa.

Wizara imepokea ushauri wa Kamati na inaendelea kufanya mazungumzo na Wizara ya Fedha kwa lengo la kuongezewa fedha kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya *DPP* pamoja na taasisi nyengine za Wizara ambazo zinahitaji kuongezewa *ceiling* zao kwa sababu mbali mbali.

Agizo la pili, Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Kamati inashauri Mahakama ipatiwe mafunzo ya kuwajengea uwezo majaji wake ambao wanakosa ujuzi unaotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kupitia programu ya mabadiliko katika sekta ya sheria yaani *Legal Sector Reform Programme* imeendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wa vyombo vya sheria katika maeneo tofauti ya kiutendaji. Mafunzo hayo yanahusu usimamizi na uendeshaji wa kesi, uhalifu wa kimtandao, mikataba, utafiti na uandishi wa ripoti za sheria na yalishirikisha wadau wa sekta ya sheria na haki wakiwemo Majaji, Mahakimu, Mawakili na Wanasheria wa Serikali, Maofisa wa Jeshi la Polisi, Chuo cha Mafunzo na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Wahujumu Uchumi na Ofisi ya Mkemia Mkuu Zanzibar. Mafunzo kama hayo yataendelea kutolewa ikiwa ni sehemu ya mradi.

Hata hivyo, naomba kutoa angalizo kwamba sio ukosefu wa mafunzo pekee unaosababisha majaji na mahakimu kutotekeleza kazi zao kwa ufanisi bali pia huchangia na ukosefu wa maadili. Natoa wito kwa taasisi zinazoshughulikia maadili na rushwa kuelekezwa nguvu zao kwenye eneo hili ili wale wenye tabia zisizokubalika za kupindisha haki wapatikane na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi na kisheria.

Agizo la tatu, Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Kamati inaishauri Serikali iharakishe kuifanyia marekebisho Sheria ya Ushahidi ya 1917 ambayo imepitwa na wakati na haiendani na mazingira ya sasa ya Sayansi na Teknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria inafahamu kuwa Sheria ya Ushahidi ya mwaka 1917 imepitwa na wakati na haiendani na mazingira ya sasa kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria, sheria hiyo imeshafanyiwa mapitio na tayari imekabidhiwa Wizara kwa hatua zinazofuata. Wizara nayo imeanza kuiwasilisha kwenye vikao vinavyohusika vya Wizara kabla ya kuipeleka Serikalini na hatimaye Baraza la Wawakilishi.

Agizo jengine ni kuwa Kamati inaiagiza Wizara kushirikiana na Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma kujadili tena suala la malipo la Waendesha Mashtaka wa Ofisi ya *DPP* kutokana na mazingira magumu na hatarishi wanaofanyia kazi na maslahi madogo wanaolipwa.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya maagizo Nam. 2(a) na (b) ya Tume ya Kurekebisha Sheria ya Wizara inahusisha pia na utekelezaji bora wa agizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi nyengine ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali ambapo hapa kuna maagizo matatu:

Kwanza, Kamati inashauri Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali ipatiwe bajeti inayotosha kuiwezesha kutekeleza mahitaji yake ya matumizi ili ifikie malengo iliyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu inaelewa umuhimu wa kuipatia wakala wa usajili wa biashara na mali pamoja na taasisi nyengine zilizo chini ya Wizara yangu fedha za kutosha kwa ajili ya kuiwezesha itekeleze majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Lakini kama tunavyoelewa tunapata mgao wa bajeti kwa kiwango maalum yaani *ceiling* ambacho tunalazimika kukigawa kwa taasisi zote za Wizara. Ina maana tunapopata kiasi kikubwa tunagawana kwa taasisi zote kwa ukubwa wake na tunapopata kiasi kidogo tunagawana hicho hicho tunachopata kwa udogo wake kwa taasisi zetu zote.

Tungefurahi kuona taasisi zetu zikiwemo Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali zinapata fedha za kutosheleza mahitaji yao, lakini hali halisi ndio kikwazo chetu. Ugawaji wa raslimali unategemea kipato cha nchi na kama tujuavyo hali yetu ya kiuchumi bado haijatuwezesha kumudu mahitaji yetu kikamilifu. Pamoja na hayo jitihada zinafanyika kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili kuona mgao wa Wizara unaongezeka ili tuongeze mgao wa taasisi zetu ikiwemo Wakala wa Usajili wa Biasharana Mali.

Agizo la pili, Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Kamati inaishauri Serikali kurekebisha mfumo wake wa usajili na kuifuta sheria ya kampuni ili iweze kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala ya Usajili wa Biashara na Mali imo katika harakati za kufanya marekebisho ya mfumo wa usajili, kwa kuanzia marekebisho ya baadhi ya sheria zinazohusiana na shughuli za wakala yamefanyika na sheria nyengine zinaendelea kufanyiwa mapitio. Kufikia sasa Sheria ya Kampuni imefutwa na kupitishwa upya na Baraza lako mwaka 2014.

Sheria hiyo imeanzakutumika kuongoza shughuli za usajili wa mali na biashara. Sheria ya Ufilisi inaendelea kufanyiwa mapitio na ikikamilika itawasilishwa kwenye vikao vinavyohusika ikiwemo Baraza lako tukufu.

Sheria nyengine ambazo zinazosimamia mifumo ya usajili zimepangwa kufanyiwa kazi kwenye mpango wa kazi, wakala wa usajili wa biashara na mali kuanzia mwaka 2015/2016; ni Sheria ya Nyaraka, Sheria ya Majina ya Biashara na Sheria ya Jumuiya za Kiraia.

Vile vile, Wizara imetayarisha Rasimu ya Kanuni za Sheria ya Kampuni na Sheria ya Dhamana zinazohamishika. Kwa upande mwengine Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha inafanya mawasiliano kwa karibu kwa ajili ya kutafuta fedha kwa ajili ya kandarasi ya kutengeneza mfumo wa usajili yaani *registration system* na mfumo wa utunzaji kumbukumbu yaani *database* kwa ajili ya taasisi hizo.

Agizo la tatu, Kamati inaishauri Serikali kuwaongezea maslahi wataalamu wa fani muhimu kama vile *IT* ili kuwatunza wasikimbie wanapoajiriwa kwenye taasisi za umma.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kuelezea masikitiko yangu kwa kadhia hii inayozikabili taasisi mbali mbali za umma zikiwemo taasisi za wizara yangu na hasa wakala wa usajili wa biashara na mali. Taasisi hii ilikuwa na wataalamu watatu wa *IT* mpaka katikati ya mwaka 2012, lakini sasa imebakiwa na mtaalam mmoja tu ambaye pia anatumikia Ofisi ya Mrajis ya Vizazi na Vifo ambayo nayo hivi karibuni iliajiri mtaalam mmoja wa fani hiyo, lakini aliondoka kabla ya kumalizika mwaka mmoja.

Hali hiyo si nzuri na inarudisha nyuma kasi ya maendeleo ya taasisi zetu, najua ziko sababu kadhaa zinachongia tatizo hili, lakini sababu kubwa ni kukimbilia kipato zaidi.

Naungana na Kamati kwamba njia moja ya kuwadhibiti wataalam wa fani hiyo na fani nyengine zenye ushindani wa kimaslahi kwenye soko la ajira ni kuongeza kiwango cha maslahi ya watumishi wa aina hiyo. Tunashukuru kwamba jambo hilo limeanza kufanyiwa kazi kwa wataalamu wa *IT*. Serikali hivi karibuni imeongeza mishahara ya wataalamu kwa baadhi ya fani ikiwemo *IT*. Tunatarajia Serikali itaendelea kuongeza maslahi ya wataalam hao wa fani maalum wakiwemo *IT* ili kuwatunza wasikimbie na kuongeza ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi nyengine ni Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ambayo ilikuwa na maagizo matatu:

AGIZO LA KWANZA

Kamati imeagiza Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kujitahidi kuilinda na kuitunza misikiti asili kwa lengo la kutunza historia ya nchi yetu. Pia, Kamati imeitaka Kamisheni kutoa misaada katika maeneo ambayo yana mazingira magumu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imepokea maoni na maagizo hayo na inayafanyia kazi kwa kuyaingiza katika mpango kazi wake kwa mwaka ujao wa fedha. Hata hivyo, Kamisheni haina jukumu la moja kwa moja kutunza misikiti iwe ya sasa au ya zamani, isipokuwa ile iliyokuwepo kwenye taratibu za wakfu. Hii ni misikiti ambayo ama imewekwa wakfu au inahudumiwa kutokana na wakfu zilizowekwa kwenye mali za aina mbali mbali hasa majengo na ardhi.

Kwa upande wa misaada ni utaratibu wa kawaida kwa Kamisheni kutoa misaada inayopatikana kwa kuzingatia maeneo yenye mahitaji makubwa yakiwemo hayo yenye mazingira magumu. Wizara yangu itaendelea kusimamia Kamisheni na kuingoza katika kudumisha utamaduni huo mzuri.

AGIZO LA PILI

Kwamba Kamati inashauri migogoro ya baadhi ya mashamba ya Kamisheni ya Wakfu itatuliwe kwa njia zinazostahiki na hatimae mwenye haki ya kumiliki mashamba hayo arudishiwe.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni inaendelea na mpango wake wa kuyarejesha kwenye wakfu mashamba ya wakfu ambayo yametoka kwenye usimamizi wake kwa sababu yoyote ile. Ingawa kazi hiyo si rahisi kutokana na mashamba hayo kuwa mikononi mwa watu kwa muda mrefu na ambao wanaendelea kuyatumia kwa uzalishaji na wengine kwa kujenga majengo ya kudumu kama vile shamba la Mfenesini, shamba la Kifoi na kadhalika.

Vile vile, Kamisheni inajitahidi kuipatia ufumbuzi migogoro inayotokana na mashamba ya wakfu ambayo yana migogoro ili wale wanaostahiki kufaidika na wakfu wa mashamba hayo wafaidike.

AGIZO LA TATU

Kwamba Kamati imeagiza Kamisheni ya Wakfu iendelee kuwaelimisha wananchi kuhusu mawakala wa safari za Hijja kwa ajili ya kuepusha usumbufu uliowahi kutoa siku za nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Wakfu ina utaratibu wa kawaida wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala mbali mbali yakiwemo ya Hijja na mawakala wa safari za Hijja. Vipindi vya taaluma hutolewa kwa njia ya redio na televisheni, mawakala nao kwa upande wao hujitambulisha kwa kujitangaza kupitia vyombo vya habari ili kuhamasisha watu kujiandika kwenye taasisi zao kwa ajili ya Hijja. Hivyo, hatutarajii kutokea usumbufu uliotokea siku za nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, agizo jengine la taasisi yangu ni Ofisi Kuu Pemba ambapo kuna maagizo mawili.

AGIZO LA KWANZA

Kamati imeagiza wizara kusimamia uingizaji wa fedha kwa Ofisi Kuu ya wizara Kisiwani Pemba iweze kupata mgao wa fedha za matumizi yake kwa wakati kutoka Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa sasa Ofisi Kuu za Wizara za SMZ zilizoko Pemba hupatiwa mgao wa fedha zao za matumizi, yaani *OC* kutoka Hazina moja kwa moja bila ya kupitia Makao Makuu wa Wizara zao. Katika hali ya kawaida fedha hizo huingizwa wakati wa mgao unapofika, lakini ni kweli kwamba kuna wakati mgao wa fedha huchelewa kunapotokea upungufu wa fedha kutoka Hazina na hali hii haitokei kwa taasisi za Pemba peke yake.

Kuna miezi ambayo hata Makao Makuu ya Wizara haziingiziwi fedha kwa wakati na hulazimika kusubiri hali inaporuhusu. Hata hivyo, Makao Makuu ya Wizara ya Katiba na Sheria kama zilivyo wizara nyengine hulazimika

kufuatilia upatikanaji wa fedha pale inapobidi kwa ajili ya kazi za makao makuu, Ofisi Kuu Pemba na taasisi nyengine za wizara hata zile zenye mafungu yao binafsi (*votes*)

Mhe. Mwenyekiti, agizo la pili, ni kwamba Kamati inashauri wizara iwapelekee watendaji wake Kisiwani Pemba gari nyengine ambayo itaisaidia ofisi katika shughuli zake za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa matumizi ya taasisi za Serikali zinaendeshwa kwa kufuata bajeti. Ofisi Kuu Pemba kama zilivyo taasisi nyengine na kifungu cha matumizi yake (*sub-vote*) na matumizi yake yote yanatakiwa kupitia kifungu hicho. Iwapo Ofisi Kuu Pemba inahitaji gari kwa matumizi yake inapaswa kujuulishwa makao makuu juu ya suala hilo na kuweka kwenye bajeti yao fedha za kununulia gari unayohitaji. Kwa kawaida wizara hutoa kipao mbele kwa taasisi zenye mahitaji zaidi ya matumizi ili kutimiza lengo fulani zikiwemo sababu za msingi.

Wizara itafanya hivyo pia kwa Ofisi Kuu ya Pemba ili kuhakikisha inapata gari kwa ajili ya shughuli zake baada ya Ofisi Kuu kubainisha kwenye bajeti yake kwamba inahitaji gari.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, baada ya taarifa hiyo naomba kumaliza kwa kutoa shukurani kwako wewe binafsi kwa uongozi wako wa busara, pia, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano na ushauri wao katika kusimamia mipango ya maendeleo wizarani kwa kipindi tulichofanya kazi kwa pamoja.

Mwisho, nawashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao ambayo itasaidia na imesaidia kutimiza malengo ya wizara yangu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha ripoti. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru *Subhana Wataalah* kutujaalia wakati huu kuwasilisha taarifa yetu ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi.

Lakini pia, nikushukuru wewe vile vile Mhe. Mwenyekiti kwa kutukubalia ombi letu la kwamba tuiwasilishe baadae kidogo kutokana na matatizo mbali mbali yaliyojitokeza.

Na tatu, niombe radhi kwamba tunawasilisha ripoti sio katika viwango vyangu vya kawaida, kwa hivyo, inabidi tufanye hivyo kutokana na hali halisi ya kiutendaji. Lakini hata hivyo, taarifa nashukuru Mungu watendaji nawashukuru wamejitahidi sana na hatimae imepatikana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumshukuru tena Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima, hekima, busara na afya njema na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kama inavyoelekeza sheria na taratibu za nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, natumia fursa hii kuipongeza na kuishukuru kwa dhati Kamati ya Katiba, Sheria, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wake wote. Kamati hii kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri wametupatia katika shughuli zetu mbali mbali za kiutendaji ili kutimiza majumuku hayo.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii ina lengo la kutoa maelezo ya utekelezaji wa maagizo, ushauri wa Kamati ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma katika ripoti hiyo kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba uniruhusu niwasilishe mbele ya Baraza hili tukufu taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma katika ripoti ya Kamati ya mwaka 2013/2014.
Mhe. Mwenyekiti, jumla ya maagizo 26 yalitolewa na Kamati na kupatiwa ufafanuzi kwa utekelezaji wa wizara yetu kwa niaba ya idara, taasisi sita zinazohusika ambazo ziko hapa chini zinaonekana.

Mhe. Mwenyekiti, katika maagizo hayo 26, la kwanza Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa.

AGIZO NI KWAMBA

Kamati inaiagiza wizara kuingiza fedha za matumizi ya kazi zote muhimu zilizokwama. Utekelezaji wizara imechukua hatua na kurikebisha tatizo la ukosefu wa fedha na tayari imeshatekeleza kazi zifuatazo ambazo zimekamilika ikiwa ni pamoja na uwekeji wa mitambo ya *CCTV*, pia, imenunua vifaa kwa mradi wa *digitalization*.

AGIZO LA PILI

Kamati imeiagiza wizara kuhakikisha kuwa kabla ya kikao cha bajeti cha mwaka 2014/2015, mipango ya *CCTV* uwe umekamilishwa na mpango wa ulinzi wa eneo hilo uwe umekamilika.

Utekelezaji, mradi wa uwekaji wa *CCTV camera* umekamilika ambapo *camera* 64 zimefungwa. Ufungaji wa mtambo huo utasaidia kwa kiasi kikubwa suala la ulinzi na usalama wa nyaraka. Hatua za kupata walinzi wenye mafunzo zinachukuliwa.

AGIZO LA TATU

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaishauri Serikali kuipa utulivu idara hii kwa kuiacha kuihamisha hamisha, wizara hii kila inapotokea mabadiliko ya miundo ya wizara na taasisi za Serikali. Agizo hili tumelipokea na wizara italizingatia.

AGIZO LA NNE

Kamati inapendekeza katika kuipa idara hadhi, idara hii ni afadhali iwe taasisi inayojitegemea na kupokea ruzuku moja kwa moja kutoka serikalini. Ushauri huu utaanziwa kufanyiwa kazi ili kuiwezesha Idara ya Nyaraka kuwa taasisi inayojitegemea ambapo Rasimu ya Sera ya Nyaraka na Kumbukumbu ya Taifa na Sheria zina mwelekeo huo.

Kamisheni ya Utumishi wa Umma

AGIZO LA KWANZA

Mhe. Mwenyekiti, ni kuongezewa muda kwa Makamishna wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

UTEKELEZAJI

AGIZO LA KWANZA

Limetekelezwa na Makamishna wa Kamisheni wameongezewa muda wa miaka mitatu baada ya kumaliza muda tarehe 27 Septemba, 2014. Muda wa uteuzi mpya umeanzia tarehe 30 Septemba, 2014.

AGIZO LA PILI

Kamisheni kupatiwa fedha za kutosha kwenye bajeti. Agizo limetekelezwa hali ya upatikanaji wa fedha kwa Kamisheni kwa sasa inaridhisha, Kamisheni imeweza kununua gari ya ofisi aina ya *Hyundai Minibus* kwa matumizi ya ofisi na ziara za Makamishna.

AGIZO LA TATU

Kupatiwa ufumbuzi wa tatizo la kuhama hama kwa wataalamu wa fani muhimu. Agizo hilo linaendelea kushughulikiwa Serikali kupitia Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma imo katika mchakato wa kupitia upya mishahara, maslahi na fursa mbali mbali za watumishi ikiwemo uhamishwaji wa fedha ya malipo ya watumishi wa umma.

AGIZO LA NNE

Serikali isaidie Kamisheni kupata jengo la ofisi la kudumu. Agizo hili linaendelea kushughulikiwa, majadiliano na taasisi zinazohusika kuhusu Kamisheni kukamilishiwa jengo liliopo Maisara yanaendelea. Kamati itajuulishwa hatua zaidi zitakazofikiwa.

AGIZO LA TANO

Kukamilishwa kwa Kanuni za Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 2011. Agizo limetekelezwa Kanuni ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 2011 imeshatolewa mwezi wa Septemba, 2014. Jumla ya Kanuni 166 zimesambazwa katika taasisi za umma Unguja na Kanuni nyengine 134 zinatarajiwa kusambazwa katika taasisi za umma Pemba.

AGIZO LA SITA

Elimu zaidi itolewe kwa watendaji wakuu na watumishi wa umma. Katika kutekeleza agizo hili mikutano 10 kati ya uongozi wa Kamisheni na viongozi watendaji wakuu wa wizara, bodi na taasisi za SMZ zilifanywa Unguja na Pemba.

Idara ya Ajira

Agizo, wizara iendelee kutoa elimu kwa wananchi wanaotafuta ajira nje ya nchi kupitia mawakala wanaotambuliwa na Serikali kwa ajili ya usalama wa kulinda haki zao wanapoondoka.

UTEKELEZAJI

Katika kusimamia sheria ya ajira Nam. 11 ya mwaka 2005, idara imewapatia elimu na taarifa muhimu zinazohusiana na kazi zao katika kulinda usalama na haki za wananchi wetu nje ya nchi. Ofisi imekuwa ikiwaelekeza mawakala kuhakikisha kwamba wananchi wanaosafiri wanakuwa na mikataba halali ya kazi, wanawapatia taarifa muhimu za nchi wanazokwenda. Kuwajuulisha juu ya mila na desturi za waajiri wa nchi wanazokwenda. Aidha, tumekuwa tukiwaunganisha makawala wetu na Balozi zetu za Tanzania nje ya nchi kuwezeshwa kupatiwa msaada unaofaa.

Idara ya Afya na Usalama Kazini

AGIZO LA KWANZA

Idara ifanye kazi kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria katika sehemu hatarishi kwa wafanyakazi kama vile Idara ya Nyaraka na Kumbumbu za Kitaifa ambapo wafanyakazi wake wanafanya kazi katika mazingira hatarishi. Idara inaendelea na kufanya ukaguzi, kutoa taaluma na ushauri juu ya masuala ya usalama wa afya katika sehemu za kazi.

Ushauri uliotolewa ni pamoja na kuwafanyia uchunguzi wa afya wanaofanya kazi kwenye mazingira hatari ya kiafya ili wale wanaopatikana na matatizo waweze kuhudumiwa.

AGIZO LA PILI

Kuwapatia wafanyakazi vifaa vya kinga zikiwemo nguo maalum za kazi hasa wale wanaotumia *chemicals* na wanaofanya kazi kwenye maeneo yenye mavumbi.

AGIZO LA TATU

Kuweka mfumo mzuri wa mzunguko wa hewa, mwangaza wa kutosha na kudhibiti harufu katika sehemu tofauti za kazi.

Pili, Agizo la idara hii ni usimamizi wa utekelezaji wa sheria Nam. 8 ya mwaka 2005 uharakishwe. Utekelezaji wa sheria Nam. 8 ya mwaka 2005, usalama wa afya kazini unakwenda vizuri kwa waajiri, waajiriwa na jamii. Idara

ikishirikiana na taasisi tofauti na kwa kutumia fursa zinazopatikana kutoa taaluma za usalama wa afya kazini, taaluma hii inawasaidia waajiri na jamii kufanya kazi kwa usalama zaidi.

Agizo la tatu, Kwa idara hii miongozo ya Sera ya Afya na usalama kazini iharakishwe ili idara ifanye kazi kwa vile Sheria ya Afya ya usalama kazini imetungwa tokea mwaka 2008.

Utekelezaji, Matayarisho ya Sera ya Usalama wa afya kazini yanaendelea vizuri na ipo kwenye hatua ya tafsiri.

Pili, Pamoja na sheria hii Idara ya Usalama wa Afya Kazini inatumia mikataba ya *ILO* pamoja na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika kutekeleza majukumu yake.

Chuo cha Utawala wa Umma

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeishauri wizara kumaliza bakaa ya malipo ya ujenzi wa mkandarasi aliyejenga majengo ya chuo ambalo mpaka leo halijamalizwa.

Utekelezaji, Bakaa ya malipo ya ujenzi kwa mkandarasi haijamalizwa wizara imechukua hatua ya kufanya mawasiliano na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kumalia bakaa hiyo ya mawasiliano na mawasiliano yanaendelea.

Pili, Kupatiwa ufumbuzi wa changamoto za uhaba wa majengo kwa vile kuna idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga na chuo huku nafasi za majengo ikiwa haitoshelezi.

Utekelezaji, Ujenzi wa jengo la Chuo cha Utawala wa Umma unaendelea na ukamilishaji wa ghorofa ya kwanza.

Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Mwenyekiti, agizo la kwanza kwa Ofisi Kuu Pemba, Kamati ilitembelea taasisi za ofisi Pemba ikagundua hakuna ushirikishwaji wa kutoshwa Afisa Mdhamini Pemba katika shughuli za *E-Government*.

Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba inashirikishwa vya kutosha katika usimamizi wa uendelezaji wa *E-Government* Pemba. Kamati inaiagiza Serikali kuhakikisha upatikanaji wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kupewa Idara ya Nyaraka kwa vile jengo linalotumiwa hivi sasa na idara hiyo liko katika hali mbaya halifai kwa shughuli za uhifadhi wa urithi wa Taifa.

Utekelezaji, Jengo lililokuwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya limeshakabidhiwa Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma na wizara iko katika hatua ya kulifanyia matengenezo jengo hilo kwa ajili ya shughuli ya uhifadhi wa nyaraka.

Agizo la tatu, Sambamba na maagizo yaliyotolewa katika Idara ya Nyaraka Unguja, Kamati pia inaiagiza Serikali kuwapatia fedha Idara ya Nyaraka Pemba kwa ajili ya kununua vifaa vya uhifadhi nyaraka kama vile *scanner, mask,* dawa za kutibu nyaraka zilizoharibika.

Utekelezaji, Ushauri umepokelewa na wizara inalifanyia kazi agizo hilo.

Nne, Kamati inaishauri Serikali kufanya uhakiki na mapitio ya mishahara kwa umakini kwani kumejitokeza tatizo la wafanyakazi wengi serikalini wa kiwango kimoja cha elimu kulipwa mshahara tofauti na wengine kulipwa mshahara tofauti na viwango vyao vya elimu. Tatizo hili lipo sana Wizara ya Elimu, Afya na Kilimo. Hivyo, Kamati inaiagiza tatizo hili kupatiwa ufumbuzi wa haraka. Agizo hili linafanyiwa kazi ili kuondoa kasoro hizo.

Agizo la tano, Ukosefu wa watumishi wa Tume ya Utumishi Pemba ni changamoto ambayo Kamati inaishauri Serikali kuwapatia ufumbuzi ili kuharakisha upatikanaji wa huduma ya Tume hiyo kwa wananchi wa Pemba bila ya usumbufu. Agizo linafanyiwa kazi ili kuondoa changamoto hiyo.

Sita, Kamati inapendekeza Serikali kuupa nguvu mpango wa kutanua huduma za Chuo cha Utawala wa Umma Pemba. Hatua zimechukuliwa na Chuo cha Utawala wa Umma kimeshafungua tawi lake Pemba.

Maagizo ya jumla kwa wizara. Agizo la kwanza, Kanuni za Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2000 ziwe tayari kabla ya kikao cha bajeti cha mwaka 2013/14. Kanuni za Sheria ya Utumishi wa Umma zimekamilika na kusambazwa na kuanza kutumika katika wizara na taasisi za Serikali.

Pili, Changamoto za Idara ya Nyaraka zipatiwe ufumbuzi haraka kabla ya kikao cha bajeti cha mwaka 2013/14. Changamoto mbali mbali za Idara ya Nyaraka zimeshapatiwa ufumbuzi zikiwemo uwekaji wa Kamera za *CCTV* na kuanza kufanyiwa kazi kwa mradi wa *Digitalization*.

Agizo la tatu kwa jumla, Kamati kupatiwa mchanganuo wa matumizi ya *E-Government* ambayo imeombwa muda mrefu bila ya kufanikiwa. Wizara imewasiliana na Wizara ya Fedha ili kupata mchanganuo huo wa matumizi ya mradi huo wa *E-Government*.

Nne, Serikali iwe na utaratibu wa kutoa taarifa Barazani juu ya hatua za kinidhamu na kisheria zinazochukuliwa juu ya wafanyakazi wanaotuhumiwa au ripoti mbali mbali zinazosomwa na Kamati katika Baraza la Wawakilishi. Agizo limepokelewa na linashughulikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho, nachukua nafasi hii kukushukuru na kuwashukuru Wajumbe kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha.

Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kwa Mwaka 2014/2015

Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Mwenyekiti, naomba kusoma Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na ya uzima na tukakutana tena hapa katika kujadili mambo ya msingi ya kulijenga Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala naomba kuchukua nafasi hii adhimu kutoa mkono wa pole kwa wananchi wa Jimbo la Magomeni kwa kuondokewa na Mwakilishi wao ambaye alikua ni nguzo kubwa ya kujenga msingi imara wa hoja katika Baraza hili. Aidha, nawapa pole wanachama wa Chama cha Mapinduzi kwa msiba huo pamoja na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, ama hakika mapenzi ya Mwenyezi Mungu yametimia na hatuna budi kumuombea mwenzetu apumzike kwa amani.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuipa Kamati yetu ushirikiano mkubwa uliotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa. Lakini pia, tunashukuru kwa kutupatia nafasi ya kueleza japo kwa muhtasari, ripoti ya Kamati inayotokana na kazi ambazo zimekuwa zikitekelezwa na Kamati kwa takriban mwaka mzima.

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha Kanuni cha 106(f) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2012 na majukumu yake yametajwa katika kifungu cha 113.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao ambayo yamewezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi mkubwa. Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:

1. Mhe. Ussi Jecha Simai — Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Bikame Yussuf Hamad — Mjumbe
4. Mhe. Nassor Salum Ali — Mjumbe
5. Mhe. Suleiman Hemed Khamis — Mjumbe
6. Mhe. Wanu Hafidh Ameir — Mjumbe
7. Ndg. Aziza Waziri Kheir — Katibu
8. Ndg. Khamis Hamad Haji — Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilifanya kazi zake kwa utaratibu wa kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya wizara pamoja na taasisi zake na baadae kutembelea na kukagua utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na taasisi hizo.

WIZARA YA NCHI, (AR), TAWALA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu ilifanya ziara katika wizara hii na kupokea taarifa za utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu, pamoja na kukagua miradi mbali mbali ya maendeleo kwa lengo la kuona jinsi utekelezaji wa bajeti unavyofanyika na kutoa maelekezo yatakayosaidia kuongeza ufanisi katika kazi za kila siku za wizara. Kamati baada ya kufanya ziara ilipata nafasi ya kushauri, kutoa maagizo pamoja na kutoa maoni yake pale yalipohitajika.
Mhe. Mwenyekiti, Kamati imetoa maoni na maagizo yake kwa kina katika maeneo mbali mbali ya wizara. Hata hivyo, muhtasari huu unaeleza baadhi ya mambo ambayo Kamati inaona kuwa ni muhimu sana kwa ajili ya kuisaidia Serikali katika utekelezaji wa malengo yake kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo enedelevu katika nyanja zote. Baadhi ya maeneo ambayo Kamati imeona ipo haja ya kuyaweka katika muhtasari huu ni kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

Tume Ya Utumishi Ya Idara Maalum

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Idara Maalum za SMZ zinafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na zinafuata utaratibu wa kisheria katika masuala ya ajira, Kamati ilifanya ziara katika Tume ya Utumishi ya Idara Maalum kwa lengo la kujionea taratibu za ajira zinavyofanywa na kupata majibu sahihi ya baadhi ya maswali ambayo wananchi wengi wamekuwa wakiyaulizia kuhusiana na masuala ya ajira katika Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati iliwahi kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wafanyakazi wa Idara Maalum hasa wa Idara ya Chuo cha Mafunzo Makao Makuu, walidai kuwa walipewa barua za likizo ya ugonjwa kinyume na utaratibu. Wafanyakazi hao walidai kuwa hawakutendewa haki kwa kulazimishwa kupewa likizo ya ugonjwa hali ya kuwa ni wazima na huku wakiwa katika likizo zao za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia ilipata taarifa kuwa wafanyakazi hao waliwahi kupata maradhi wakiwa kazini, lakini idara ikashindwa kuwasaidia huduma za matibabu, isipokuwa iliwapatia barua za kuwastaafisha kwa ugonjwa baada ya kupata nafuu. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa jambo hilo lilifanyika kwa baadhi ya wafanyakazi huku wafanyakazi ambao walikuwa ni wagonjwa waliachwa wakiendelea na kazi hali ya kuwa hali zao kiafya ni mbaya wanaugua vitandani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kupokea malalamiko hayo, Kamati iliyafanyia kazi kwa kuonana na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum na kuiagiza kufuatilia malalamiko hayo kwa kukutana na wahusika na hatimae kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa, kuchukuliwa kwa taratibu za kisheria kwa watumishi wote ambao ni wagonjwa na hawawezi kuendelea na kazi kwa kuwapa haki zao zote na kutoa nafasi kwa vijana wengine kuchukua nafasi zao.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hali hiyo, Kamati ilisikitishwa sana na mazingira iliyoyakuta katika Afisi za Tume kutokana na kuwa afisi hizo haziendani na uhalisia wa chombo chenyewe. Kamati ilipofanya ziara katika tume hiyo, ilielezwa changamoto mbali mbali zilizopo katika tume ambapo miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na eneo linalotumika kwa ajili ya ofisi za tume kuwa katika eneo finyu, ambapo Katibu wa Tume anatumia eneo moja dogo na Katibu Muhutasi pamoja na watendaji wengine. Hali hii inasikitisha sana kutokana na hadhi ya tume kutoendana na mazingira yake ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuitafutia tume ofisi zitakazoendana na hadhi ya tume yenyewe, pamoja na kuifikiria Tume ya Utumishi ya Idara Maalum kwa kuiwezesha kuwa na fungu lake katika bajeti badala ya kuwa na kasma katika matumizi ya wizara. Aidha, Kamati inaiagiza tume kuchukuwa hatua dhidi ya malalamiko ya baadhi ya wafanyakazi wa Chuo cha Mafunzo, Makao Makuu ambao Kamati inamashaka kuwa taratibu za kuwapa likizo ya ugonjwa hazikufuatwa kwa mujibu wa sheria.

Idara Maalum za SMZ

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia ilipata nafasi ya kufanya ziara katika Idara Maalum za SMZ, ambapo ilijionea juhudi za msingi zinazochukuliwa na idara hizo katika kuhakikisha kuwa zinajikwamua katika baadhi ya changamoto

zilizopo katika maeneo yao ya kazi. Kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuvipongeza vikosi vyote vya SMZ kwa juhudi wanazozichukua pamoja na hali ngumu ya ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zao za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Chuo cha Mafunzo Unguja na Pemba na kukutana na changamoto mbali mbali katika kambi za Chuo cha Mafunzo. Kamati inachukua nafasi hii kueleza kwa masikitiko makubwa kabisa kutokana baadhi ya kambi za chuo kuwa katika hali mbaya na kutofaa kabisa kwa matumizi ya ofisi.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida Kamati ilishangazwa na hali ya kambi ya Kengeja, ambapo majengo ya ofisi hayafai kabisa hali iliyopelekea Kamati kukaa chini ya mwembe kupokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti. Aidha, katika kambi hiyo na nyenginezo zilizopo Unguja na Pemba zinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa makaazi ya askari pamoja na gereza lililokuwepo kuanguka kwa upepo kutokana na kuchakaa sana.

Mhe. Mwenyekiti, Gereza la Wete nalo hali yake ni mbaya sana ambapo eneo la Ofisi ya Kamishna wa Idara ni sehemu ndogo tu, ambayo ni chumba na Kamati ilishanganzwa sana na hali hiyo kutokana na udogo wa chumba hicho na kutokuwa na nafasi ya kutosha kwa matumizi ya oifisi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu imeeleza kwa kina zaidi katika Ripoti ya Kamati kuhusiana na hali ilivyo katika Chuo cha Mafunzo. Kwa ufupi hali ya majengo ya kuishi wanafunzi, majengo ya nyumba za askari pamoja na majengo yanayotumika kwa shughuli za kiofisi katika maeneo mengi ya Idara ya Chuo cha Mafunzo ni mbaya sana. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hali ya tahadhari kwa kuangalia vipaumbele vyake vya maendeleo na kuiingiza idara hii katika mpango wake wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kutatua changamoto zilizopo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hali hiyo, Kamati ilisikitishwa sana na taarifa ilizopatiwa kisiwani Pemba na baadhi ya wakuu wa kambi kuwa hawashirikishwi katika uandaaji wa bajeti. Hali hii hupelekea shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa bajeti kukwama kutokana na ukosefu wa fedha na kutojua kinachoingizwa katika maeneo hayo. Hivyo, Kamati inamuagiza Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo kuhakikisha kuwa kinapofika kipindi cha kuandaa bajeti ya idara anawaalika wahusika wote kutoka kisiwani Pemba na wanapofika katika kikao hicho kila mmoja ajue kiwango halisi cha fedha kinachoingizwa katika kambi yake.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia ilipata nafasi ya kufanya ziara katika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ambapo hali kama kawaida ni mbaya katika baadhi ya kambi kutokana na changamoto kubwa inayozikabili baadhi ya taasisi za Serikali ya ukosefu wa fedha. Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti ikiwa imesimama kwenye uwanja wa eneo la kambi ya Zimamoto iliyopo Mkoani nje kutokana na kambi hiyo kuwa na ofisi zisizokuwa na mazingira rafiki ya kufanyia kazi pamoja na ufinyu wa eneo lenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilisikitishwa sana na hali hiyo na hasa ikizingatiwa kazi ngumu zinazofanywa na askari hao katika jamii. Kamati inasisitiza umuhimu wa kuvipa kipaumbele Vikosi vya SMZ katika maeneo mbali mbali ikiwemo majengo ya ofisi kutokana na unyeti wa shughuli zinazofanywa na vikosi hivyo. Aidha, Kamati inashauri askari wa kikosi cha Zimamoto wote waliokosa makaazi katika kambi za kikosi hicho walipwe fedha zao za *house allowance* ili waweze kulipia gharama za makaazi.

Mhe. Mwenyekiti, Idara Maalum zina changamoto nyingi kiasi ambacho kila Kamati ilipokuwa inakagua katika kambi mbali mbali za vikosi hivyo, ilitegemea kukutana na changamoto zaidi ukilinganisha na mafanikio ya utekelezaji wa malengo ya mwaka ya kibajeti. Hata hivyo, Kamati inachukua nafasi hii kuvipongeza sana vikosi vyote vya SMZ kwa juhudi zao.

Mamlaka Za Serikali Za Mitaa

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka za Serikali za Mitaa zina majukumu mengi ya kutoa huduma moja kwa moja kwa wananchi. Aidha, majukumu hayo yanaendana na shughuli za kuwaingizia kipato wananchi kiasi ambacho Mamlaka hizo zinapotekeleza majukumu yake zinapaswa kuwa makini na huduma wanazozitoa, ili kuepusha malalamiko yanayotoka kwa wananchi kutokana na ubovu wa huduma wanazozipata na kukiukwa kwa utaratibu katika maeneo mengi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipokea taarifa ya ujumla ya wizara ambapo ilielezwa kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa wataalamu katika fani mbali mbali, wanaohitajika katika kuendeleza mamlaka hizo kufikia hatua mabayo itawezesha mamlaka hizo kujisimamia na kutoa huduma nzuri kwa wananchi.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ilizishauri mamlaka hizo zihakikishe kuwa zinaajiri wataalamu wa fani mbali mbali ili kuimarisha utendaji kazi katika kila ngazi . Aidha, kutokana na uwepo wa sheria mpya ambayo inatoa miongozo katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali za Mitaa, Kamati imeagiza matakwa ya sheria hiyo mpya yatekelezwe kwa kila Serikali ya Mtaa kusimamia majukumu yake ipasavyo.

Wizara Ya Katiba Na Sheria

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu ilitembelea taasisi mbali mbali za wizara hii na kukagua miradi kadhaa inayotekelezwa na taasisi hizo. Baada ya kutembelea na kuona utekelezaji wa shughuli hizo, Kamati ilitoa maoni, maagizo na ushauri kwa wizara na taasisi zake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Afisi Ya Mkurugenbzi Wa Mashtaka

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ina jukumu la kusimamia mashtaka na kufungua kesi katika Mahakama kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki inatendeka. Kamati ilifanya ziara katika afisi hii na kupokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Unguja na Pemba ambapo ilipokea changamoto mbali mbali zilizopo.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtakata inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti na majukumu ya kazi ni mengi ambayo yanaathiriwa na bajeti ndogo. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa bajeti inayokadiriwa kutolewa kwa mujibu wa makisio yaliyokubaliwa hayatolewi kwa kutosheleza ambapo Ofisi ya *DPP* ni kubwa ukilinganisha na taasisi nyengine za Serikali ambazo zina majukumu madogo, lakini bajeti zao ni kubwa. Hivyo, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuiongezea afisi hiyo bajeti ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati kisiwani Pemba ilipata taarifa kuwa kuna tatizo la mtaalamu wa kuchunguza maiti *(Pathologist)* na kupelekea ushahidi kukosekana. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kulishughulikia tatizo hilo ili haki iweze kutendeka pamoja na kuongeza idadi ya wakemia watakaosaidia kurahisisha kazi za waendesha mashtaka.

Wakala Wa Usajili Wa Biashara Na Mali

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara katika Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali na kuelezwa changamoto mbali mbali kama zinavyooneshwa katika kitabu cha Ripoti za Kamati. Kutokana na changamoto hizo, Kamati imetoa ushauri na maagizo kwa kuiomba wizara kufanya juhudi za kuitenganishwa na ofisi ya vizazi na vifo kisiwani Pemba kama ilivyo Unguja ili taasisi hizo ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Afisi Ya Mrajisi Wa Vizazi Na Vifo

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa eneo la ujenzi wa ofisi katika Wilaya ya Wete. Kamati ilielezwa kuwa eneo linalotumika hivi sasa kwa matumizi ya ofisi kisiwani Pemba hali yake hairidhishi na ipo ndani ya jengo la Afisi ya Mkuu wa Wilaya, ambapo hali ya eneo hilo ni mbaya sana na kufanyiwa ukarabati ni gharama kubwa. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kutafuta eneo kwa ajili ya ofisi na kuepuka usumbufu unaojitokeza hivi sasa kwa watendaji wa ofisi hiyo na kuondoa kabisa tatizo la kuhama hama kwa ofisi ambapo hupelekea baadhi ya kumbukumbu muhimu kupotea.

Wizara Ya Nchi, (Ar), Kazi Na Utumishi Wa Umma

Wizara hii ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa linazingatia haki za watumishi wote serikalini pamoja na kuzingatia maslahi ya wananchi wote, sambamba na kuliangalia suala la ajira na kulipa uzito kwa kuhakikisha kuwa idara husika inalisimamia suala hilo kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imeundwa na taasisi mbali mbali kama zinavyooneshwa katika kitabu cha Ripoti za Kamati, ambapo muhtasari huu unaelekeza kwa ufupi tu yale yaliyojitokeza katika ripoti hiyo katika idara na taasisi mbali mbali za wizara hii kama ifuatavyo:

Idara Ya Miundo Ya Taasisi, Utumishi Na Maslahi Ya Watumishi

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipofanya ziara kisiwani Pemba katika idara hii ilielezwa kilio cha muda mrefu cha wafanyakazi wa idara hii, kiasi ambacho baadhi ya watendaji wanahisi kama Kamati haifanyi kazi ipasavyo ya kuishauri Serikali kutokana na changamoto zilizopo kujirudia rudia kwa muda mrefu na kila Kamati inayokwenda kisiwani Pemba kuelezwa changamoto hizo pasina mafanikio yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa, idara haina bajeti yake jambo ambalo linaisababishia idara hiyo kukosa fedha za kutekeleza majukumu iliyojipangia. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa yale inayoyashauri kwa wizara na Serikali kwa ujumla yatekelezwe ipasavyo ili baadhi ya watendaji ambao wanahisi Kamati za Baraza la Wawakilishi zinakwenda katika taasisi hizo kutembea tu na sio kutekeleza majukumu yake yaweze kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inayazungumza haya kutokana na hali iliyojitokeza wakati wa ziara za Kamati, ambapo ilionekana kama vile Kamati hazifanyi wajibu wake wa kuishauri Serikali ipasavyo kutokana na ushauri na maagizo ya Kamati kutotekelezwa ipasavyo. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali iyafanyie kazi haya inayoyashauri ili isionekane kuwa Kamati hazitekelezi wajibu wake.

IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilisikitishwa sana na taarifa iliyopewa kisiwani Pemba kuwa Idara kwa hivi sasa ina changamoto ya kutofanya ukaguzi katika taasisi za Serikali na inafanya kazi ya ukaguzi kwa kuangalia usalama wa wafanyakazi katika taasisi binafsi tu kutokana na kutokamilika kwa muongozo wa wafanyakazi wa Serikali ambapo muongozo huo haujakamilika tokea mwaka 2005 sheria ilipoelekeza hivyo.

Kamati inaagiza kukamilishwa kwa muongozo huo ili ukaguzi ufanyike kwa taasisi zote za Serikali na za binafsi.

IDARA YA AJIRA

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipofanya ziara kisiwani Pemba ilielezwa kuwa Idara inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa usafiri ambapo Idara haina usafiri tokea mwaka 2010 na wanaazima gari kwa Kamisheni kwa ajili ya kufanya shughuli zao za kila siku. Kamati imesikitishwa sana na taarifa hiyo na inaiomba Wizara ifanye utaratibu wa kuipatia Idara usafiri wake.

HITIMISHO

Katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na Sheria nyenginezo, Kamati imetoa maelekezo, maoni, ushauri na maagizo yake ambayo tunaamini kuwa yatasaidia katika kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma.

Maelekezo na maoni hayo yalitolewa na Kamati kwa dhamira ya kuwawakilisha vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao, kwa mujibu wa sheria yanapewa kipaumbele. Kamati yetu inatumai kuwa maelekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati kwa Wizara hizo yatazingatiwa kwa lengo la kutoa huduma zilizotukuka kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi inaushukuru uongozi wa Wizara zote zilizo chini ya Kamati kwa ushirikiano mkubwa walioupatia Kamati yetu katika kipindi chote cha kazi za Kamati kwa Unguja na Pemba.

Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Pandu Ameir Kificho, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza

majukumu yake vizuri, lakini zaidi kwa ushauri walioupatia Kamati yetu katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yake.

Mwisho kabisa, Kamati inawashukuru Makatibu wa Kamati hii kwa kutekeleza majukumu yao ya kuisaidia Kamati na Wajumbe wa Kamati ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.
Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Wanu Hafidh unaombwa kutoa hoja, hujatoa hoja.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa hivi tunaaza kuchangia ripoti na taarifa zilizotolewa na Mawaziri pamoja na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. Mchangiaji wa mwanzo ni Mhe. Makame Mshimba, anayefuata ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baada ya hapo sina mchangiaji. (*Makofi*)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia hizi ripoti tumepewa leo hii na tumepewa ripoti mbili au wizara tatu lakini vibuku ni viwili. Kwa kuwa Mheshimiwa hizi ripoti ni kitu ambacho ni muhimu sana hasa kwa Wajumbe katika kujadili na kutafakari na kutoa mawazo. Kwa kuwa leo ni wizara tatu zimewasilisha ripoti zao kwa wakati mmoja, Mheshimiwa muongozo wangu naomba kwako kwa nini tusiweze kuzibagua leo tukaanza na wizara moja na kesho tukaendelea na wizara nyengine na hasa kutokana na hali ngumu ya ripoti hizi. Kwanza Mheshimiwa naomba nipate muongozo wako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kwa utaratibu wetu tunachangia wizara zote tatu usianze kutuvuruga hapa. Tunachangia wizara zote tatu na umeomba Mhe. Makame Mshimba tangu asubuhi kujua kwamba utakuja kuchangia hivi jioni, nakuomba uendelee na uchangiaji wako.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu huo kwenye kanuni haumo lakini mnatufanyia lakini twende hivyo hivyo ahsante, tutapiga humo humo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na wizara ya mwazo itabidi sasa Mhe. Mwenyekiti, tutapiga hivyo hivyo tu kwa sababu hata kwenye kanuni hamna hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niingie katika wizara iliyowasilisha mwanzo ya Idara Maalum hiyo. Mhe. Mwenyekiti kwa kweli inasikitisha sana Waziri simuoni sijui atanijibu nani, watu juu naona siwaoni Mhe. Mwenyekiti, namuona mtu mmoja sasa leo sijui tunafanya kazi gani Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti kwa wakati mmoja nilimuona Mhe. Waziri wangu Mhe. Abubakar Khamis alitizama watu kule akaona hana watu akatikisha kichwa. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, hatuko makini hasa kwa kusema ukweli na ripoti hizi ambazo ni ripoti muhimu wanatusikiliza wananchi ripoti zinasema nini leo angalia juu hamna watu.

Tizama wenzetu sasa siku zote nasema sheria gani tunakuwa tunazitumia. Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa nikae kitako nisichangie kwa kuwa sioni atakayenijibu sioni Waziri wala sioni kule juu ambao watakaoweza kumsaidia Waziri atakapojibu. Mhe. Mwenyekiti, *message* imefika. Mhe. Mwenyekiti, *message* imefika, waziri kaingia lakini watu wake sijaona kusogea mbele sijaona hao makamanda wala sijaona nani pale. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti naendelea. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niulize katika wizara hii mara nyingi sana huwa mimi nauliza tunapotunga sheria au tunapofuata sheria hasa katika wizara mnapotuletea sheria zao au wanavyozitoa zile sheria huwa wananukuu katika nchi gani au kamusi gani. Kwa sababu mimi naomba sana nianze na suala ambalo linasikitisha sana, lakini kwenye ripoti humu sijaliona nimejaribu kulitafuta sijaliona.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba utaratibu mmoja kutokana na hali ya kila siku hili suala nilisema leo nilikuwa naliotea usingizini na *inshaallah* Mwenyezi Mungu amenibariki kaniweka hai niweze kulisema.

Mhe. Waziri hebu leo ukitoka nje, aah Mheshimiwa usimfundishe Mwenyekiti. Mheshimiwa usimwambie tusome kwenye ripoti, sasa si tunachangia Mwenyekiti tutizame huku Mwenyekiti nazungumza mimi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna ripoti humu ndani kasoro hazimo, sasa ripoti zile lazima tuzisaidie na ndio kuchangia yenyewe ripoti na wizara ndiyo husika. Sasa zinapokuwa hazimo lazima tuziseme, Mhe. Mwenyekiti, umenifahamu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kumuomba Mhe. Waziri kutokana na hali ambayo sasa hivi msongamano mkubwa sana, wa kutopelekea wananchi hawajui wakae wapi, hawana vituo vya kudumu, hilo tumesema tuliseme, kwa sababu imekuwa zogo, imekuwa tatizo, sasa nalo ni la msingi lakini humu kwenye ripoti halimo kwa nini tusiliseme.

Wananchi leo kila kituo hujui kiko wapi pale CCM wamejaa tele, watu kila sehemu hili tuliseme tulitafutie ufumbuzi wa haraka mpaka tusababishe ajali. Sasa nalo hili nawajibika kulizungumza kwa mujibu wa taratibu.

Sasa hiyo namuomba sana Mhe. Waziri alitafakari nalo hilo. Kwa kuwa halimo kwenye ripoti lakini tumelisema sana kwenye Baraza hili kituo cha daladala Mhe. Mwenyekiti, wanapata shida warejeshewe kituo cha zamani, na ndio maana tukasema kiutaratibu tuweze kuzungumza na kufuatisha katika sheria za wenzetu. Sasa sheria za wenzetu kila ninapokwenda vitu vya daladala vinakuwa katikati ya mji. Sasa leo hakijulikani kituo kiko wapi. Tunaomba sana hili suala tuondoe usumbufu hebu nenda *time* hizi za jioni Mhe....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe ninavyoelewa mimi utakuwa na nafasi nzuri ya kulizungumzia hili wakati wa Bajeti ambao sio muda mrefu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Vipi sijakusikia, hebu ongeza sauti.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba unisikilize, hapa sasa tunajadili ripoti na taarifa ambazo zimetolewa hayo ambayo yamo ndani ya ripoti. Kwa hiyo, naomba uende huko zaidi kuliko huko unakokuzungumza. Muda huo utapata wa kufanya hili.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, najadili ripoti na hii ndiyo ripoti na hii ni moja ya ripoti.

Itabidi sasa nitoe darasa, kuna ripoti ambazo zinakuwa *in report* na kuna ripoti *out report.* Sasa zote zinakuwa *included* katika hii daftari Mhe. Mwenyekiti, naendelea. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 17 lakini *message* imefika Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu idara hii ya Mikoa na Tawala za Mikoa ndio ninayozungumzia mimi sio wizara nyengine zozote. Maana yake sijui tunakusudia Wizara ya Afya simuelewi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika masuala ya Chuo cha Mafunzo. Kwanza niwashukuru sana viongozi wakuu wa Chuo cha Mafunzo lakini kama ulivyosema kuwa kwanza masuala ya mishahara nayo hii haimo kwenye ripoti?.

Mhe. Mwenyekiti, kusema la ukweli Vikosi bado fedha za mishahara haikidhi haja kila siku tunasema tunageuza tutatekeleza ni lini kwa sababu hawa askari wetu wanafanya kazi hichi kifungu cha tatu. Kila siku tunasema hii Idara ya Utumishi inavyoonesha haikamiliki kila siku imo tu. Kwa kweli hatuwatendei haki tunasema na hasa kwa mfano wenzetu wa idara hii wanalisha wanajibinya. Kwa kweli fedha zinazoingizwa katika idara zao zinakuwa ni kidogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, askari wetu hawa wanafanya kazi kubwa sana, tena kubwa sana lakini katika mambo ya mishahara hatuwafikirii, wapeni tu mzigo mzito. Mimi ningeomba sana hili suala la kila siku kuwa marekebisho ya Tume tuko mbioni mpaka lini na hili nalo limo ndani ya ripoti. Kwa kweli haileti taswira nzuri sana tunawatia unyonge askari wetu.

Mimi nilitoa wazo langu la kusema wizara hii iwe *dependent* kabisa na masuala ya Tawala za Mikoa, iwe *special* kuwa Wizara ya Vikosi Maalum kwa sababu nilikuwa naiombea iwe na bajeti yake lakini tafsiri imekuja vyengine, unajua kila mtu ana lugha yake au sehemu yake ya kutumia lugha.

Lengo na madhumuni kwa sababu sasa hizi wanapata bajeti kidogo na kila siku tunaambiwa na Waziri wa Fedha uchumi umeinuka, na kweli uchumi unainuka kila leo, lakini uchumi unainuka kunako *document* lakini ukienda hasa katika sehemu yenyewe utakuta uchumi uko chini. Sasa nikisema hivyo kwa sababu kwa nini tunashindwa

kuwafanyia mishahara yao iridhishe na wakati uchumi upo juu. Sasa hichi ndicho kitu ambacho kinanipa matatizo, kinanipa taswira ambayo sitoweza kuifahamu. Mwalimu wangu atakuja kunikosoa nini maana ya taswira.

Kwa hiyo, ninachoomba sana tuwe na marekebisho mazuri kabla ya kufika siku za bajeti. Nitakuwa mkali sana, nitavaa uso wa chui kabisa siku hiyo bajeti hii nitaing'ang'ania sana kwa sababu inasikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana nayo kuwe na sehemu ambayo nafikiria sijui jengo likoje la Chuo cha Mafunzo. Nashukuru sana hawa wenzetu wa Magereza sio wachoyo kusema ukweli maana yake niseme ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, hili la Chuo cha Mafunzo nitakuja kuleta hoja baadae nitakuja kuleta hoja maalum ya kuja kuondosha hii tuweke Magereza moja kwa moja. Maana yake naona iko mdomoni sana na inaniingizaingiza.

Mhe. Mwenyekiti, tunatembea Magereza ya wenzetu nilienda Zambia katika Mkutano wa *SADC* baada ya kumaliza ule mkutano ndio maana mnakuwa mnanipa tabu sana, kwa sababu kule sheria zikiwekwa zile sheria zinatakiwa ziendane na ile *East African* yenyewe Afrika Mashariki na sisi tupo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wamepiga hatua katika jengo zuri la Magereza sijui sasa hivi wenzetu nilisikia zamani sana Mhe. Waziri lile jengo lile la Magereza huku sijui vipi. Mhe. Mwenyekiti, hakuna mtu anayependa kifungo lakini Magereza niliyoyaona kule Zambia utatamani ufungwe. Kwa sababu Gereza lao ni zuri linaendana na wakati; vitanda vizuri, vyoo vizuri, kwa kweli wameendelea sana halafu wana *tools* zile za kufanyia kazi hata majiko yao yanakwenda na wakati sio sisi tuna majiko ya kukata kuni kila siku msitu unayoyoma.

Kwa hivyo, naomba sana na hilo naliunga mkono, Magereza hili jipya sasa hivi hatujui liko *standard* gani mpaka sasa hatuji likoje kama vizuri au vipi sijui, lakini naomba hili suala liweze kufanyika haraka sana.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombee sana askari wetu suala la mavazi. Kwa kweli anavaa mtu sare mpaka inachujuka ni suala ambalo linasikitisha sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa hiyo, naomba sana hili suala nalo lifikiriwe kwa wakati, na vile viatu sasa hivi utakuta mwengine anavaa viatu ambavyo haviendani na vile viatu vya kiaskari mtu, anavaa kiatu kutokana na hali halisi ilivyo, pamoja na kuwa bajeti yetu finyu lakini kuna mambo mengine tunahitajika kuweza kufanya suala la umuhimu.

Mhe. Mwenyekiti, niingie katika kikosi cha Magendo kwanza niwapongeze sana kwa Hospitali yao, hilo la kwanza japo nitaambiwa kuwa halimo katika ripoti.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya KMKM ni nzuri sana na vitendea kazi nimeona vizuri sana, wako *hard working* wanafanya kazi masaa 24. Hilo mimi nawapongeza sana Mhe. Mwenyekiti, lakini jitihada ya vifaa bado vingali finyu na tumeitegemea. Sasa hivi hospitali ile ambayo itakuwa muokozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja kama tunaiendesha vizuri kama tutaisaidia vifaa vizuri. Kwa kweli niwapongeze sana Makamanda mwenyewe Kamanda Mkuu na machifu wake hili suala limenifurahisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni kulitokea tatizo ambalo nilikuwa na wasi wasi nikasema mtume hapa kutakuwa hakuna dawa baada ya wananchi wangu kula mbegu zile za mbarika, lakini nikagundua imepatikana dawa mapema kabisa. Kwa kweli hili suala lilinifurahisha sana nikasema nilitolee baraka na niwashukuru ili na mimi Mwenyezi Mungu iwe kheri yao na mimi kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu hizi zana ziweze kufika katika wakati mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hili suala ni zuri Mwenyezi Mungu awajaalie waweze kupata vitu kwa wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, tukiingia katika changamoto ambazo kutokana na ndugu zetu wanazozipata kukabiliwa na hali halisi ya ufinyu huo kama wanavyosema wa bajeti zao. Hili suala ambalo lilikuwa uzoefu, kila siku tunasema na ndiyo maana tukasema hata maoni ya kamati inaeleza, hapa nimepata masikitiko sana, sasa tunakuwa tuna maana gani sisi Kamati. Hebu itakapofika Wizara ya Fedha kwenye ripoti kidogo hapa nitaweza kuogelea vizuri sana. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sijui vitabu hivi vingapi, kama utavichukua vitabu zaidi ya hamsini tulivyoanzia na Baraza changamoto hizi zimo tu haziondokani.

Mhe. Mwenyekiti, ninavyosikitishwa sijaona, haioneshi hata ile theluthi ya kusema kuwa changamoto hii imefikia kiwango moja, mbili, tatu. Imekuwa tena sijui niite nini changamoto au changabaridi.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana, lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hawa wenzetu ni watu ambao wa baharini na inavyotakiwa kisheria, ya kazi zao masaa ishirini na nne wawepo baharini kutokana na kutulinda katika ukingo wa bahari pande zote za bahari.

Siku hizi munajua mara leo nani wameingia huko wanakutwa, lakini utakuta sasa mtu wa kwenda kufuatilia hili jambo ana *fiber*, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, tulilisema sana suala tuondokane na dhana ya *fibre*.

Mhe. Mwenyekiti, *fibres* sasa hivi haziwezi kusaidia kitu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niingie na JKU.
Mhe. Mwenyekiti, JKU kama kweli tumekusudia kama JKT basi niseme minalfaidhina, lakini tunaichukulia JKU *just* ni JKU tu, kwa sababu wenzetu kule JKT kwa kweli wamepiga hatua kubwa sana na wao ni marafiki. Ni lazima wanakuwa wanaona aibu, wanaona uchoyo kwa kuwa sisi hatwendi vile kiutaratibu ulivyo. Sasa sijui tatizo lipo wapi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiria wapeni fursa hawa sasa hivi JKU, kama sheria za wenzetu kule zimetoa fursa na hawa JKU wapeni fursa.

Mhe. Mwenyekiti, tutakuwa tunawarundika vijana tu kule, wakitoka hawana taaluma. Taaluma kubwa ile *parade* tu, sasa hivi wapi inatakiwa mtu atoke na ujuzi; wa umeme, fundi kijiko, fundi bomba na mambo mengineyo. Halafu wanafanya biashara sasa hivi wenzetu. Sheria ya kuanzisha sheria ya Kuanzisha Kampuni ya ulinzi tushaipitisha hapa sijui imeishia wapi, sijaiona mpaka leo haujatiwa saini na Mhe. Rais, sijui vipi, angalau tulifikiria itasaidia ili kuokoa kwenye mahoteli humo majambazi wasiingie.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli inasikitisha sana. Niwashukuru sana kamati wameenda juzi, wameona raha zao. Mhe. Mwenyekiti, leo wenzetu wanafika kupata matrekta. Mhe. Mwenyekiti, musione tabu hawa wazalendo wafanyabiashara wetu, hebu naomba jamani sasa ninakusaidieni maarifa.

Mhe. Mwenyekiti, sheria tumeshaipitisha ya *PPP,* na sheria ile kama nilivyosema ilipata wataalamu, walipata watu wenye historia, ilipata watu wenye kufuata mifumo mbali mbali ya nchi mbali mbali na hatimaye leo *alhamdulillah* Mhe. Waziri kapeta, kapita vizuri, kiulaini kutokana na hali halisi. Waheshimiwa walivyosoma walivyoifahamu, unafanya mchezo wewe na semina, wamepata semina nzuri, wameelewa na ile ndivyo inataka, utupe kitu mapema kabla ya kuingia kwenye shimo. Wamefanya vizuri, wameelimisha vizuri hatimaye tumeipitisha.

Sasa hii sheria ya *PPP* Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hebu kukutana nao hawa wahusika watu wa Idara ya Mipango wakusaidie, wakutafutie watu wa aina hiyo, tusione tabu. Unajua tatizo letu sisi tunashindwa kufuatilia, hata mimi njoo uniite nitakutafutia matajiri wapo kabisa, maana yake utanidharau bure lakini usinidharau ninazungumza na watu wangapi, siku hizi mitandao ipo wazi, wala usione tabu hebu niite, wewe fanya kama masihara siku moja uniite, halafu leo unione, halafu kesho utakuja kunisifu pale kwenye kiriri utasema *yes*, Mheshimiwa ametuletea matajiri anakopesha matrekta. Kama ukinisifu sawa hukunisifu basi. *(Makofi).*

Lakini sasa hili ni tatizo letu, tunaona tabu kuwatafuta matajiri, ukakaa nao, ukazungumza nao ukafanya biashara ili kuweza kuleta tija. Hii kuleta vivespa, sijui vihonda, hii haisaidii kitu. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba sana, kwa sababu leo kwa mfano wenzetu wa Magereza wana kampuni yao sasa hivi lakini kijidogo cha kuwajengea nyumba askari. Ni vizuri sana lakini kwa kesho naamini wanaweza wakaendelea wakawa kampuni kubwa wakaendeleza kujenga majumba. Kwa kweli nimependa sana utaratibu huo, wanakopeshana kujenga nyumba kwa njia ya mkopo.

Sasa naomba sana Mheshimiwa *idea* yangu, kaeni na makamanda na unao wazuri tu wa uchu wa madaraka wa kazi hizi kutafuta maendeleo. Sasa watu kama hao ukiwa nao basi ujue mambo yanakwenda vizuri. Naomba sana Mhe. Waziri hili suala tusione tabu kwenda mara kwa mara kule JKT, usione tabu Mheshimiwa, nenda mara kwa mara mpaka utafika pahali pazuri, watakupatieni watu kule jinsi wale walianzaje nyinyi mulishindwaje.

Sasa hilo moja nimeona, hata maeneo yatafute sasa hivi ya kuweza kuwekeza masuala ya mboga mboga na masuala mengine, si trekta moja, mbili, tatu ambacho Mheshimiwa utapata shida sana.

Mheshimiwa niendelee na sehemu ya Idara ya Kazi. Mheshimiwa kuna hii wanaita Idara ya Nyaraka. Mheshimiwa Idara ya Nyaraka kwa kweli inasikitisha. Kwanza nisifu sana agizo tulililokuwa tukilisema la *CCTV*.

Mhe. Waziri hapa ametwambia kwa furaha kabisa, unajua Mhe. Waziri anapokuwa kafanya jambo lake zuri husoma kwa pozi kabisa pale. Kwa kweli ametwambia *CCTV* tayari ameshakamilisha ambalo hili suala tulikuwa tukilipigia kelele sana ili kunusuru nyaraka zilizobakia zisiibiwe. Hilo ninashukuru sana suala halina tatizo.

Lakini Mheshimiwa zipo karatasi zipo katika miaka mingi sana, tena zina miaka mingi sana. Na kitu chochote Mheshimiwa kikawa hakina *plan* ya kuwekwa vizuri kinaota mwani, kinakuwa kina mavumbi, kina matatizo na wale watu wetu ni binadamu.

Kwa hivyo Mheshimiwa wanakuwa wanaomba fedha za kuweza kujikimu kwa kufanya *check-up* ya afya zao. Mheshimiwa kwa kweli inasikitisha sana, tena ninakaribia kutaka kulia machozi. Kwa sababu Mheshimiwa afya ni kitu muhimu sana kwa binadamu, wakati wale wanafanya kazi, kila mara wanachezea ma-*chemicals*, halafu leo wanataka fedha za kwenda kutaka kujifanyia *checking* za afya zao, tunakuwa kila siku kesho, kesho tunategemea nini.

Mimi ninakuombeni sana Waheshimiwa kwa hili muwe *serious,* viongozi mukae kimya nitajua kama kweli muna uchungu na wananchi. Kwa sababu Mheshimiwa inasikitisha. Kuna mfanyakazi mmoja nasikia hivi karibuni alikuwa anakohoakohoa haijulikani kama lile vumbi ama majaaliwa ya Mwenyezi Mungu, lakini mtu atakuwa na wasi wasi, anaweza akasema labda inawezekana maskini ya Mungu mwenzetu yule ametutoka kutokana na lile vumbi, kaanza kukohoahoa kapoteza maisha, hii inakuja Mhe. Mwenyekiti.

Sasa mimi naomba kuna mambo mengine tunashindwa kuyatolea mchango wa hali ya juu, hatulifikirii. Tukisema meli tunaipata haraka sana basi hata hili. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana tuwe *serious* na hili suala kwa kweli inasikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Wizara ya Katiba na Sheria. Mhe. Mwenyekiti, tunalia na suala la rushwa. Tunasema rushwa lakini sasa rushwa huijui *control*, huitaki iwe imedhibitiwa rushwa kwa sababu ya kuwa basi tu, sijui kwa sababu gani. Humu tumesema kuwa mishahara ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, nilipiga kelele sana irekebishwe. Mhe. Mwenyekiti, hivi kweli tupo *serious* na wananchi wetu kweli.

Mhe. Mwenyekiti, maana yake tuseme ukweli hivi kweli tupo *serious* kweli. Na ndio maana utakuta kesi zina-*delay*, mtu asile rushwa. Hebu niambeni atakula rushwa kwa sababu hatumthamini. Leo utamkuta mtu Mahakama ya Mwanzo ana diploma halingani na mshahara na watu, anapata mshahara mdogo kabisa. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha na hili suala tulilisema sana.

Mhe. Waziri alisema ana-*fight* na mimi ninakubaliana naye kwa sababu hana uwezo wa fedha. Saa nyengine Mawaziri mimi siwatii makosani, nitakuja kuwatia makosani kwenye jungu kubwa, kwa sababu jungu kubwa ndiyo kwenye kasma zote zinazotakiwa kutolewa.

Wanajitahidi katika kufanya mambo mengine, tunaziona kweli Mahakama nyengine zinafanyiwa marekebisho, nakubaliana nalo. Mimi hilo sina tatizo kwa sababu Mahakama lazima ziende na wakati. Kwa mfano Mahakama ya Mwera tizama hali halisi ilivyo, ndiyo inavyotakiwa. Lakini ukiingia ndani Majaji wake fedha zenyewe haziendi haja na hizo Mahakama zenyewe zinavyotakiwa. Kwa hivyo mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hili suala la mishahara bado Serikali hatujawa *serious* kwa kuweza kulitekelezeka. Kwa nini, sijui napata shida sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hapa kuna kamati imesema imeshauri Serikali iangalie tena suala la mishahara kwa watumishi ambapo kamati hii ndiyo kamati ambayo ina uwezo wa kuishauri Serikali kwa mujibu wa sheria na Kanuni zetu za Baraza, na ndiyo tukaweza kuzichangia. Ndiyo maana nikakuomba muongozo kwa sababu kuna jambo Mhe. Mwenyekiti, lazima ukae ulitafakari na ulitolee jibu na uweze kulichangia kwa mujibu wa utaratibu. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mimi naomba sana viwango hivi bado haviridhisha kweli kwa hawa watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala la ma-*assessors* tumelisema sana. Ma-*assessors* leo wanafika sijui kama miezi minne mpaka mitano lakini kwenye ripoti linakuwa hamna. Basi haya jamani Mhe. Mwenyekiti, tusiseme ma-*assessors* na wale watu. Kwa kuwa kitu hakimo kwenye ripoti na jambo muhimu sana, linagusa jamii na ni haki yao.

Mhe. Mwenyekiti, inakuwa hatuwatendei haki, lazima tumekuwa tumelisahau tulijazie humu kwenye ripoti. Ma-*assessors* mpaka leo hii kwa kusema kweli Mahakama Kuu na Mahakama ya Mikoa hawajalipwa pesa zao, ni watu ambao wana watoto, watu ambao wana familia na wazee wao wanawategemea wale, hawajalipwa Mheshimiwa wameshachoka kukopa, watafungwa na wao. Kwa sababu itafika pahali watakuja kujadiliwa.

Mhe. Spika, sasa hilo naomba sana na wao kutokana na hali halisi ilivyo ma-*assessors* lazima na wao waweze kufikiriwa, walipwe kwa *time* ambayo inakubalika, na sababu gani sijui wanakuwa hawalipwi. Hichi kitu kinasikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na wizara hii, kwa kweli hapa kuna hili suala la kamati la Serikali kuangalia upya ukomo wa bajeti wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Mwenyekiti, tunafanya masihara sana kusema la ukweli. Mhe. Mwenyekiti, niseme moja katika Ofisi ya *DPP*. Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo ningeomba sana kwa kuwa ni wale watu ambao ndiyo ninasema sasa hivi ni kiungo cha sheria. Na kwa kuwa maslahi yao yanakuwa si mazuri, sidhani Mhe. Mwenyekiti, kama kutatendeka haki ya kupelekwa kesi Mahakamani. Ndiyo maana nikasema hebu tuangalie uwezo. Mimi sidhani kama Rais anaweza kukataa. Mimi nadhani sisi wenyewe Mawaziri, niweze kusema wazi, kwa sababu Mawaziri wawe *friendly* na Rais, lakini leo inakuwa pengine Waziri hataki kuwa *friendly* na Rais. Rais ni mtu ambaye ni binadamu. Rais ni mtu ambaye anakubali ushauri na kusikiliza, lakini ukianza aah! ati eti wanataka mshahara Mheshimiwa. Rais atafanya nini, atakuunga mkono asilimia kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ukimwambia upo *serious* Mheshimiwa kutokana na hali, hali ya hewa ina-*change* na mishahara i-*change* kutokana na hali halisi ilivyo, ukimuelekeza vizuri *wallahi* nakwambia Rais na hasa Dkt. Ali Mohamed Shein hakatai, atakwambia nenda katoe pesa, lakini wewe mpeleka ripoti unaanza ku-*doubt*, eeh! haki ya Mungu ninakwambia *chief* wanaanza ku-*doubt* wale watu wanaopeleka ripoti, unamwambia eti maana yake Mheshimiwa na nini lakini wao Makatibu Wakuu wanane wachukua mapesa chungu nzima. Kwa kweli hii inasikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala ambalo linasikitisha sana. Jamani kuna hizi *department* muhimu sana, musizifanyie masihara. Mimi nashangaa sana, maana yake sijui niseme nimekwambieni zamani twendeni kwa nchi za wenzetu tuka-*quote* vitu kama hivi. Vitengo kama hivi twendeni nchi za wenzetu, si kitu cha mchezo, wengine humu wanapewa ma-*body guards*, wanapewa nyumba za ulinzi. Sisi tupo *care* tu, sisi tunatunga sheria gani hapa. *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, hichi kitu kinashangaza kweli, tunatunga sheria gani. Leo Mwanasheria Mkuu yule pale hana hata ulinzi kwake, yupo *free man*, eeh! niseme ukweli kwa sababu si mchezo, roho ile ya Serikali, lakini watu wanakuwa, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, ni suala linasikitisha sana. *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, uende nchi za wenzetu, Jaji Mkuu unaambiwa au Jaji Msaidizi, Majaji wa Mahakama ya Mwanzo, nenda katizame katika nchi za wenzetu huko. Sasa mimi nikauliza hizi sheria tunatumia *SADC* za wapi hazimbulikani. Sasa kwa kweli *commonwealth* haziji sheria kama hizi. *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo tuwe *serious* na haya mambo. Kusema kweli yanasikitisha sana, tena inanisikitisha sana kutokana na hali ya uhalisia. Kwa sababu kuna mambo ambayo hatujaweka kukaa tukakubaliana. Humu muna ushauri, wakae Mwanasheria Mkuu, akae Mwendesha Mashtaka, akae Jaji Mkuu basi *wallahi* itatimia mwaka mzima hawajakaa, utafika muda wa mwaka mzima Mhe. Waziri hawa watu watakuwa hawajakaa ili waweze kupanga mustakabali mzuri wa wafanyakazi wao kupata mishahara, watakuwa hawajakaa, hili wazi tuseme.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninakubaliana na kifungu kinachosema sheria sasa zinapitwa na wakati. Nakubaliana nalo. Mhe. Mwenyekiti, leo sheria Mkoa inakataza kutoa ruhusa dhamana ya mtu anayekamatwa na silaha, lakini ikikatiwa rufaa mtu anapewa dhamana mtu aliyekamatwa na silaha akatolewa nje.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile mtu anaua anapewa dhamana mtu kama yule. Mhe. Mwenyekiti, sheria zinapitwa na wakati. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, ziangaliwe kwa vizuri kabisa kwa sababu ni suala ambalo linasikitisha sana kuwa watu kutokana na sheria za sasa hivi, sijui kwa sababu silaha ni kitu kibaya sana, mtu anaua vibaya vibaya, anamkata mtu vibaya vibaya, anapewa dhamana. Unatarajia nini, utampata tena unafikiria Mahakamani yule ukishampa dhamana ile, lakini sheria zetu zipo *open* zinaruhusu hivyo.

Sasa mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hili litamuhusu labda Mwanasheria Mkuu au Waziri mwenyewe atuletee mabadiliko. Ni kweli wananchi wanapiga kelele wanasema aah! mtu sheria na haki za binadamu sijui, haki zifanyike, mtu apewe dhamana. Sasa jamani dhamana basi za sheria hizo zipo kwa upande mmoja tu, haiwezekani. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana hili suala wakae wataalamu wanasheria wakuu, wakae wajifungie ndani waone jinsi gani wanaweza kurekebisha kwa njia ya upole kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona hapa Wizara imetengeneza programu ya mabadiliko ya sekta ya mambo za *legal* na mambo ya sheria kupita kuwaelimisha wananchi, vitengo husika, mawakili na halikadhalika. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, sijaona na jamii, tungeomba

na Masheha nao wakapewa taaluma katika haya mambo ya sheria za hapa na pale ili kuweza kufahamu nini utaratibu, kujua kesi ya jinai, kujua kesi ya madai kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti, nalo hili siyo baya kwa sababu watu wengi sana wana ukosefu wa kupata kujua sheria ambazo hazistahiki vizuri na utakuta mtu, Sheha au mtu mwengine, anafanya jambo bila ya kufikiria maskini ya Mungu, kumbe ile sheria hajui, anaweza akasema maneno mtu katika vyombo bila ya kufahamu anazungumza nini na hajui athari zake zitakuwa kitu gani.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana katika hizi programu zao za kupita kuelimisha, siyo hawa wakubwa tu Mapolisi, Majaji, Mahakimu, Mawakili na hawa vile vile Mheshimiwa.

Ningeomba sana hilo Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri afikirie na wao kushuka chini kuwaelimisha watu sheria, kwa sababu mtu hajui kama ukimtukana mtu tayari kosa unalo, hajui lakini ana raha tu kuweza kumchambua mtu na kuweza kumtakana, lakini ni kosa kubwa sana.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana. Kwa kuwa hichi kifungu unacho hapa kimejieleza kwa Wizara kupitia programu zake za mabadiliko katika sekta za sheria, mabadiliko ya hizi sheria ambazo zinaendeshwa mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wa vyombo vya sheria. Mheshimiwa nako huku twende ili huku waelewe na wao sheria ya mabadiliko ya sheria zinavyokwenda sasa hivi.

Na sasa hivi kama nilivyosema kuwa tunaomba sheria zibadilike kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kuna sheria nyengine zinasema kuwa mtu anaweza angalau kulipa au alipe milioni tano, maana yake angalau ile isipande isishuke lakini unaweza ile sheria ikaelekeza kuwa mtu anaweza kulipa laki moja na nini na sheria ikaona imefaa, lakini kumbe lengo letu ni kumpiga faini milioni tano.

Sasa mimi naona Mhe.Mwenyekiti, nalo hilo tuweze kurekebisha vifungu vidogo vidogo, vilugha vilugha vidogo vidogo vinamtoa mtu katika kesi kwa mujibu wa sheria inavyoendeshwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika utaratibu huu wa sheria na hasa kuhusu habari ya kesi za ubakaji. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana katika Ofisi hii ya *DPP,* kwa kweli hili suala naomba sana zikija ziwe *faster*, maana yake katika kesi ambazo hasa zinaanzia ku-*delay* katika uchunguzi wa mwanzo katika polisi.

Mhe. Mwenyekiti kwa kweli zinachukua muda sana, kwa kweli inafika pahali watu wanatokwa na imani na Jeshi letu la Polisi. Saa nyengine watu wasiojua wanasingizia hoo! wameshapeleka kwenye Ofisi ya *DPP*, ndio wengine wanaona hilo, kumbe pengine ukifuatilia unakuta ile kesi kule hata haijapiga hodi. Sasa na hili Mhe. Waziri naomba sana liangalie kwa makini, sasa hivi wimbi la ubakaji limekuwa ni kubwa sana na tishio kubwa sana. Hapa sio pahali pake leo lakini nataka nidokolee tu ili tuone ni jinsi gani utekelezaji wake utakavyokuwa katika uchunguzi.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu polisi hawajawa *serious* na suala hili. Wanawadanganya wananchi, wanasema kuwa tayari sisi tumeshakamilisha au tumo kwenye utaratibu, lakini *DPP* ameturudishia, wameturudishia kwa sababu wanatwambia tumekosea utaratibu, lakini kumbe wao wenyewe wame- *delay,* au pengine pale umeshatoka mshiko, watu wameshalishwa fedha pale pengine, inawezekana ikawa hivyo. Kwa sababu pengine hawa nao wanaofanya hili jambo, kwa sababu mtu anajiandaa, nafanya jambo hili na mimi nitaweza kuli-*control* kwa njia hii. Sasa nalo hilo Mhe. Mwenyekiti naomba sana, jambo limekuwa kubwa sana ni wimbi kubwa sana. Rai yangu ninayotaka kuitoa nitakuja kuitoa katika wizara husika.

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nimechangia baada ya hapo naomba kukaa kitako. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Makame Mshimba. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Waheshimiwa Wajumbe naomba kama kuna mchangiaji yeyote basi nafasi ipo baada ya Mhe. Ismail Jussa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Muumba wetu *Allah Subhanahu Wataala* kwa kuturuzuku neema zake za uhai na uzima na muda huu tukaendelea na shughuli zetu hapa.

Nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa na mimi kutoa mchango wangu katika mjadala au hoja hii ya Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na taarifa za utekelezaji za wizara tatu ambazo zinasimamiwa na kamati hii.

Ni imani yangu Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyomruhusu kutumia muda wa kutosha Mhe. Mjumbe aliyetangulia, maana nilikuwa naangalia alitumia zaidi ya dakika 40. *Inshaallah* saa yako itakuwa inaangalia hivyo hivyo kwa wajumbe wengine Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa masikitiko, na masikitiko kwamba ukipitia ripoti za kamati kwa jumla zote, lakini kwa sababu tunazungumzia kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala nitaizungumzia kamati hii, na ukiziangalia ripoti za utekelezaji za wizara unachokigundua ni kwamba serikali hii ime- *fail,* imeshindwa kazi. Kwa nini nasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kila mwaka unapokuja kusoma maagizo ya kamati unakuta yanajirejea yale yale. Hiyo maana yake nini Mhe. Mwenyekiti? Maana yake ni kwamba maagizo yaliyotolewa mwaka uliopita hayakufanyiwa kazi yako vile vile.

Kwa hivyo, kamati inarudi kufanya kazi inarejea maagizo yale yale. Nina hakika Mhe. Mwenyekiti, tukitizama ripoti za kamati tutagundua masuala haya haya yapo katika ripoti ya mwaka 2011/2012, 2013/2014 na sasa tuko 2015 kipindi cha lala salama kuelekea katika uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nimesema nasikitishwa na ninaona dalili ya kushindwa kazi, kwa sababu ninapoangalia ripoti za utekelezaji. Mhe. Mwenyekiti, ripoti hizi zinatoa taarifa katika chombo hiki cha wananchi; Baraza la Wawakilishi la wananchi wa Zanzibar, juu ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa mwaka jana kipindi kama hichi. Sasa Waziri baada ya miezi 12 anapokuja kutupa ripoti akasema wizara imepokea ushauri wa kamati na itaufanyia kazi na itauzingatia. Itauzingatia lini tena? Ningefahamu lugha hiyo ingekuja katika maagizo yanayohusu mwaka huu, lakini yanapokuwa yale ya mwaka jana, nilikuwa nasikiliza kwa makini hapa, tunaambiwa wizara imeupokea ushauri itauzingatia, wizara itaufanyia kazi, wizara itafuatilia.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika hali kama hii ndio maana hali halisi katika nchi imefika hapa ilipofika, kama nitakavyotoa mifano Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hii. Kwa hivyo, mimi kusema kweli nasema nasikitishwa sana na hali hii.

Moja ambalo niseme kwa jumla, kabla sijaingia katika sehemu moja moja. Sehemu nyingi na kama hiyo ndio sababu watakuja kutueleza wenyewe, utakuta maagizo hayakutekelezwa sababu iliyotolewa ni fedha.

Sasa mimi naomba Mhe. Mwenyekiti, tusaidiwe au kesho atakapokuwa anafanya majumuisho sijui, kwamba serikali hii hii inatutangazia na imemuaminisha mpaka Mhe. Rais na inatangaza hivyo hivyo, kwamba ukusanyaji wa mapato unaongezeka kila mwaka. Tutatoa vilinganisho kuonesha kwamba tumevuka *record* nyingi za miaka iliyopita.

Sasa tafsiri yangu mimi niliyekuwa sio mtu wa uchumi katika masuala haya, ngumbaro na mambo ya uchumi. Natafsiri kama mapato yakiwa yanaongezeka maana yake na ufanisi wa serikali utaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, takriban kila waziri aliyesoma hapa, maeneo mengi yaliyokuja katika utekelezaji halisi panalalamikiwa fedha. Sasa napata tabu zaidi kwa sababu mengi yaliyogusiwa hayahusu miradi ya maendeleo. Mimi natambua kwamba kutokana na hali halisi ilivyo katika nchi, miradi ya maendeleo takriban mingi inategemea fedha kutoka washirika wa maendeleo, lakini shughuli za mishahara na shughuli za matumizi mengineyo *OC's*, hizi zinatokana na fedha za mapato ya ndani. Sasa tunapoambiwa mapato yameongezeka tungetegemea kwamba tuyaone katika utekelezaji wa serikali, na Mhe. Mwenyekiti, mlinganisho uliotolewa ni kwamba zimeongezeka kutoka bilioni 17 zilizokuwa zikikusanywa kwa mwaka 2010, tumeambiwa zimeshafikia takriban bilioni 29, tumeambiwa wakati fulani, na sijui kama sio zaidi hivi sasa.

Sasa kama ni hivyo tunajiuliza kuongezeka huku kwa kiasi kikubwa, kwa nini inapokuja uingizwaji wa fedha katika mawizara tatizo ni kubwa, hizi fedha zinakwenda wapi Mhe. Mwenyekiti? Ndipo wananchi wanaposhindwa kutuelewa, wakaona kwamba kumbe hii biashara ya serikali inakuwa ni biashara ya watu kujinufaisha wao, lakini sio kuwapelekea huduma wao Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, ili nifahamike sasa naomba niende katika hizo ripoti zenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya kamati hii ukiiangalia ukurasa wa 17 imezungumzia Tume ya Utumishi ya Idara Maalum, halafu baadaye ikaenda katika idara takriban moja moja. Jambo moja linaloonekana ni kwamba na naomba tuangalie Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 18 kwa mfano, unakuta Idara ya Chuo cha Mafunzo inasema, ripoti ya kamati kwamba inafika kuingiziwa shilingi laki mbili 200,000 ndio matumizi mengineyo kwa Pemba*, other charges(OC's).*

Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini hata Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi hapa akiambiwa anapewa shilingi laki mbili (200,000) atazikataa atasema hazimtoshelezi kuishi maisha yake. Unakipa kikosi kizima kwa Pemba shilingi laki mbili (200,000) kwa mwezi kitekeleze majukumu yake tunategemea ufanisi utoke wapi hapo Mhe. Mwenyekiti.

Hali hii lakini sitaki ku-*create* mijadala, iko katika kila wizara. Sasa najiuliza sisi wengine katika kamati tulikuwa tukiuliza hali ndio imekuwa hivi hivi miaka yote. Tunaambiwa imezidi kipindi hicho. Tunachojiuliza kuna nini serikalini hata inafika pahala matumizi yanakwama kiasi hicho.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, na mimi niseme. Mimi navipongeza sana Vikosi vya SMZ kwa kazi wanayoifanya lakini hali halisi ya maslahi yao ni mbaya sana.

Leo tena unaposoma ripoti hii unagundua bado kamati inaendelea kusisitiza juu ya maslahi yao, yameelezwa Mhe. Mwenyekiti, humu kwamba wanahamishwa pa kukaa hawana, *housing allowance* hawapewi, na sio posho ya nyumba tu Mhe. Mwenyekiti. Nyumba hawana, posho ya nyumba hawapewi, lakini na maposho mengine yote, tunakutana nao mitaani huko wanalalamika kila siku hakuna hata kimoja walichotimiziwa.

Mhe. Mwenyekiti, hawa kila siku wanasema sisi tukilala usingizi, wao ndio wanaokesha kutulinda, tunafanya nini kuwatunzia maslahi yao. Nasema Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa hivyo, yaliyoripotiwa nayakumbuka, na nafikiri aliyesoma ripoti kwa niaba ya kamati leo Mhe. Wanu Hafidh anakumbuka tulikuwa pamoja katika kamati zilizopita, kwamba haya haya tangu tuko sisi tunayarejea mpaka leo tunamaliza miaka mitano, ridhaa ya miaka mitano hii kwa serikali hii inakaribia kumalizika mambo yako vile vile Mhe. Mwenyekiti.

Sasa tujiulize kwamba ikiwa tunakwenda katika hali hii, kweli wananchi munategemea waridhike kwamba fedha zao, kodi zinazokusanywa zinatumika bado hali ya nchi iko vile vile.

Muda Mhe. Mwenyekiti, hautoshi kwenda katika moja moja, lakini nasema ukiangalia idara moja moja inayotajwa humu, utaona ni kiasi gani kwamba mambo ni yale yale yanarejewa kila siku, maana yake ni kwamba hayatekelezwi kila mwaka, na hayatekelezwi kwa sababu kila mwaka tukija ripoti ni ile ile, bado waziri anaripoti mwaka uliopita anasema kwamba atafanyia kazi. Mwaka mzima umefanya kazi gani kama bado unaendelea kufanyia kazi. Hii Mhe. Mwenyekiti, maana yake hufai, na kama hufai ondoka uwapishe wengine wafanye kazi, wasiwe mzigo kwa Mhe. Rais.

Lakini hii Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema nalilaumu Baraza letu wenyewe, kwa sababu gani Mhe. Mwenyekiti? Tungesimama kidete hapa kuhakikisha tunaiwajibisha serikali, nidhamu ingepatikana na haya yasingeonekana Mhe. Mwenyekiti, lakini mengi yanarudi hivi hivi kwa sababu tumeshaonekana ni watu wa kawaida tu hapa, tunakuja tunasema kisha inakuja ahadi nyengine tunapiga makofi tunaondoka, mwakani tunakuja ndio yale yale Mhe. Mwenyekiti, lakini wananchi wetu wanachoka sana Mhe. Mwenyekiti.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, limezungumzwa humu mfano mwengine kwamba ofisi za kufanyia kazi hazina hata mazingira ya kufanyia kazi za idara maalum. Na mimi nikiri hili tumeliripoti tangu tuko sisi kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mpaka leo linarejewa vile vile.

Kwa hivyo, nasema Mhe. Mwenyekiti, unapokwenda kwenye mazingira ya kufanyia kazi. Humu imetajwa kwa Pemba kwa sababu inaonekaka kwa kipindi hiki kamati imefanya kazi kwa upande wa Pemba, lakini ukienda Pemba, ukienda Unguja hali bado mbaya sana.

Nitatoa mfano mmoja Mhe. Mwenyekiti, tunalizungumza tangu tuko sisi na tunalirejea tena sasa katika Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Suala la mazingira ya kufanyia kazi ya Askari wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, pale katika Kiwanja cha Ndege cha Karume Pemba. Mwaka wa tatu linazungumzwa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunajiuliza kwamba kweli tuna nia ya dhati ya kuyamaliza masuala haya.

Ndio maana Mhe. Mwenyekiti, nikisoma mimi ripoti kuna sehemu humu Kamati imekwenda kujifunza katika ukurasa wa 18 na 19 inasema,

"ziara ya kamati ya kujifunza katika Magereza ya Segerea na Ukonga Dar es Salaam"

Mimi najiuliza haya yaliyoandikwa humu namba 1 mpaka namba 9 katika ukurasa wa 19 wanatoa ushauri, kweli tunategemea wizara hii itutekelezee wakati haya ya msingi ambayo kila mwaka tunasema yafanyiwe kazi, hayajafanyiwa kazi tunadanganyana tu Mhe. Mwenyekiti.

Ndio yale aliyosema Mhe. Wanu Hafidh kwa niaba ya kamati. Inafika pahala hata tukienda kufanya ziara za ukaguzi katika mawizara, tunaonekana kama vile tunakwenda kuwapotezea wakati tu, kwa sababu wanatwambia mambo yale yale na tukirudi hakuna yanayotekelezwa tunarudi tena, tunaonekana kama sisi ndio tunakwenda kuhalalisha kwenda kula posho hakuna kinachokuwa, ndivyo wanavyotuona Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, narudia tena kusema kwamba, serikali katika hili inaonekana imeshindwa kazi na kusema kweli mawaziri hawamsaidii Mhe. Rais katika suala hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, pamezungumzwa katika ukurasa wa 23 wa ripoti ya kamati. Hili nitaliunganisha na ripoti ya Mhe. Waziri kabla sijaingia katika wizara nyengine, juu ya suala la Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, hili naomba ninapolichangia nilisome pamoja na maagizo ambayo yalihusu Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, lakini ukweli inahusu takriban Baraza la Manispaa na Halmashauri zetu zote.

Ukurasa wa 5 wa Ripoti ya Utekelezaji au Taarifa ya Utekelezaji ya maagizo ya kamati kwa Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum ya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, pamezungumzwa kwenye agizo namba 4 suala la kamati kuziagiza Halmashauri kuwachukulia hatua za kisheria wanaokiuka taratibu zilizowekwa katika suala la kutupa taka kiholela, uharibifu wa mazingira na masuala mengine.

Lakini soma utekelezaji, mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa uwezo uliopewa na sheria pamoja na sheria ndogo ndogo zilizopo, watazitumia ili kukabiliana na wale wote watakaozihalifu sheria za afya ya jamii na mazingira pamoja na sheria ya mazingira, watazitumia. Hili ni agizo la mwaka Mhe. Mwenyekiti. Mimi nilitegemea tuje tuambiwe katika mwaka uliopita tumefanya nini katika utekelezaji, sio watazitumia na lugha hii ya *wata*, *tuta* ndio iliyojaa katika ripoti za utekelezaji. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hili limefika pahala linakifu. Leo Mhe. Mwenyekiti, nasikitika kusema tulikuwa tukimbana sana alipokuwa Mheshimiwa waziri rafiki yangu Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame, lakini nasikitika kusema hali imekuwa *ahasi* tangu rafiki yangu Mhe. Haji Omar Kheri kakaa kwenye kiti kile. Mji mzima unanuka uvundo kwa taka zisizozolewa.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema mwanzo kwamba, haya tunamuaibisha Mhe. Rais, mara baada ya kuingia madarakani palikuwa na nyimbo katika siku zile bado ilikuwa *TVZ* kabla haijawa *ZBC*, ya mradi wa *ZUSP*.

Mhe. Rais anawekwa kipande pale kabla ya taarifa ya habari anasema miji yetu itang'ara, na hapa katika hotuba ya mwanzo ya bajeti, nakumbuka tulivyopangiwa mipango mizuri ya mradi wa *ZUSP*. Leo mradi wa *ZUSP* umekuja ilikuwa kuna magari ya kukusanyia taka, ajabu magari yale baada ya kuja yanashindwa kunyanyua yale matangi ya kukusanyia taka yameondoshwa, tumejengewa vibaraza taka zinatupwa chini katika karne ya 21 Mhe. Mwenyekiti.

Kila unapokwenda kuna vundo la taka. Leo mataka yale, huku kuna *failure* nyengine ya ofisi ambayo iko chini ya waziri huyo huyo Baraza la Manispaa, suala la kuweka mitaro ya maji safi. Unayakuta maeneo kama ya Michenzani

jaa hapo hapo na makaro yamefuka hapo hapo, yanachanganyika halafu inakuja na mvua ya masika Mhe. Mwenyekiti, nisikilizie tunavyotekeleza utendaji wa serikali katika nchi hii.
Sasa baada ya mwaka mzima unakuja kuripoti kwamba tutayafanyia kazi. Sasa hizi fedha zinazotumika za walipa kodi Mhe. Mwenyekiti, zinafanya kazi gani.

Siku moja Mhe. Mwenyekiti, nateremka nyumbani niliwahoji wafanyakazi wa Manispaa. Wanatwambia sisi hata *overtime* kulipwa hatulipwi Mheshimiwa, lakini hata yale mazingira ya kufanyia kazi, anacheza na taka kwa mikono yake ile hana vifaa vya kumsitiri yeye mwenyewe, hana *mask* wala hana chochote anachezea uchafu ule, lakini na juu *overtime* halipwi. Halafu tunasema tunawadanganya wananchi kuwa tunawatumikia Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ninachosema Mhe. Mwenyekiti, hali mbaya sana na kusema kweli mimi najiuliza sana kwamba hivi rafiki yangu Mhe. Haji Omar Kheri tangu kaja kumepatikana faida gani katika wizara hii. Ndio nikasema kwamba imefika pahala tujitathmini, na tusipojitathmini tumefika mwaka wa mwisho wananchi watatutathmini katika uchaguzi huu Mhe. Mwenyekiti. Tunamuangusha Mhe. Rais, hakuna kitu na kuna suala la mwisho nitalizungumza mwisho Mhe. Mwenyekiti, katika hili wapi wana matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Wizara ya Katiba na Sheria. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, hapa maagizo yale yale yanajirejea. Nimeona humu kuna suala kwa mfano la maslahi ya waendesha mashtaka katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Humu aliposoma ripoti Mhe. Waziri, katwambia kwamba tayari limefanyiwa kazi, sasa sijui nani anasema kweli Mheshimiwa, kwa sababu karibuni mimi nimetembelea Ofisi ya *DPP* baada ya kupewa malalamiko na baadhi yao, nikasema niende nikawasikilize nimeorodhesha Mheshimiwa Mwenyekiti na nikitakiwa naweza kuleta majina waendesha mashitaka *seniors* kumi na moja mpaka pale nilipokuwapo mimi wamehama Ofisi ya Muendesha mashitaka wamekwenda kutafuta kazi sehemu nyengine. Wengine wamo ndani ya hii hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; wako waliokwenda Mamlaka ya Viwanja vya ndege, wako waliokwenda katika usajili wa ardhi, wamehamishwa katika sehemu mbali mbali wanakimbilia maslahi mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, wa mwisho kabisa kaomba katika Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala bora kwa sababu gani, kwa sababu maslahi yaliyokuwepo hayaridhishi, na tulisema zamani Mheshimiwa kwamba tumepandisha maslahi ya Majaji na Mahakimu na hawa waangaliwe, hawa kazi zao pia zinahusisha *risk* ya maisha yao, kwa sababu wanasimamia mashitaka wanaona wenzao wanasonga mbele, wao wameachwa leo wanahama.

Ofisi ya *DPP* nimesikitika kwamba wale waanzilishi Ofisi iliyokuwa inataka kupigiwa mfano ilipoanzishwa leo wanakimbia wamebakia wachache sana katika wale *seniors* waliokuwepo pale.

Sasa humu tunaambiwa kwamba maslahi yao yamerekebishwa, mimi ningeomba akija tupate maelezo ya ziada yamerekebishwa kiasi gani, na kwa sababu bado najiuliza kama ripoti hii ni sahihi ya Wizara, kwamba yamerekebishwa bado naona katika ripoti ya kamati nikisoma Kamati imetoa agizo kwamba bado yaangaliwe upya. Sasa naomba suala hili tuwekewe sawa juu ya maslahi ya Ofisi ya *DPP*, ile ofisi ilikuwa ni mfano wa Zanzibar katika masuala ya utawala bora yanavyopiga hatua, lakini hivi tunavyokwenda itakujakuwa yale mafanikio yaliyofikiwa tumerudi nyuma, hakuna chochote, kwa sababu watu wazoefu wanaondoka.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Waziri anisaidie, tena hili limejitokeza jana tu katika ukurasa wa tisa wa ripoti yake kwenye suala la Kamisheni ya Wakfu, kuna maagizo pale namba mbili. "Kamati inashauri migogoro ya baadhi ya mashamba ya Kamisheni ya Wakfu itatuliwe kwa njia zinazostahiki na hatimaye mwenye haki ya kumiliki mashamba hayo arudishiwe".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa kasema kwamba anaendelea kuyafanyia kazi lakini kuna ugumu sasa ndio nikasema mambo mengine mimi napata tabu kuelewa, kwamba Serikali hii inasimama wapi na inasimamia nini.

Jana Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoka barazani hapa naangalia taarifa ya habari ya *ZBC* nimemuona Mhe. Makamo wa Pili wa Rais anatoa agizo Pemba, kwamba vibango vilivyowekwa na Kamisheni ya Wakfu kwenye shamba la Wakfu ving'olewe kama vinawazuia wananchi kutotumia kwa sababu hili ni shamba la wakfu ili watu waendelee na shughuli zao. Na maelezo yalivyokuwa yanatolewa ni kwamba vile yalikuwa yanamgonga Waziri wa Katiba na Sheria, kwa sababu alisema kwamba ikiwa Waziri wa Katiba na Sheria ni Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi tutajadili katika Baraza la Mapinduzi, sasa nikajiuliza kwamba Serikali hii inafanya kazi vipi Mhe. Mwenyekiti.

Kwamba Waziri wa Katiba na Sheria na Makamo wa Pili wa Rais wanakwenda kugongana hadharani wanaoneshwa katika *TV* ya Taifa *ZBC*, lakini pia nikajiuliza ningeomba Mhe. Waziri akija anisaidie kwamba hivi ninavyokumbuka mimi kuna sheria ya mwaka 2007 ambayo imetoa mamlaka kwa mali zote za Wakfu zirejeshwe katika usimamizi wa Kamisheni ya Wakfu, je, kuna mamlaka ya kiongozi wa siasa kuingilia mali za Wakfu. Nasema hili nimeliona jana, na tumeambiwa kwamba Kamisheni imejitahidi lakini bado kuna ugumu, sasa nimemuona Kiongozi mkubwa wa nchi naye anaingilia kazi za Kamisheni wakati kazi za Kamisheni hizi zimetolewa mamlaka na sheria ya mwaka 2007 ambayo ililetwa ili kuipa mamlaka yale makosa yaliyofanyika nyuma yarekebishwe, kwamba mali za wakfu zirudi katika pale ambapo panahusika ambapo ni kwenye Wakfu na Mali ya Amana. Naomba na hili tuwekewe wazi Mhe. Mwenyekiti.

Jengine ambalo limetajwa katika ripoti ya kamati la Wizara hii nimuombe Mhe.Waziri tumemwambia sana lakini halikutajwa *specifically* katika ripoti ya kamati kwa namna nitakavyozungumza mimi, lakini limetajwa suala la kuendelea kwa tatizo la upatikanaji wa vyeti hivi vya kuzaliwa.

Mara moja Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala tulipokwenda wakati ule alikuwa Mrajis Mkuu wa Serikali kabla haijagawanywa Ofisi ile, alikuwa anatwambia Zanzibar haina sababu katika Afrika kwa nini isiwe nchi inayolingana na Misri kwamba kila raia wake aweze kupata cheti cha kuzaliwa, lakini moja ambalo linakwamisha ni suala la watu wazima ambao hawakuwahi kuchukua vyeti vya kuzaliwa walipozaliwa, na la kwanza ambalo kubwa mbali ya urasimu ni suala la ada kubwa ya *registration.*

Sasa hili tumekuwa tukimuomba Mhe. Waziri sana, kwamba liko katika mamlaka yake lini litarekebishwa, kwa sababu ada yake takriban ni shilingi 35000, kwa mwananchi masikini hawezi ikawa ndio kipaumbele chake cha kwenda kutafuta cheti cha kuzaliwa wakati huku hana chakula yeye na wanawe, lakini bado linakwaza, bado linasababisha upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa usifanikiwe.

Naomba na hilo tusaidiwe Mhe. Mwenyekiti, kwa nini tunaendelea kuomba mambo yale yale hayafanyiwi kazi, kwa nini tusiseme kuwa tumeshindwa kazi Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa ufupi sana kwenye Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma. Katika hili kuna masuala ya maslahi ya wafanyakazi yamezungumzwa na ripoti ya kamati imeendelea kuitaka Serikali iweke wazi masuala haya kutokana na malalamiko yasiyokwisha.
Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka jana tulipokuwa tukichangia tulitaka maelezo humu na mpaka leo yanashindikana kwamba Serikali iliahidi kufanya marekebisho makubwa sana ya maslahi ya wafanyakazi, lakini kilichotokezea wengi wanalalamika kwamba wafanyakazi wengi wa kada za kati na za chini ambao wamefanya kazi muda mrefu sana wamepandishiwa shilingi elfu ishirini na tano (25000), lakini sehemu kubwa ya nyongeza imekwenda kwenye *fungu* kama wanavyosema Waswahili, wamelalamika sana tukienda. Na imeua sana ari ya utendaji kazi kuona kwamba yakija maslahi yanawafikia walio juu kwanza ngazi ya kati na ngazi ya chini hawakumbukwi. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija hilo atupatie maelezo.

Jengine Mheshimiwa imetajwa katika Idara ya Ajira hapa. Katika idara ya Ajira pamezungumzwa masuala ya ajira zinazopatikana nchi za nje na haja ya ofisi hii kuendelea kuwashauri vijana wetu.

Sasa karibuni nilisikia aliporudi Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais kutoka ziara nchini Qatar akitaja katika mkutano wake na waandishi wa habari pale, kwamba kuna suala linaonekana kwamba kulikuwa na makubaliano na nakumbuka haya tangu miaka ya mwanzo 2011/12 Mhe. Waziri wakati ule ni Mheshimiwa Haroun huyu huyu katika Wizara ya Kazi, Uwezeshaji na masuala mengine. Alitwambia kwamba alikwenda na kulikuwa na makubaliano ya Zanzibar kupata *quarter* yake, lakini Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais kaja kuturipotia rasmi kwamba inaonekana kwamba kuna vizingiti makusudi vinafanywa na ndugu zetu wa damu wa upande wa pili Tanganyika, huko katika Muungano inaonekana kupigiwa mfano duniani kwa maslahi mazuri kwa Wazanzibari, wameingilia kati na Wazanzibari wamekuwa hawanufaiki na suala lile.

Wamegeuka *dog in the manger,* mbwa kayakalia majani yeye hayali lakini ng'ombe asisogee. Sasa Mheshimiwa hebu ukija uje kutusaidia, humu kumetolewa maelekezo kwamba iwaelimishe, lakini naambiwa fursa zipo wana hamu sana kuajiri vijana wa Kizanzibari kwa sababu ya utamaduni, silka zetu zinafanana, na historia zilizokuwepo

lakini ndugu zetu wa damu wanatupenda wametuwekea vikwazo. Naomba hebu atusaidie Mheshimiwa hili naona halikuripotiwa.

Na la mwisho kabisa Mheshimiwa ndio katika ile jumla ya masikitiko yangu kusema kwemba hatuko *serious,* ni agizo ambalo liko katika ukurasa wa saba wa ripoti ya Mheshimiwa Waziri, agizo namba tatu.

Kamati kupatiwa mchanganuo wa matumizi ya *e-government* ambayo imeomba muda mrefu bila ya mafanikio. Majibu inasema Wizara imewasiliana na Wizara ya Fedha ili kupata mchanganuo wa matumizi ya mradi wa *e-governmet.* Hiyo Mheshimiwa ni kutuondosha njiani, na hii inathibitisha kwamba kuna uchafu umefanyika hapa, kuna wizi unafichwa, ndio ninavyosema mimi Mhe. Mwenyekiti.

Kwa nini nasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, tangu 2011 tunaomba mchanganuo huo hatupewi, unafichwa nini? Tumeuomba mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba na barua tukaandika tukazungushwa Wizara tatu, tuliambiwa tupeleke Wizara ya Fedha, tukaambiwa tupeleke Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakati ule, tukaambiwa tupeleke Wizara ya Mawasiliano, hakuna mahala tulipopewa mchanganuo wa fedha zile. Fedha takriban dola milioni ishirini.

Imeondoka Kamati ile imekuja kamati nyengine mpaka leo tunamaliza mwaka wa tano, miaka mitano Serikali inayojiita makini inashindwa kutoa mchanganuo wa fedha ambazo naamini zimetumika kwa jambo halali kunafichwa nini.

Ndio niliposema Mheshimiwa mwaka mzima ripoti inakuja kutwambia imeombwa Wizara ya Fedha, huku Wizara ya Fedha tumeshaomba kwa mabarua hatukupewa, ndio maana kuna wakati niliwahi kuomba iundwe Kamati teule, lakini rungu lako Mhe. Mwenyekiti, kwa kutumia mtu mmoja aliyekaa hapo juu akazima hoja ile, ndio nikasema Baraza hili linajitakia, badala ya kufanya kazi ya kuichunguza Serikali sisi kazi yetu imekuwa ni kuilinda Serikali katika matumizi mabovu kama haya.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kusema, na leo namalizia kwa sababu ndio tunaaga mwaka wa tano wa mwisho huu, baada ya miaka mitano kujenga hoja hii kwamba wataalamu waliotambua mambo ya *e-government* wametwambia fedha milioni ishirini haiwezi kufika kwa mradi ule ulivyoendeshwa, kwamba kwa vyovyote labda kama zimetumika zingekuwa dola milioni sita.

Sasa inawezekana hakunambia ukweli lakini ningethibitisha ningepewa mchanganuo kwa nini mchanganuo huo hautolewi. Kama maelezo hayo ni sahihi Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba katika dola milioni ishirini, kama kweli fedha halisi ilipaswa kuwa dola milioni sita tu, dola milioni kumi zilizobakia ukifanya hesabu Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa sawa na shilingi bilioni 25.2 kama kiwango cha ubadilishaji kingetimia shs. 1,800 tu, sasa bilioni 25 Mheshimiwa Mwenyekiti, zingemaliza kiasi gani ya matatizo yetu hapa badala ya kwenda kuwapa *OC's* laki mbili Idara ya Mafunzo wangepewa kiasi gani kama fedha kama hizo zingekuwa zinaokolewa katika nchi yetu Mheshimiwa Mwenyekiti.

Lakini ndio *collaboration,* mashirikiano baina ya watendaji wetu na hao wanaoambiwa wanatoa mikopo, na ndio maana hatuwezi kutoa michanganuo. Tumeuomba mwaka 2011 umekwisha, tumeomba 2012 umekwisha, tumeomba 2013 umekwisha, tumeomba 2014 umekwisha, tunaomba tena 2015 tunaambiwa bado Wizara inaiomba Wizara ya Fedha, hakuna majibu Mheshimiwa, watu wametafuna fedha Mheshimiwa Mwenyekiti wanafichiwa.

Mimi ndiyo *conclusion* yangu leo baada ya miaka mitano kwamba Serikali haina majibu mengine, kwamba imeshindwa kutupa miaka mitano mchanganuo mradi mmoja tu. Mhe. Mwenyekiti haya ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi, na *ishaallah* wananchi wa Zanzibar wataihukumu Serikali yetu tukijaaliwa. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tunao muda wa nusu saa, sasa kama kuna mjumbe yeyote anataka kuchangia. Karibu Mheshimiwa Abdalla Mohamed Ali.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi magharibi haya kupata fursa ya kusema machache katika ripoti hizi zilizowasilishwa mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, waswahili wana msemo wao wanasema kwamba *sitaki niumize kisu changu kwa mnyama asiyeliwa*, wengi wameshasema hapa na tunarejea yale yale tu kwamba kila siku tunakumbushana, lakini utekelezaji sijui uko mbali na sisi. Mimi nataka nianzie na hapa ambapo Mhe. Ismail Jussa Ladhu amemalizia na kuhusu kamati kupatiwa mchanganuo wa *e- government.*

Huu ni mradi ambao ulianzishwa na Serikali kama miaka mitatu iliyopita nyuma, na kila siku zinavyoendelea hautajwi, haupo tena katika mawazo ya Serikali. Sasa labda mimi niulize tu, hivyo upo hai huu mradi, na kama upo hai kuna fungu lolote la kuuendeleza kama haujamalizika, au upo jina tu umesimama hivi sasa haufanyi kazi tena na labda Serikali inautaka mradi huu uendelee.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hivi sasa bajeti zetu zinaelekezwa katika mpango wa *PBB Program Based Budget;* na hii ni moja katika *program* iliyoainishwa na Serikali, sasa je, *program* hii Mheshimiwa Waziri imefikia hatua gani, na inataka kuendelezwa ifikie tamati au imemalizikia njiani? Naomba ungetupatia maelezo kuhusu mradi huu Mhe. waziri kama upo tujue bajeti inakuja tuunge mkono namna gani au umekufa.

Jengine Mhe.Mwenyekiti, ni kuhusu vizazi na vifo kama Mheshimiwa alivyosema kwamba taratibu hivi sasa zinaonesha kwamba ni sheria katika nchi yetu kupata usajili wa kizazi na kifo lakini imekuwa ni usumbufu mkubwa. Kila unapoelekea katika idara hii inayohusika na usajili wa vizazi basi hujui uanzie wapi. Nafikiri hivi sasa tumeanzisha Serikali za Mitaa na nyenginezo ili kurahisisha utawala na uongozi, sasa nahisi umefika wakati ili kuondoa usumbufu huo basi haya mengine tukayaondosha sehemu moja tukajaribu kuyasambaza sehemu tofauti. Nashangaa sijui ni kipengele gani kinachohofiwa hata ikawa wananchi bado wanasumbuka, ukienda hiyo Ofisi yenyewe hujui hata utie mguu wapi, hujui mhusika wa kuanzia ni yupi. Kwa hivyo nafikiri hivi sasa kungeangaliwa utaratibu mwengine.

Kuna taratibu Serikali inaweza ikafanya kuanzia hospitali pale pale wakatoa, nini wanachoogopa, Sheha yupo anayeaminiwa, nini wanachoogopa hata ikabidi mtu ahangaike kutafuta usajili jambo ambalo limeainishwa katika Katiba yetu ya nchi, nafikiri taratibu zingebadilishwa, usumbufu tunaoupata ni mkubwa katika kutafuta kusajili mtu yaani kizazi chake.

Mhe. Mwenyekiti, nije jengine kuhusu Idara hii ya miundo ya taasisi. Mimi napata shida sana kwamba kuna baadhi ya watumishi ambao wanakuwa wao wanafaidika zaidi, na baadhi ya watumishi ambao hadi hivi sasa wanahangaika.

Mwenyekiti ukija katika kada ya ualimu unakuta walimu wengi hivi sasa wanapewa likizo ambao wanastahiki wapewe na huduma lakini bado anapata barua tupu inayomuelekeza yeye aende katika likizo tu lakini huduma asubirie, lakini ukija katika mamlaka na Idara nyengine za Utumishi unakuta wao wakipewa barua ya kwamba yeye aende likizo basi na huduma yake ambayo anastahiki wakati ule ameshatimiza miaka mitatu anaipata. Sasa sijui idara hii inalifikiria vipi suala hilo, kwa nini watumishi wengine wapatiwe maslahi yao lakini watumishi wengine wa umma wakawa wanachelewa zaidi ya watumishi wengine.

Pia Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hivi sasa nilitarajia labda idara hii ingekuwa na kipimo maalum cha kujua maslahi ya nchi hivi sasa nchi inahitaji nini. Ni aibu kuona kwamba tunatumia fedha za Serikali kuwakopesha vijana wetu kwenda masomoni vyuo vikuu, lakini wanaporudi ajira yake au kupata ajira kwa ajili ya kurudisha zile fedha ambazo kakopeshwa anachukua miaka mitatu minne, sasa sijui kuna mpangilio wowote huko Serikalini ambao Idara hii inauweka, kwamba sasa hivi Serikali inahitaji fulani, kwa hivyo tukamsomeshe zaidi fulani, huyu tumpe *priority* kwamba sasa tunahitaji kitu hiki, au tunakwenda bila ya mpangilio maalum, hakuna *priority* yoyote inayoonesha, kwa maana hiyo unakuta watu wanazubaa waliosoma vyuo vikuu fedha zinataka kurudishwa katika mfuko wa elimu ya juu lakini matokeo yake watu hawapati ajira.

Sasa nafikiri imeshafika wakati sasa ya kujua nchi inahitaji maslahi gani hivi sasa tuyashughulikie, si hivyo siku zote tutakuwa tunakwenda ovyo, pesa tunazitumia ovyo na hatuna tunachokifanya kwa maendeleo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, labda jengine ni kuhusu uhamisho hasa hawa watumishi wa Idara maalum. Ni aibu kuona kwamba mtu amehamishwa kutoka kisiwa kimoja kwenda kisiwa chengine anapewa shilingi elfu arubaini (40,000) nauli ya kwenda na kurudi, wao ni watumishi wa umma kwa nini sasa wapewe kiwango kama hicho. Watumishi wengine wanapewa huduma zote zinazohitajika katika kumuhamisha kutoka sehemu moja kwenye sehemu nyengine

au kutoka kisiwa kimoja kwenda kisiwa chengine cha kazi, lakini watumishi hawa wanagaiwa nauli asubuhi elfu ishirini kapande Maendeleo nenda zako, hana huduma nyengine yoyote anayoipata. Hapa huhisi kwamba Mhe. Mwenyekiti, pana ubaguzi wa watumishi wa umma, wengine wanafikiriwa wanapewa haki zao na wengine hawapewi haki zao inavyotakikana. Nafikiri sheria lazima itumike kwa pande zote mbili.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala jengine la nyaraka. Nafikiri ule umuhimu hasa wa nyaraka nchi yetu haijajua nini umuhimu wake. La kusikitisha kwamba unapokwenda katika idara hii unakuta hizo nyaraka zenyewe zilivyotunzwa ni aibu kusema kweli.

Nafikiri watu wengi tunatoka hivi sasa kwenda kutembea katika nchi mbali mbali. Tunaona jinsi gani wenzetu wanavyotunza nyaraka zao. Hapa kwetu ukienda sasa nafikiri wa makaratasi ni mchwa pale, wanakuwa ndio rafiki zao. Makaratasi yapo ovyo Nyaraka pale, hujui mwanzo wapi, hujui mwisho wapi. Kunahitajika hivi sasa twende katika viwango vya kimataifa, kwa sababu tunapata wageni kutoka nchi nyingi kuja kujifunza na kujionea historia yetu.

Mhe. Mwenyekiti nafikiri kwa hayo machache nimalizie hapa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa na mimi jioni hii kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Katiba na Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi napenda niwasifu sana Wajumbe wa Kamati kwa kufanya kazi vizuri, lakini pia mimi nina masikitiko kidogo kabla ya kuingia kwenye michango. Mheshimiwa tunakuwa tunafanya kazi kila siku suala hili tunalizungumza. Tunafanya kazi mwaka mzima kutafuta kazi za serikali yetu, yaani kuielekeza serikali, kuisindikiza serikali katika utekelezaji wa kazi, pamoja na kuangalia bajeti tunayoipitisha ya mwaka ili ufanisi wa utendaji kazi.

Mhe. Mwenyekiti, tunafanya kazi mwaka mzima lakini tukija katika Kamati uwasilishaji wa Kamati mimi naona tunafanya kama mchezo. Kwa sababu mwaka mzima tunaofanya kazi tunakuja tukipitisha kazi za Kamati za mwaka mzima ambazo tumefanya kazi za kwenda hapa na pale, kufanya kazi kuangalia lakini utekelezaji tukija tunapitisha kwa nusu dakika tu. Nusu dakika tunapitisha ripoti za Kamati tunamaliza, haiwezekani, wizara tatu zote saa hizi tuzifanyie kazi kwa wakati mmoja na wakati hasa ukizingatia kama ripoti zote tumezipata jioni ya leo.

Sasa jioni ya leo hizi tunazozipata Utekelezaji wa Kamati ni jioni tu hatujazisoma tukazifanyia kazi vizuri. Wajumbe wako ndio unaona wanasuasua. Kwa hivyo Mheshimiwa tunapofanya kazi mwaka mzima, tuachiwe tufanye utekelezaji wake tutoe ripoti zetu kwa kuendelea kwa ufanisi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa napenda niendelee kutoa michango yangu katika kazi hizi za Kamati. Kwanza kabisa mimi naomba nianze na hii Katiba na Sheria lakini niende kwenye Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

Mhe. Mwenyekiti, wametoa mapendekezo hapa Wajumbe wa kamati. Kamati imetoa maagizo na bahati nzuri Kamisheni yenyewe imepokea maagizo ya kamati, imefafanua vizuri. Mimi napenda niwasifu kwanza na wao kama wanafanya kazi zao kwa uadilifu na wameelezwa na Kamati kama waangalie ile misikiti ambayo kuwa ni ya zamani waitunze pamoja na kuangalia misikiti ambayo kuwa ina sehemu zilizokuwa zina watu masikini zaidi waziangalie.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza napenda niwaunge mkono Wajumbe wa Kamati kama hili linastahiki. Mara nyingi mimi nikichangia nafikiri kama mara mbili kwenye bajeti nimeshasema na leo nitasema tena. Kama hili ni uhakika kwa sababu katika nchi yetu hii ya Zanzibar kuna sehemu ambazo kuwa kidogo angalau zina nafuu kama sehemu za mijini lakini sehemu za vijijini zinakuwa na matatizo zaidi.

Mhe. Naibu Spika, hii Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana naomba iangalie sana wakati wa kujenga hii misaada, wanakuja watu na misaada yao kutoka sehemu mbali mbali. Wanapokuja kutoa misaada aidha ya kujenga misikiti, madrasa na mambo mengine, naomba sana waangalie sehemu za vijijini. Huku vijijini kuna waumini, tena na wao ni wasalihina ni watu wenye dini kama mijini. Lakini jamani mijini kila siku mnataka kujenga misikiti mikubwa mnataka kuoneshana kushindana kujenga misikiti mijini tu.

Kwa hiyo naomba sana hii ripoti wanayoitoa ya Kamati, rai wanayoitoa ya kamati kama tuangalie na vijijini. Sasa nawaomba sana waangalie vijijini na wao pia wanataka kusaidiwa. Mijini misikiti *alhamdulillah* tunayo ya kushindana hasa, kila pahali ukisema kuna msikiti mkubwa zaidi kuliko pahali fulani. Kwa hivyo sasa umefika wakati wa kuangalia na vijiji vikasaidiwa. Kwa sababu kuna watu ambao kidogo hali zao ziko dhaifu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati huo huo wanatakiwa wao ingawa ni kazi yao wameambiwa hapa watoe elimu kwa taasisi zinazopeleka watu Hijja. Si kutoa elimu kwa Taasisi, watoa elimu, watoe na rai kwenye vyuo vyetu vya Qur-an ili kusaidia kukuza, hiyo dini yetu ya Kiislamu yaani elimu yetu ya Kiislamu ili kukuza na kuwapa motisha watu ili wafanye kazi zaidi katika kutekeleza kazi hizi, lakini katika wizara hii nikiondoka hapa nije kwenye suala alilozungumza mwenzangu aliyekaa kitako.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye vizazi na vifo, hili suala linatakiwa na tumeshazungumza mara nyingi sana kwamba jamani tunaiomba serikali yetu kupitia hii taasisi, iangalie uwezekano. Sasa hivi tunapata tabu sana, watu wanazaliana lakini vyeti wana muamko navyo ni tofauti kabisa na siku za nyuma. Sasa kama watu wana muamko na vile vyeti viwe vinapatikana kiurahisi. Inawezekana mtu akachukua mwaka mzima anasubiri cheti hakipati. Ukiachana na watoto, hao watoto wanaweza kutimiza miezi mitatu, minne, sita, kipindi kikubwa hiki tulikuwa tuna tatizo la magamba. Magamba yale ya vyeti hayapatikani, yalikuwa ni haba sana yanayopelekwa mawilayani, kwa hiyo kulikuwa na mrundikano wa vyeti.

Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu ifanye kazi kuondoa matatizo haya madogo madogo na ndio ushauri tunaoutoa kila siku. Sisi kazi yetu ni kuielekeza serikali kuishauri. Tunaomba sana katika ripoti tunazozisoma kama serikali izitekeleze ifanye kazi, ili matatizo hayo yaondokane.

Moja tulilolizungumza kuhusu vyeti tulizungumza kwamba sasa hivi mtu akiwa huku nyuma kulikuwa muamko wa vyeti hakuna, kwa hivyo kuna baadhi ya watu walikuwa hawana sasa hivi wanavitaka na ni muhimu kuvipata. Kwa sababu kama unataka *passport* huwezi kupata *passport* kama huna cheti cha kuzaliwa. Sasa ni muhimu kila mtu kukipata hichi cheti.

Mhe. Mwenyekiti, sasa serikali lazima ifanye jitihada,. Pia tulisema kwamba wapunguze bei za vyeti. Mtu mmoja akikipata cheti gharama zake mpaka sasa kama ni mtu mzima zaidi ya shilingi arubaini elfu. Anakwenda kutafuta hati ya kiapo kwanza kule, akipata fomu kwenye hati ya kiapo hata akikamilisha, akija akitafuta cheti basi zinafika shilingi arubaini elfu au thalathini na tano elfu. Kwa hivyo Mheshimiwa tunaomba sana serikali na hili ilione na ilifanyie kazi ili watu wapate kidogo nafuu. Masikini ya Mungu wengine shilingi arubaini elfu kwa siku ni kazi kuzipata, anachukua mwezi kuzitafuta kwa hiyo akishapata zile pesa zake kidogo haweze kupata cheti ili matatizo yake mengine yaondoke.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo kwenye suala hili sasa naingia kwenye suala la upande huu wa Tawala za Mikoa. Mheshimiwa maagizo pia kuna maagizo ya Kamati yanayotolewa na wao pia kama nilivyokwambia nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati wamefanya kazi nzuri. Wana maagizo mengi na wana ushauri mwingi wanaoutoa. Wajibu wetu ni kuufanyia kazi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, haya maagizo ya Kamati tuyasimamie ili tuone kama maagizo yanayotolewa yanatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona hapa katika ripoti ya Kamati katika suala la Tawala za Mikoa humu. Kuna maagizo yametolewa kwamba Waheshimiwa sasa hivi kutokana na udogo, wao wametumia neno kutokana na uhaba, lakini mimi nasema udogo sisemi uhaba. Nasema kutokana na udogo wa ardhi yetu tuliyonayo Zanzibar wamesema sasa hivi serikali lazima iangalie watu wa mipango miji, pamoja na serikali yetu ipange ili utumiaji wa ardhi yetu uwe ni utumiaji mzuri wa ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, wameagiza kama kuna sehemu ambazo ni sehemu za mawe kwa mfano kama Micheweni na maeneo mengine Tunguu na kwengineko, basi hizo iwe ndio sehemu za kujenga nyumba, lakini zile sehemu ambazo ni sehemu za kilimo basi zile zisiwe sehemu za kuweka miji iwe ni sehemu za kilimo. Mimi naungana nao na nakubali sana. Ukiangalia kutokana na udogo wa ardhi tuliyonayo, tukijenga zile sehemu ambazo kuwa za kilimo, mwisho watu watakuwa hawana sehemu za kulima.

Hili linatakiwa nalo lisimamiwe kwa nguvu zote kuona kwamba sasa hivi mipango miji inapangwa miji. Watu wa Halmashauri za Wilaya na wao watu wa Halmashauri hawasimamii suala la mipango miji. Halafu hizo sehemu

ambazo kuwa zinajengwa hazisimamiwi. Ndio maana ukaona katika mipango miji yaliyokuwemo katika Halmashauri za Wilaya zinakaa tu shaghala baghala shaghala baghala.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano tukiangalia kama masoko yetu tuliyonayo kama soko la Wete lile, watu wa Halmashauri ya Wilaya ya Wete wameshindwa soko lile kulihudumia mpaka leo hii, ukifika pahala kwenyewe pachafu, hapana maana yoyote ile. Hii ni kukosa kupanga, na kama kweli wanapanga basi pale wangepasimamia ikawa kidogo pana unafuu. Lakini hali ile iliyokuwepo, halafu huku tunapanga miji, huku zile sehemu tulizonazo kwenye miji tunakuacha kunaharibika. Sasa kama lile soko vile lilivyo hiyo mipango miji tunakwenda kupanga kwengine lakini mle ambamo kuwa tunamo tunakuacha hakusimamiwi.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri anayehusika na hizi Halmashauri za Wilaya azisimamie Wilaya zake katika masuala haya ya mipango miji na wao wanahusika wasimamie kuangalia mipango yao ya miji yao.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ninalotaka nilizungumze katika suala hili ni suala la hao hao watu wa Halmashauri. Nia ya serikali ni kukusanya mapato, katika Halmashauri zetu zinakusanya na tunazisifu kuwa zinakusanya na ndivyo tunavyotaka kuwa zikusanye na tutumie, lakini makusanyo yanayokusanywa yasikusanywe mpaka yakabidi kuwanyonya wananchi wetu mpaka wakawa hawawezi hata kufurukuta, lazima tukusanye tukiwaangalia na wao. Tusikusanye ikawa tunawanyonya moja kwa moja.

Nataka nitoe mfano, kama Halmashauri ya Wilaya yangu ya Micheweni, inakusanya mapato kupitia pale pana Halmashauri ya Wilaya, pana Misitu, pana na watu, wengine wote wanakusanya mapato sehemu moja, lakini pale makusanyo yenyewe yanayo uhakika sana pana pita mawe, matofali, chokaa, kokoto na mambo mengine. Leo masikini ya Mungu wale madereva pamoja na wale wafanyakazi waliomo garini wote wanategemea kipato chao ni kile kile, waende wakachukue shehena ya mawe wapeleke na wao wapate kipato.

Lakini gari kama inakwenda gari moja kama itakuwa ina tripu nne basi lazima iandikiwe risiti nne kwa siku moja. Na kila Shehena moja inayopita shilingi elfu saba. Hivi kama gari itakuwa inakwenda kuchukua tripu kumi siku ile anakwenda kulipa shilingi sabini elfu. Sasa je, wao wale wananchi tunategemea wapite wapi. Maana tukishakuwa tunakusanya ni sawa kusanya na ndivyo ilivyo tukusanye, lakini lazima na wao tuwaonee imani. Kule kukusanya kwetu, tukusanye na wao wajue. Gari moja inakusanya shilingi sabini elfu kwa kwenda kuchukua mawe wao wapate wapi. Naomba sana na hili lizingatiwe kwamba katika kukusanya tukusanye lakini tukiwaangalia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine wanavyoeleza humu katika maagizo waliyoagiza Kamati hii, wameelekeza kwamba ziangaliwe sehemu zile zinazochimba mawe, zinazochimba michanga ili tusiendelee kufanya uchafuzi wa mazingira na uharibifu mkubwa wa mazingira. Ni vizuri sana na wamejenga sana, lakini Mheshimiwa bado nasema Manispaa ya Jiji la Zanzibar na wao wanachangia uchafuzi wa mazingira na uharibifu wa afya za binadamu wanachangia. Kwa nini niseme hivyo.

Mheshimiwa katika Baraza hili kama kuna mtu anayepiga kelele kwa jaa lile la Darajani ama mimi naongoza kwa kupiga makelele na bado nitaendelea kupiga makelele na kusema. Mheshimiwa lile jaa pale ndio sura ya Mji wetu. Jaa lile kukaa pale halifai.

Mheshimiwa pale pana Mahoteli, pale ukienda ukila chakula pale *wallahi* utatamani ukiache. Mimi nimeshakula siku moja sijaenda tena na wala siendi tena. Mheshimiwa pale pananuka kama kidonda, Mji wetu unanuka kama kidonda. Hivi lile jaa kuondoka pale mnaona hasara ya nini? Pale ndio uso wa sura yetu ya Zanzibar, wageni wote wanakwenda pale.

Mhe. Mwenyekiti, lile jaa, pale tunaharibu hadhi yetu na hasa kipindi hichi kinachoingia cha mvua, tunaweza tukapata maradhi ya miripuko. Kama ni uharibifu wa mazingira pale pana uharibifu wa mazingira mkubwa. Lile jaa halifai kuwepo pale, pananuka pale huwezi kupita mara mbili, hata kama kuna gari basi hata ukifunga vioo basi harufu inaingia. Mheshimiwa kwa nini lile jaa mnaona hasara kuliondoa pale. Ule ni uchafuzi wa mazingira kwa sababu harufu yote inawaingia watu na sio uchafuzi wa mazingira tu na afya za watu tunazisababishia kuharibika.

Mhe. Waziri nakuomba sana fanya iwezekanavyo lakini jaa lile pale liondoke, pale hapafai kuwepo lile jaa liondoke. Hapa tulipiga kelele siku za nyuma lilikwenda likafanywa jaa Skuli ya Jang'ombe, tukapiga kelele kwa jaa lile, kama hivi tukisema tunaiomba itusikilize na sisi. Kwa sababu tunayoyasema tunasema kwa faida yetu na faida ya

wananchi wetu. Sisi tukisema mambo mengine tunakuwa tumeshasikia kwamba inatuondoshea sura ya mji wetu, wale watalii watatudharau wakija, pale watatudharau sana.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia, muda unamalizika sasa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nataka nilizungumze ni kwamba Kamati ilipotembelea katika Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi ilitoa taarifa kwamba wanajitahidi kukusanya mapato lakini wakasema kwamba wao yale mapato yao wanayokusanya mapato yale yale. Yaani vile vyanzo vyao vya mapato basi na *ZRB* inataka ikusanye au yakusanye kutokana na vyanzo vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana pamoja na kuwa Waziri amesema hapa kama kutokana na hali hiyo ya kukusanya mapato ikawa vile vyanzo vina mgongano baina ya Wizara hii na taasisi nyengine. Wakasema kwamba katika sheria hii iliyopo ya Serikali za Mitaa wamejitahidi kuondoa migongano.

Kwa hiyo na mimi hapa ushauri wangu ninaotaka kuutoa ni kwamba namuomba Mhe. Waziri atumie fursa hii kuondoa hii migongano ya makusanyo ya mapato ambayo kuwa ni Vyanzo vya Mapato vya Halmashauri na hii *ZRB* katika kukufanya mapato hayo, kwa hiyo ajitahidi sana kuondoa hii migongano ili makusanyo ya watu wa Halmashauri waendelee kupata makusanyo yao, lakini na *ZRB* waendelee kukusanya kutokana na vyanzo vyao vya mapato.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu umenambia muda umeshamaliza, ilikuwa niendelee lakini *Inshaallah* kwa hapo ninapofika nitawaachia na wenzangu waendelee. Nakushukuru sana na naunga mkono ripoti hii ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru leo kwa michango yenu na tukijaaliwa *Inshaallah* kesho tutaendelea na michango. Kwa hiyo naahirisha kikao hadi kesho asubuhi saa 3:00 tarehe 18/03/2015.

(Saa 1:40 jioni Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 18/03/2015 saa 3:00 asubuhi)